**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA SABA**

**Kikao cha Saba - Tarehe 18 Aprili, 2007**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Naibu Spika ( Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua*

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:**

Taarifa ya Ishirini na Moja ya Utendaji na Hesabu zilizokaguliwa za Bodi ya Tumbaku Tanzania kwa Mwaka wa Fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2006 *(The 21st Annual Performance Report and Audited Accounts of the Tanzania Tobacco Board for the Year ended 30th June, 2006)*

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA):**

Taarifa ya Mwaka na Hesabu ziliozokaguliwa za Bodi ya Usajili wa Wahandisi kwa Mwaka Ulioishia tarehe 30 Juni, 2006 *(The Annual Report and Audited Accounts of the Engineers Registration Board for the Year ended 30th June, 2006.*

**MWENYEKITI WA KAMATI YA HUDUMA ZA JAMII:**

Taarifa ya Kamati ya Huduma za Jamii kwa Mwaka 2006.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA FEDHA NA UCHUMI:**

Taarifa ya Kamati ya Fedha na Uchumi kwa Mwaka 2006.

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 83

**Ofisi ya Waziri Mkuu**

**MHE. PAUL P. KIMITI** aliuliza:-

Kwa kuwa Mji wa Sumbawanga umepata hadhi ya kuwa Manispaa kamili:-

(a) Je, Serikali inasema nini juu ya uendelezwaji wa jengo la Ofisi ya Manispaa ambalo limetengewa fedha kidogo?

(b) Je, Serikali haioni ni vema kwa Mji huo kupatiwa fedha za kutosha mwaka ujao wa fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara za mjini kwa awamu ya kwanza ili kuwavutia makandarasi kwenda huko badala ya kuwapa tenda ndogo ndogo za kilomita 2 – 3 ambazo ni kidogo kwa kampuni zilizoko mbali na Sumbawanga kuja kwa fedha kidogo?

(c) Je, ni nani atahusika na kusimamia ujenzi wa barabara hizo za lami katika miji mbali mbali ili kuridhika kuwa fedha za wahisani zinatumika kulingana na kazi zilizofanywa ili kukwepa wizi au rushwa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba, kujibu swali la Mheshimiwa Paul P. Kimiti, Mbunge wa Sumbawanga Mjini, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga ilikuwa na Ofisi katika majengo ya shule iliyokuwa *Middle School*. Majengo hayo yalichukuliwa na kuwa Shule ya Sekondari Sumbawanga mwaka 2003 na Ofisi za Manispaa zilihamia katika Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Rukwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuanzia mwaka 2005, Manispaa ya Sumbawanga iliamua kuanza ujenzi wa jengo la Ofisi linalotarajiwa kugharimu jumla ya shilingi bilioni moja litakapokamilika. Taratibu za kumpata Mkandarasi zimefanyika kwa kutangaza tenda. Mkandarasi aliyepatikana ni *Southern Link Limited Building and Civil Contractor*. Aidha, Mshauri ni *Tanzania Building Agency.* Hadi Machi, 2007 Mkandarasi amelipwa shilingi 318,484,865/= ambazo kati ya hizo Serikali Kuu imechangia shilingi 226,000,000/= na Halmashauri imechangia shilingi 92,484,865/=

Mheshimiwa Naibu Spika, jengo hilo ni ghorofa na nguzo za ghorofa moja zimeishajengwa. Katika mwaka wa fedha 2007/2008 ujenzi wa ukuta utaendelea. Halmashauri imetenga shilingi milioni 100 kutoka kwenye vyanzo vyake vya mapato na imeomba Serikali Kuu shilingi milioni 500 kwa ajili ya ujenzi huo. Jukumu la kujenga Ofisi ya Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga ni la Manispaa yenyewe. Hivyo,

naishauri Manispaa hiyo kuendelea kuweka katika kipaumbele ujenzi wa jengo hilo kila mwaka ili likamilike kwa wakati unaotakiwa.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, kujenga barabara kwa kilomita 2 – 3 kwa kiwango cha lami kunagharimu kati ya shilingi milioni 800 – 900. Aidha, Halmashsuri ikifanikiwa kujenga kilomita 2 – 3 za lami kwa mwaka ni hatua kubwa ya maendeleo kuliko kukaa na kusubiri fedha nyingi ambazo si rahisi kupatikana. Ofisi yangu imepokea maombi ya shilingi 3,532,429,500/=, kutoka Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga ili kujenga kilomita 11.55.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha hizi ni nyingi kutolewa kwa fedha za mradi wa maendeleo ya barabara kwa mwaka mmoja na si kwa Manispaa ya Sumbawanga tu. Maombi yote yamewekwa kwenye *databank* na kusubiri fedha zitakapopatikana. Hata hivyo, Halmashauri inashauriwa kuendelea kuzifanyia ukarabati barabara hizo ili ziendelee kupitika kwa urahisi wakati wote.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, katika kila Halmashauri kuna wataalam kwa maana ya Wahandisi wa Halmashauri. Aidha katika Sekretarieti za Mikoa kuna Wahandisi Washauri. Katika kuhakikisha kuwa fedha zinazotolewa zinatumika vilivyo, wataalam hawa watasimamia ujenzi wa barabara hizo. Pale inapobidi, wataalam wa Halamashauri na Mkoa wanaweza kuomba ushauri kutoka Wahandisi wa *TANROADS* waliopo katika kila Miji yote ya Mikoa husika.

**MHE. PAUL P. KIMITI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kushukuru kwa majibu ambayo Mheshimiwa Naibu Waziri ameyatoa. Lakini, nina maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa tamko la Mheshimiwa Rais tangu alipoingia madarakani, alitoa agizo kwa Serikali yote ya kwamba kipaumbele sasa kitakuwa katika Mikoa ile yote ya pembezoni na kuipa kila aina ya msaada ili kuweza kufanikisha katika malengo yao. Mkoa wa Rukwa pamoja na Mji wa Sumbawanga, kwa kipindi cha miaka 25, hata kilomita moja ya lami haijajengwa. Je, Waziri haoni ya kwamba matamshi aliyoyatoa hayaendani sambamba na maagizo ya Rais katika Mikoa ambayo iko nyuma?

Pili, Uwezo wa Manispaa na Halmashauri ya Mji wa Sumbawanga, Mheshimiwa Waziri anaufahamu ya kwamba ni mdogo na kama tutategemea vyanzo vya Halmashauri yenyewe kujenga ghorofa la shilingi bilioni moja. Je, haoni kwamba kwanza itachukua muda mrefu, halafu itafikia mahali fulani ambapo gharama yake itafika hata zaidi ya bilioni 3 na ikizidi kuingiza mzigo kwa wananchi na walipa kodi kwa ujumla?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kama alivyosema, Mheshimiwa Rais katika kauli zake nyingi, ameahidi kwamba Mikoa ya pembezoni itapewa kipaumbe. Mipango hii ya kupewa kipaumbele ipo. Kwa mfano, kwa Manispaa ya Sumbawanga, kama nilivyojibu katika jibu langu la mwaka jana kuhusu upande wa barabara kwamba upande wa Sumbawanga kwa mwaka 2007/2008 imewekwa kwenye kipaumbele cha ukarabati au utengenezaji wa barabara ya Manispaa ya Sumbawanga na nilitaja baadhi ya Mikoa ambayo itapewa kipaumbele. Nilisema kwamba, mpango huu

unaanza mwaka 2007/2008. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Mbunge awe na subira kwa upande huu wa barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ujenzi wa majengo ya Manispaa, kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi kwamba Manispaa yenyewe itoe kipaumbele kwanza kwa ujenzi wa majengo haya. Pili, Serikali Kuu pia inasaidia katika ujenzi huo wa majengo. Kwa hiyo, naomba Manispaa wahakikishe kwamba wamepanga kiasi fulani katika ujenzi wa hilo ghorofa na Serikali Kuu itasaidia pia kuongezea kiasi fulani kulingana na uwezo wa kifedha. Mimi nina uhakika tukifanya hivyo, tutakuwa tumetatua hilo tatizo la ujenzi wa ofisi za Halmashauri.

Na. 84

**Utendaji Mbovu Katika Halmashauri**

**MHE. VEDASTUSI M. MANYINYI** aliuliza:-

Kwa kuwa utendaji mbovu unaozikumba Halmashauri zetu ikiwemo Manispaa ya Musoma, unatokana na upungufu wa wataalam na watumishi wetu na mlolongo mrefu wa vibali vya ajira:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha maslahi ya watumishi wa Halmashauri ili waweze kuleta tija katika kazi?

(b) Je, Serikali itarekebisha vipi huo mlolongo mrefu wa utoaji wa vibali vya ajira?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijajibu swali la Mheshimiwa Vedastusi M. Manyinyi, Mbunge wa Musoma Mjini, napenda kutoa maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, maslahi ya watumishi wa umma ikiwa ni pamoja na mishahara yamepangwa kwa kuzingatia sifa za kielimu, kitaaluma, uwezo na uzoefu kama ilivyoainishwa kwenye miundo ya utumishi wa kada mbali mbali. Maslahi haya yamekuwa yakiongezwa mwaka hadi mwaka kulingana na hali ya uchumi inavyokuwa.

Pia, suala la ajira linadhibitiwa na Serikali ili kuepuka kuwa na watumishi hewa. Aidha, idadi ya watumishi waliopo na wanaoajiriwa inategemeana na Ikama ya Halmashauri iliyopitishwa na Halmashauri yenyewe na kupata kibali toka Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kutoa maelezo hayo, sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inajali sana maslahi ya watumishi wake ikiwa ni pamoja na kuboresha mishahara kwa watumishi wa Serikali za Mitaa. Kwa kuanzia Serikali imeongeza Mishahara ya Wakurugenzi wa Halmashauri na Wakuu wa Idara na kwa sasa wanapata mishahara ya kuridhisha sawa na Wakurugenzi na Wakuu wa Idara wa Serikali Kuu.

Katika juhudi za kuendelea kuboresha maslahi ya watumishi wa Serikali za Mitaa, kati ya Mwezi Desemba 2005 – Julai, 2006 Serikali ilitafuta Mtaalam Mshauri ambaye alifanya tathmini ya kazi katika Serikali za Mitaa. Lengo ni kujua watumishi wa Serikali za Mitaa wanastahili kulipwa mishahara ya kiwango kipi kulingana na uzito wa kazi zao. Tathmini imekamilika na imekabidhiwa Serikalini kwa hatua zaidi. Aidha, Mheshimiwa Rais aliteua Tume ya kupitia na kupendekeza mishahara na maslahi ya watumishi wa umma ikiwemo watumishi wa Serikali za Mitaa na taarifa hii imekwishawasilishwa Serikalini na inafanyiwa kazi. Taarifa ya Tume ya Rais imezingatia maoni na mapendekezo ya taarifa ya Mtaalam Mshauri wa Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba hatua zote hizi zinachukuliwa na Serikali, zina lengo la kuboresha maslahi ya watumishi wake wakiwemo wale wa Halmashauri ili waweze kuleta tija katika kazi.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, hakuna mlolongo mrefu wa utoaji wa vibali vya ajira. Halmashauri baada ya kuwa imeidhinishwa Ikama ya watumishi, huomba kibali kutoka Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma ili iweze kuajiri, jambo ambalo kwa kawaida halichuki muda mrefu.

Hata hivyo, baadhi ya Halmashauri hususan zilizoko pembezoni, baada ya kutangaza nafasi, zimekuwa zikishindwa kupata waombaji wenye sifa. Ili kukabiliana na tatizo hilo, Ofisi yangu kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, imekubaliana na Wizara ya Fedha pamoja na Wizara za Kisekta kama Elimu, Afya, Maji na Miundombinu, kutafuta wataalam na kuwapangia moja kwa moja kwenye Halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ofisi yangu pia imeamua kujaza nafasi za Wakuu wa Idara katika Halmashauri kwa kuwateua watumishi wenye sifa kutoka Halmashauri mbali mbali kwenda kushika nafasi za Wakuu wa Idara kwenye Halmashauri zenye upungufu. Uamuzi huo umepunguza kwa kiasi tatizo la Wakuu wa Idara wanaokaimu kwa muda mrefu.

**MHE. VEDASTUSI M. MANYINYI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwanza, namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri ambaye naye amekubaliana na mimi kwamba baadhi ya Halmashauri zinakosa watumishi wenye sifa na sababu pekee ni kwa sababu ya maslahi madogo. Lakini, madhara ambayo yanapatikana, Halmashauri nyingi zinanyimwa fedha za *Capital Development Grants* kutokana na baadhi ya vigezo kwamba labda *Internal Auditor* au Mwanasheria au watumishi kama hao. Sasa, swali langu, Serikali haioni kwamba kuna haja ya

kurekebisha ukosefu wa watumishi kuwa kigezo kinachosababisha wananchi wakose fedha za *Capital Development Grants? (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili ambalo ni dogo kwamba pamoja na kwamba Mheshimiwa Naibu Waziri amesema mpango huo wa ajira hauchukui muda mrefu, lakini ni kwamba toka Manispaa itoe maombi kule Utumishi mpaka kuja kujibiwa na hatimaye wakatafuta watumishi, inachukua muda mrefu sana. Sasa, ni kwa nini Halmashauri zisiwe zinaomba watumishi kutoka TAMISEMI moja kwa moja na hawa watumishi wawe wanatolewa moja kwa moja kuliko kupitia katika Wizara mbili?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la kukosa fedha za *Capital Development Grants* kwa ajili ya kukosa watumishi muhimu. Suala hili limeishashughulikiwa na Serikali. Wizara ya Fedha kwa sasa imesomesha wafanyakazi wengi wanaoshughulikia masuala ya fedha na kwa sasa imepeleka watumishi na wahasibu katika kila Halmashauri. Kwa hiyo, tatizo la watumishi wahasibu katika Halmashauri kwa sasa limepungua. Na Wizara ya fedha imehakikisha kwamba kila Halmashauri sasa ina Mkaguzi wa ndani. Kwa hiyo, kwa sasa hakuna Halmashauri ambayo haina Mkaguzi wa ndani. Kwa hiyo, tatizo hili sasa limekwishatatuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la pili, mlolongo ambao ameusema Mheshimiwa Mbunge, ni hatua za kawaida kwamba kibali cha ajira kinatoka katika Menejimenti ya Utumishi wa Umma. Iwapo Halmshauri ikiishapata kibali hicho, Halmashauri yenyewe ndiyo inayotakiwa itangaze ili kupata hao watumishi. Serikali haiwezi kubatilisha huo uamuzi kwa sababu mpaka sasa watumishi wote wa umma wako chini ya Wizara ya Utumishi wa Umma. Hii inafanyika hivyo ili kupunguza tatizo la watumishi hewa. Kwa hiyo, mpaka sasa hivi kinachoendelea ni kwamba Menejimenti ya Utumishi wa Umma inatoa vibali haraka na Halmashauri zinatakiwa zitangaze nafasi hizo haraka. Na kama nilivyosema kwamba hatua nyingine ni zile za kuwapeleka watumishi husika moja kwa moja katika Halmashauri husika kutoka vyuoni.

**MHE. BENSON M. MPESYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kuniona kwa jicho lako la huruma. Ninaomba niulize swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa katika mwaka wa fedha uliopita, zipo Halmashauri ambazo kwa kutumia vigezo vilivyowekwa zitakosa hiyo *CDG* kwa sababu hawakuwa na wahasibu au wakaguzi walio na sifa. Je, Serikali itakuwa tayari sasa kwa Halmashauri za namna hiyo ambazo ni wazi kabisa zilikuwa na watu ambao walikuwa hawana sifa kuzipa hizo fedha za *CDG* ili tuanze upya na hao watumishi wapya?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwanza nimshukuru sana Mheshimiwa Kombani kwa majibu mazuri sana. Lakini, niongeze sasa kujibu swali la Mheshimiwa Mpesya kuhusiana na hili suala la fedha ya maendeleo ambayo tunapeleka kwenye Halmashauri zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala hili ni pana zaidi kidogo kuliko pengine linavyoelezwa na baadhi ya Waheshimiwa Wabunge. Kukosa Mweka Hazina au kukosa mtu anayeitwa *Internal Auditor*, ni sehemu tu ya mlolongo wa mambo mengi ambayo yanakuwa yameonekana dhahiri kwamba yana upungufu kwenye Halmashauri inayohusika. Kwa hiyo, mara zote utakuta viko vigezo vya aina mbili na inapotokea kwamba pengine ni jambo ambalo linaweza kurekebishwa, wanapewa muda wa kurekebisha. Lakini, unapoona hili limetokea, ujue si kukosekana kwa huyu mtu peke yake, yako madhambi mengine mengi ambayo yamesababisha hatua hiyo kuweza kuchukuliwa. Kwa hiyo, mimi nafikiri nitoe rai tu kwa Waheshimiwa Wabunge kwamba jukumu hili kwa ujumla ni letu wote hasa katika Wilaya zetu kuhakikisha kwamba vigezo vile vyote vinatimizwa kwa kadri inavyowezekana. *(Makofi)*

Na. 85

**Ukosefu wa Gari ya Kitengo cha Dawa za Kulevya Zanzibar**

**MHE. FATMA OTHMAN ALI** aliuliza:-

Kwa kuwa dawa za kulevya zinaingizwa kwa kasi sana Zanzibar; na kwa kuwa maduka ya dawa hizo yamekuwa ni mengi ikiwa ni pamoja na mashamba yenye mahoteli; na kwa kuwa Kitengo cha Dawa za Kulevya Zanzibar hakina gari la kufanyia kazi:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kukipatia magari Kitengo hicho ili kiweze kufanya kazi zake kwa ufanisi zaidi?

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Fatma Othman Ali, Mbunge wa Viti Maalum, naomba kutoa maelezo yafutayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba dawa za kulevya ni tatizo kubwa katika pande zote mbili za nchi yetu. Dawa hizi za kulevya zina athari kubwa kwa maendeleo ya Taifa letu na vijana wetu ambao ndio nyenzo na nguvukazi ya Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakubali kwamba dawa za kulevya zinauzwa lakini kwa usiri mkubwa na siyo sahihi kusema kwamba kuna maduka mengi ya dawa za kulevya ikiwa ni pamoja na mashamba yenye mahoteli.

Hivi karibuni tumeona jinsi dawa hizo zinazvyosafirishwa kwa njia ya kumeza, kuficha sehemu za siri na kwenye soli za viatu. Huu ni uthibitisho kwamba uhalifu huo unafanywa kwa njia ya siri. Hata hivyo, Jeshi la Polisi limepania kufichua mbinu hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo ya utangulizi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Fatma Othman Ali, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Kitengo cha Polisi cha Kudhibiti Dawa za Kulevya Zanzibar, hupata huduma ya usafiri wa magari kutoka Idara ya Upelelezi, Zanzibar.

Pamoja na Kitengo hicho kupata huduma hiyo kutoka Makao Makuu ya Upelelezi Zanzibar, Serikali bado inaona umuhimu wa Kitengo hicho kupatiwa magari na pikipiki ili kukiimarisha zaidi. Hivyo, Kitengo hicho kitapatiwa magari katika kipindi hiki cha Bajeti yetu ya mwaka 2006/2007. Taratibu za manunuzi kwa magari mapya ziko katika hatua za mwisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba askari wetu wamejipanga vizuri kupambana na biashara haramu ya dawa za kulevya nchini. Tunaamini tutashinda vita hii kwa ushirikiano wa kila mmoja wetu.

**MHE. FATMA OTHMAN ALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Majibu mazuri aliyoyatoa Naibu Waziri yamenipa faraja. Lakini, kwa kuwa hivi karibuni tulisikia raia wa kigeni amekamatwa katika Bandari ya Dar es salaam anapeleka dawa hizo za kulevya Zanzibar.

Je, Bandari ya Zanzibar ina udhibiti gani wa dawa hizo zisiingie Zanzibar?

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimhakikishie kwamba udhibiti ambao Dar es salaam upo, basi upo pia kwa Zanzibar. Hata hivyo, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya Ofisi ya Waziri Kiongozi pia inacho Kitengo Maalum kinachoshughulikia suala hili la kuratibu na kudhibiti dawa za kulevya.

Aidha, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii Zanzibar pia nao wanayo Idara Maalum inayoshughulikia dawa hizo za kulevya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo kwa Zanzibar kuna vyombo vingi vinavyosimamia udhibiti wa suala hili la dawa za kulevya. Nataka nimhakikishie kwamba Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na Vyombo vingine vya dola, litafanya kila jitihada kudhibiti uhalifu huo usiendelee katika Visiwa vya Zanzibar na Tanzania kwa jumla.

**MHE. BENITO W. MALANGALIALA:** Mheshinmiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa Serikali yetu imejitahidi sana katika kuhakikisha kwamba dawa za kulevya haziingizwi nchini na watu wengi wanakamatwa.

Lakini, watumiaji wa dawa za kulevya ni watu wanaojulikana, wengi tunawajua, tunazo Serikali zetu za Mitaa zinawajua, kwa nini hawafikishwi Mahakamani?

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa nchi yetu inafuata utaratibu wa sheria na wale wahalifu wote wa aina zote

wanaothibitika, wanachukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria. Na wale wote wanaotumia dawa za kulevya, inapothibitika wanafanya hivyo, basi hatua za kisheria zinachukuliwa.

Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba sasa tutazidisha kuongeza mapambano haya ili wale wote wanaohusika na kutumia dawa za kulevya waweze kuingia katika utaratibu wa kuchukuliwa hatua za kisheria. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa nchi yetu inafuata utaratibu wa sheria na wale wahalifu wote wa aina zote wanaothibitika wanachukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria. Wale wote wanaotumia madawa ya kulevya inapothibitika 00 wanafanya hivyo basi hatua za kisheria zitachukuliwa. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, kwamba sasa tutazidisha kuongeza mapambano haya ili wale wote wanaohusika na kutumia madawa ya kulevya waweze kuingia katika utaratibu wa kuchukuliwa hatua za kisheria. (*Makofi*)

Na. 86

**Askari wa Jeshi la Kujenga Taifa**

**MHE. RIZIKI S. LULIDA** aliliza:-

Kwa kuwa Tanzania ni Mwanachama wa Umoja wa Mataifa; na kwa kuwa Umoja wa Mataifa hutoa nafasi kwa Askari kwenda kusaidia Ulinzi sehemu mbali mbali, mfano *Darfur*, *Afghanistan na Congo*; na kwa kuwa nchi yetu haitoi Askari wake :-

Je, kwa nini Askari wa Jeshi letu hawapelekwi kushirikiana na wenzao wa nchi mbali mbali katika ulinzi na amani duniani kupitia Umoja wa Mataifa na Umoja wa Afrika ?

**NAIBU WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA** alijibu :-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Riziki S. Lulida, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo :-

Mheshimiwa Naibu Spika, sababu ya msingi inaliyolifanya Jeshi la Wananchi wa Tanzania, kutokushiriki kwa kiwango kikubwa katika ulinzi wa amani kwa nchi mbalimbali duniani kupitia Umoja wa Mataifa au Umoja wa Afrika ni uwezo mdogo wa kiuchumi wa nchi yetu. Nchi yoyote inapokubali jeshi lake kushiriki katika Ulinzi wa amani jeshi hilo linatakiwa kwenda na zana na vifaa vyake vyote vinavyohitajika. Mahitaji ya zana na vifaa kwa ajili ya ulinzi na amani ni makubwa na yanategemea zaidi mambo yafuatayo:-

(i) Aina ya jukumu.

(ii) Idadi ya Maafisa na Askari wanaopelekwa.

(iii) Jiografia na hali ya hewa na nchi husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, gharama za zana na vifaa Jeshi letu kwa hivi sasa uwezo wake wa kizana na kivifaa ni mdogo wa kuliwezesha kushiriki katika ulinzi wa amani kwa nchi zote zilizotolewa mfano na Mheshimiwa Mbunge.

Hata hivyo, Jeshi letu linashiriki katika ulinzi wa amani. Mnamo mwaka 1993 hadi 1995, wanajeshi 800 wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania walishiriki kwa mara ya kwanza katika ulinzi wa amani nchini Liberia. Aidha, Februari, 2007 wanajeshi 80 wamekwenda *Lebanon* kwa ajili ya ulinzi wa amani nchini humo. Ni imani yetu kwamba upatikanaji wa zana na vifaa kila utakapokuwa mzuri, ndipo kushiriki katika nchi nyingi zaidi. (*Makofi*)

**MHE. RIZIKI SAID LULIDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kuipongeza Serikali kwa kushiriki kwa wanajeshi wetu katika kulinda amani katika nchi mbalimbali. Lakini nina swali kama ifuatavyo:-

Je, pamoja na ushiriki huu je, askari wangapi wanawake wanapewa kipaumbele katika ushiriki huo ? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA**: Mheshimiwa Naibu Spika, kipaumbele kwa askari wanawake kipo na mwezi Februari mwaka huu 2007 wanawake 11 wapo Lebanon kwa ajili ya kushiriki ulinzi wa amani. (*Makofi*)

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri aliyoeleza Mheshimiwa Naibu Waziri na matatizo ya msingi aliyoeleza kwamba nchi yetu hali yetu ni ngumu ni vifaa ni vya ghali lakini bado tumeweza kushiriki katika baadhi ya ulinzi. Sasa mimi ningependa kujua tunapopeleka askari wetu kama nchi pamoja na matatizo hayo na wasiwasi wa kupoteza wanajeshi wetu vijana wetu, nchi inafaidika nini na upelekaji wa askari katika kazi kama hiyo ? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, faida kwa nchi zipo nyingi. Lakini naomba nizitaje chache tu. Kwanza, nchi yetu inapata faida ya kuwepo katika ramani ya ulinzi wa kimataifa, lakini pili, wanajeshi wetu wanapata ujuzi na uelewa, wanapata kubadilishana mawazo na wanajeshi wa nchi nyingine. Lakini la tatu, kwa kuwa baada ya kipindi cha miezi sita umoja wa mataifa wanawajibika kurejesha gharama ambazo nchi zimetumia. Kwa hiyo, tunafaidika vile vile kwa vifaa ambavyo vinatolewa na Umoja wa Mataifa. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na swali lingine, lakini kabla ya hapo naomba niwatangazie wajumbe wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii, watakuwa na Mkutano na Wageni wa Bunge kutoka Denmark halafu wameondoka kabla sijawatambulisha kwa hiyo kuna wageni hao. Kwa hiyo, Kamati ya Maendeleo ya Jamii,

wataondoka saa 4.00 kuna mkutano chumba namba 231. Kwa hiyo, nategemea mtawahi kuzungumza na wageni hao. *(Makofi)*

Na. 87

**Kujenga Reli ya Tanga, Arusha, Musoma Hadi Uganda**

**MHE. ALOYCE B. KIMARO** aliuliza:-

Kwa kuwa usafiri wa Reli ndiyo unaosafirisha abiria na mizigo kwa wingi na kwa bei nafuu na hivyo kuharakisha ukuaji wa uchumi kwa kasi na kwa kuwa Ari Mpya, Nguvu Mpya na Kasi Mpya ya kuleta maendeleo na maisha bora kwa Watanzania:-

(a) Je, Serikali haioni umuhimu wa kujenga Reli ya Tanga, Arusha, Musoma hadi Uganda?

(b) Je, kama ndivyo reli hiyo itaanza kujengwa lini?

(c) Je, nchi ngapi za Afrika Mashariki na kati ziko tayari kushiriki mpango huo?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (DR. MAUA A. DAFTARI)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Aloyce Bent Kimaro, Mbunge wa Vunjo, lenye sehemu (a), (b) na (c), kama ifuatavyo:-

(a) Tangu mwaka 1967, Serikali iliona umuhimu wa kujenga reli ya Tanga, Arusha, Musoma hadi Uganda, kwa maana ya kuunganisha kwa *wagon ferries* kwa manufaa ya Tanzania na nchi jirani. Reli hii ilibuniwa chini ya iliyokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki na kufanyiwa upembuzi yakinifu wa awali *(pre- feasibility study)* mwaka 1970.

Kutokana na umuhimu wa reli hii, Serikali inaendelea na juhudi za kumpata mzabuni atakayeandaa *railway master plan* na reli ya Tanga, Arusha – Musoma imewekwa kwenye *program* za Jumuiya ya Afrika Mashariki, aidha reli hii imewekwa kwenye mpango wa Wizara ya Miaka kumi (2006 – 20160 ya uwekezaji katika sekta ya uchukuzi *(Ten years Transport Sector Investment Program 2006 – 2016).*

Hivi sasa *NDC* na *Tata Group* ya India wameajiri kampuni kutoka *Norway* kufanya utafiti juu ya mazingira na hali ya jamii *(environmental and social impact assessment)* kwenye eneo linalozunguka Ziwa Natron, kazi iliyolenga kufanyika kati ya Oktoba 2006 hadi Septemba, 2008. Hali kadhalika *NDC* na *Tata Group* wameajiri kampuni ya *RITES* ya India kufanya *transport logistics study* eneo la kati ya Ziwa Natron na bandari ya Tanga.

Endapo mradi wa uchimbaji wa madini ya magadi Ziwa Natron utaonekana kuwa wa manufaa, uboreshaji wa njia ya reli ya Tanga – Arusha na ujenzi wa reli mpya ya Arusha – Ziwa Natron utafanyika kuanzia mwaka 2009. Kwa kufanya hivyo ujenzi wa reli ya Tanga – Arusha – Musoma utakuwa umeendelezwa kwa kiwango kikubwa. Mradi huu wa magadi, kati ya mingine, utaifanya reli ya Tanga- Arusha – Musoma kuwa na manufaa zaidi kiuchumi *(economically viable).*

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyoeleza awali Reli ya Arusha – Musoma, kuunganishwa na *wagon ferry* hadi Uganda, imewahi kufanyiwa upembuzi yakinifu wa awali kwa misaada ya nchi za Japan na China kwa nyakati tofauti. Hatua inayofuata ni kufanyiwa upembuzi yakinifu utakaohusisha pia namna ya kuepusha athari kwa mazingira katika sehemu ambazo reli hiyo, itapita zikiwemo mbuga za wanyama. Tunategemea fedha za upembuzi huo zitapatikana kutoka kwa wahisani kupitia Jumuiya ya Afrika Mashariki na programu ya Wizara ya kuendeleza miundombinu. Baada ya upembuzi yakinifu kukamilika na fedha kupatikana kutokana na vyanzo vyetu na wafadhili, ujenzi wa reli hii utaanza.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, nchi za Tanzania, Kenya na Uganda ziko taarifa kushiriki mpango huu na ndiyo maana Serikali za nchi hizo zimeiagiza Sekretarieti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki kutafuta fedha zitakazowezesha upembuzi yakinifu kufanyika. (*Makofi*)

**MHE. ALOYCE B. KIMARO:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ambayo hayana matumaini ya kujenga hiyo reli kwa siku za karibuni nina maswali mawili kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa ujenzi wa reli sasa hivi kwa kilomita gharama yake ni sawa sawa na ujenzi wa barabara wa kilomita. Lakini ujenzi wa barabara matumizi yake ni miaka 12 ndiyo ufanye matengenezo makubwa. Lakini ujenzi wa reli utatumia kwa miaka 50 ili uweze kufanya matengenezo makubwa. Lakini na reli pia inabeba mizigo mingi na kwa haraka na kwa rahisi na kwa kuwa ujenzi wa reli hiyo utaleta faida Mkoa wa Tanga kwa kuwa bandari itapanuka, Mkoa wa Kilimanjaro, mazao ya kahawa yatasafirishwa kwa wingi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, wenzio hawapendi hotuba wanataka swali.

**MHE. ALOYCE B. KIMARO :** Sasa maswali:-

(a) Kwa kuwa Serikali ya Uganda iko tayari reli hiyo ijengwe mara moja. Je, Serikali ya Tanzania, iko tayari kuwafadhili au kuwadhamini watu binafsi wapate wakope ili wajenge reli hiyo? (*Makofi*)

(b) Kwa kuwa ujenzi wa reli hiyo utaleta faida nyingi na kupunguza gharama za bei za bidhaa, Mikoa yote mitatu *including* Musoma. Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga hiyo reli kwa muda wa kipindi cha miaka kumi?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (DR. MAUA A. DAFTARI):** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nikubaliane naye kwamba ujenzi wa reli unapojenga inachukua miaka 50 ndiyo ufanye matengenezo madogo madogo na ujenzi wa barabara ni kila baada ya muda mfupi lazima ufanye aidha *parching* au *resurfacing* ya barabara hizi. Ninalotaka kumwambia Mheshimiwa Mbunge, kwamba *investment* kwenye sekta ya reli ya kubwa sana ukilinganisha na *investment* katika barabara. Ndiyo maana tulipotangaza watu binafsi katika shughuli hizi za reli kujenga hawakujitokeza na waliojitokeza ni watu wa *NDC* na *Tata Group* kwa lengo la kwamba wanaweza wakapata *Sodaesh* katika Ziwa Natron.

Napenda nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba juhudi zinafanywa kuhakikisha kwamba reli hii tukimaliza *feasibility study* ambayo ita-*determine cost* halisi ya reli hii iweze kujengwa. Napenda nimwambie Mheshimiwa Mbunge kama wako wanaojitokeza kutaka kujenga reli hii basi milango iko wazi. Lakini nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, kwamba ujenzi wa reli ya *pound* 80 kwa *yard* ni dola 2082,000 kwa kilomita na ile ya 120 *pound* ni 340,000 dola kwa kilomita.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Uganda majadiliano yamefanywa na kwa pamoja kwa kupitia *East African Community* na tukakubaliana kimsingi kwamba reli hii ina umuhimu kwa ukanda huu ambapo reli hii itapita na kwa pamoja tunahangaika kutafuta fedha za kufanya *feasibility study* na baadaye ujenzi uweze kufanywa fedha itakapopatikana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Aloyce, yeye anajua wanapatikana hao wapi. Tumechukua muda mwingi sana kwa swali hili.

Na. 88

**Minara ya Kuongoza Vyombo Baharini**

**MHE. ABUBAKAR KHAMIS BAKARY (K.n.y. MHE. KHALIFA S. KHALIFA)** aliuliza:-

Kwa kuwa, minara ya kuongozea vyombo vya baharini iliyomo sehemu za Mwambao ni muhimu sana na kwa kuwa baadhi ya minara hiyo ina matatizo:-

(a) Je, ni minara mingapi ipo katika mwambao wa bahari ya Tanzania na sehemu za maziwa?

(b) Je, katika hiyo ni minara mingapi ina matatizo ya kuwaka mara kwa mara?

(c) Je, ni teknolojia ipi inayotumika kuifanya minara hiyo iwake?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MAUA A. DAFTARI)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Khalifa S. Khalifa, Mbunge wa Gando, lenye sehemu (a) (b) na (c), kama ifuatavyo:-

(a) Katika mwambao wa bahari ya Tanzania na sehemu ya maziwa kuna minara 26 ya kuongozea meli.

(i) Kwa upande wa mwambao wa bahari iko minara 17 katika maeneo yafuatayo:-

Dar es Salaam minara 2, Tanga mnara 1, Mtwara mnara 1, Lindi mnara 1, Kilwa minara 2, Mafia minara 2, Unguja minara 6 na Pemba minara 2.

(ii) Pia kwa upande wa maziwa kuna minara 9 katika Ziwa Victoria. Upande wa Ziwa Tanganyika na Ziwa Nyasa hakuna minara.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, katika minara 26 niliyoitaja, minara 15 imeharibika au ina matatizo ya kuwaka kama ifuatavyo:-

Dar es Salaam mnara 1, Mtwara mnara 1, Kilwa mnara 1, Mafia mnara 1, Pemba minara 2 na Ziwa Victoria minara 9. Kando ya minara hiyo pia kwa upande wa Tanzania Bara:-

(i) Taa za kuonyesha mwelekeo 33.

(ii) Kuna vifaa vinavyoelea vya kusaidia kuongoza meli 6.

(iii) Kuna Vifaa vya kusaidia kuongoza meli visivyoelea *(fixed beacons)* 13. na;

(iv) Maboya yanayoelea 40.Kwa upande wa Tanzania Visiwani kuna:-

(i) Taa za kuonyesha uelekeo na vifaa vya kusaidia kuongoza meli 8

(ii) Maboya 21.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, teknolojia inayotumika kufanya minara hiyo iwake ni pamoja na matumizi ya umeme wa nguvu za jua *(solar power)* na gesi *(Aga Gas)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania pamoja na Shirika la Bandari za Zanzibar ina mipango ya kurekebisha minara hiyo kama ifuatavyo:-

Kwa upande wa Dar es Salaam kujenga mnara mpya eneo la Ras Kazi katika mwaka wa fedha 2007/2008, kuufanyia matengenezo ya *buoyant beacon* mpya na kuongeza maboya matatu. Kwa upande wa Tanga kuna mpango wa kufunga mfumo unaotumia jua. Vifaa husika vimeshaagizwa pia kumalizia ujenzi wa *beacon* iliyobaki

katika mwaka huu wa fedha. Kwa upande wa Mtwara, kuna mpango wa kukarabati mnara uliopo na kufunga mfumo unaotumia nguvu za jua. Pia kuna mpango wa kufunga mfumo unaotumia nguvu za jua upande wa Lindi na kukarabati mitambo yote.

Hii ni pamoja na Kilwa ambapo upo mpango wa kununua maboya mapya yanayotumia mfumo wa jua. Kwa upande wa Mafia ujenzi wa mnara unatarajiwa kuanza katika mwaka wa fedha 2007/2008. Ununuzi wa maboya mapya matatu yanayotumia mfumo wa nguvu za jua umeshafanyika na yameagizwa maboya mengine mawili.

Katika Ziwa Victoria ukarabati wa minara yote utaanza baada ya kumaliza *survey* ya Ziwa, kazi inayotarajiwa kuanza mwezi Mei 2007 na itachukua miaka miwili. Kazi hii inafanywa na Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Unguja na Pemba, upo mpango wa kukarabati minara yote na kufunga vifaa vya kisasa katika mwaka ujao wa fedha.

**MHE. ABUBAKAR KHAMIS BAKARY:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuuliza maswali mawili kama ifuatavyo:-

(a) Kwa sababu minara hii ni minara ambayo iko katika bahari kuu na kwa sababu meli nyingi za kigeni zinapita kwa kuongozwa na minara hii na kwa sababu minara hii ni mibovu. Je, haoni kwamba Serikali inaweza ikapata hasara kubwa iwapo meli za kigeni zitapata taathira yoyote kutokana na ubovu wa minara hii?

(b) Ni lini minara hii itajengwa haraka kwa sababu ajali hazisubiri miaka miwili ambayo Naibu Waziri ameahidi? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (DR. MAUA A. DAFTARI):** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Abubakar, kama ifuatavyo:-

Napenda nimhakikishie Mheshimiwa Abubakar kwamba Serikali inachukua juhudi zipasavyo katika kuboresha na kuweka minara hii katika hali nzuri. Lakini pia nimwambie Mheshimiwa Abubakar kama umepata nafasi ya kutembelea Magogoni, pale tunajenga mnara wa kuongozea na mnara huu utakuwa na *facilities* nyingi sana za kuweka pale ili kuona hata meli kama iko kilomita ngapi na ina matatizo gani ili kuweza kusaidia. Na tunategemea mnara huu mkubwa ulioko Magogoni Feri pale utamalizika *August* mwaka huu. Hiyo minara mingine ambayo tumesema itaendelea kuboreshwa kama nilivyoongea hapo awali. (*Makofi*)

Na. 89

**Barabara ya Lami Kati ya Kwimba – Magu**

**MHE. BUJIKU P. SAKILA** aliuliza:-

Kwa kuwa moja kati ya ahadi za Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, alipofika Ngudu, Kwimba wakati wa kampeni za Uchaguzi Mkuu ilikuwa ni kuimarisha kwa kiwango cha lami barabara kati ya Kwimba- Magu ambayo kwa sasa haina lami:-

(a) Je, sababu za barabara kutokuwa na lami hivi sasa kwa kisingizio cha upatikanaji wa fedha haiwezi kuwa sababu ya muda mrefu ya kukwepa utekelezaji wa ahadi hiyo ya Mheshimiwa Rais, huku barabara nyingine zikiendelea kujengwa na kufanyiwa ukarabati kwa kiwango cha lami?

(b) Je, Serikali inatoa ahadi gani kuwaonyesha wananchi wa Kwimba na Magu, ambao ni watumiaji wa barabara hiyo juhudi za makusudi za kutekeleza ahadi hiyo kabla ya mwaka 2010 badala ya kuendelea kuifanyia ukarabati wa kawaida usio wa kiwango cha lami?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHAGA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Bujiku Sakila, Mbunge wa Kwimba, lenye sehemu (a) na (b), kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara kati ya Kwimba na Magu inaanzia Kijiji cha Mabuki kwenye barabara ya lami itokayo Mwanza kwenda Shinyanga kiasi cha kilometa 62 toka Mwanza Mjini. Barabara hii inapitia Vijiji vya Jojiro, Ngudu (Makao Makuu ya Wilaya ya Kwimba) na Nyambiti, kwa upande wa Wilaya ya Kwimba na Vijiji vya Bukwimba hadi Magu (Kijiji cha Isandula) ambapo inaungana na barabara ya lami itokayo Mwanza kwenda Musoma. Barabara hiyo ni ya Mkoa na ina jumla ya urefu wa kilometa 77.

Ni kweli Mheshimiwa Rais, wakati wa kampeni akiwa mgombea kwa tiketi ya Chama cha Mapinduzi na hata baada ya kuchaguliwa, ameahidi kuziimarisha barabara mbalimbali nchini kwa viwango tofauti, ikiwemo hii ya Kwimba hadi Magu. Hivi sasa Wizara yangu inaendelea kuweka mipango madhubuti ya kuzitekeleza ahadi hizo katika kipindi cha miaka mitano yaani hadi 2010.

Hivyo basi, ninaomba wananchi na Waheshimiwa Wabunge, kuvuta subira, kwani sote tunafahamu kuwa miradi ya ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami inahitaji fedha nyingi na kulingana na uwezo wa Serikali yetu kwa sasa, ni wazi kwamba ahadi hizo zitatekelezwa kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha katika kipindi cha miaka mitano ijayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa Wizara yangu itaendelea kuifanyia ukarabati na matengenezo kwa kiwango cha changarawe barabara ya Kwimba hadi Magu ili iendelee kupitika wakati wote. Katika mwaka huu wa fedha 2006/2007 kiasi cha shilingi milioni 57 kimetengwa kugharamia ukarabati wa jumla ya kilometa 7 na shilingi milioni 500 pia zimetengwa kugharamia matengenezo ya barabara hiyo chini ya mradi wa

*PMMR* unaofadhiliwa na Benki ya Dunia na Serikali ya Tanzania. Mradi huu unatarajiwa kuanza muda wowote kuanzia sasa baada ya taratibu za kutolewa fedha hizo na benki Dunia kukamilika.

**MHE. BUJIKU P. SAKILA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Watanzania wengi pamoja na wananchi wa Kwimba waliokuwa wanamsikiliza Mheshimiwa Rais, wakati alipokuwa anatoa ahadi hiyo, wanafahamu kabisa kwamba anafahamu Kiswahili, alitumia neno kujenga wakati tunafahamu barabara ile anaifahamu, hakutumia neno kukarabati.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, watu wa Kwimba wangependa kufahamu ni nani Wizarani au Serikali aliyeamua kutoa tafsiri ya neno kujenga lililotumiwa na Mheshimiwa Rais, liwe na maana ya kukarabati kwa kiwango cha changarawe? *(Makofi/Kicheko)*

(c) Kwa sababu watu wa Kwimba tangu mwaka 1997/1998 wamekuwa wakiomba kipande cha Barabara kutoka Hungumala kwenda Ngudu kiunganishwe na barabara kutoka Magu kuja Ngudu. Je, Serikali iko tayari sasa baada ya ombi hilo kuwa ni la muda mrefu kwa sababu kufikia kujenga barabara hiyo cha lami kufikiria pamoja na kipande hicho cha barabara kutoka Ngudu kwenda Hungumala? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHAGA):** Mheshimiwa Naibu Spika, nimesema katika jibu langu la msingi kwamba kwa kweli Serikali inaendelea kutekeleza ahadi alizozitoa Mheshimiwa Rais. Lakini kwa kweli ahadi hizi zitatekelezwa kutengemea na upatikanaji wa fedha. Kwa sababu ahadi zilitolewa kwa miaka mitano tunaendelea kuweka *program* wa utekelezaji wa ahadi hizi ili tuweze kuzitekeleza.

Lakini nimesema kabla fedha hazijapatikana kwa ajili ya kujenga barabara hiyo kwa kiwango alichoahidi Rais cha lami, basi tutaendelea kukarabati kwa kiwango cha changarawe. Nataka niseme kwamba hata Mheshimiwa Rais, alilitambua hilo la fedha na ndiyo maana napenda ninukuu alichosema kama ilivyorekodiwa katika ahadi zake, alisema kama ifuatavyo na nanukuu:-

"Tutaimarisha barabara ya lami kati ya Kwimba na Magu kama hali ya fedha itaruhusu" ni maneno halisi aliyotumia. Kwa hiyo, wananchi na Wabunge tuendelee kuvumilia tumeanza kutekeleza na mifano ipo na bado tutaendelea kutekeleza katika miaka mitatu na nusu iliyobaki ili kutimiza ahadi alizosema Mheshimiwa Rais.

Kuhusu kuunganisha barabara hiyo niliyoitaja kutoka Ngudu ili na yenyewe ihudumiwe na wakala wa barabara *TANROADS* kwa sababu leo hii tunaanza kuzungumzia Muswada wa barabara na kwa sababu katika kipengele kama mtakachoona namba 12 kinaelezea vizuri vigezo vya kuunganisha vya barabara kuwa ya Mkoa au *trunk road* au ya Wilaya, viko wazi, basi nina hakika tutaliangalia hili ombi kulingana na vigezo vitakavyokuwa vimewekwa na sheria mpya ya barabara.

**NAIBU SPIKA:** Siruhusu maswali mengine muombe kuchangia kwenye Muswada utakaokuja baada ya maswali. Mambo yote ya barabara yatapatikana humo.

Na. 90

**Ujenzi wa Barabara Nchini**

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA** aliuliza:-

Kwa kuwa, wakala wa barabara *TANROADS* iliundwa kisheria ili kuongeza ufanisi katika ujenzi wa barabara nchini na hivyo kuongeza kasi ya ukuaji uchumi na kuwa, wahandisi wengi waliokuwa Wizara ya Ujenzi wakati huo walihamishiwa *TANROADS* na kwa kuwa kwa hali ilivyo sasa kuna barabara zinazoshughulikiwa na Wizara na zingine na *TANROADS*:-

(a) Je, ni barabara zipi zinashughulikiwa na Wizara na hushughulikiwa na *TANROADS*?

(b) Je, ni sababu zipi zinasababisha kuwe na makundi hayo mawili?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA)** aliuliza:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Victor Kilasile Mwambalaswa, Mbunge wa Lupa, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba Wakala wa Barabara (*TANROADS*) iliundwa kisheria ili kuongeza ufanisi katika ujenzi na matengenezo ya barabara nchini na hivyo kuongeza kasi ya ukuaji wa uchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya *TANROADS* kuanzishwa, ujenzi na matengenezo ya barabara zote nchini ulikuwa ukisimamiwa na Wizara ya Ujenzi. Mwaka 2001 baada ya kuanzishiwa *TANROADS*, kazi zote za matengenezo zilihamishiwa *TANROADS*.

Aidha, miradi ya maendeleo ilihamishiwa *TANROADS* kwa awamu kutokana na sababu mbalimbali zikiwemo za kuupa wakala muda wa kujijenga kiuwezo na kukamilisha mfumo wake wa kiutawala.

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi mingi ya ujenzi wa barabara inayotekelezwa nchini inafadhiliwa na wadhili mbalimbali wakiwemo baadhi ambao walitoa masharti wakati *TANROADS* inaanzishwa kwamba hadi hapo *TANROADS* itakapokuwa imejijenga kikamilifu, utekelezaji wa miradi wanayoifadhili uendelee kubaki Wizarani.

Kwa mfano, *Kuwait Fund* ambao wamefadhili ujenzi wa Daraja la Mkapa, barabara ya Mkuranga - Kibiti na hivi sasa wanafadhili ujenzi wa barabara ya Ndundu – Somanga, walitoa masharti hayo hapo awali lakini sasa wameridhika na utendaji wa *TANROADS*.

Hii ilitokea kwa wafadhili wengine pia kama Serikali ya Japan kwa mradi wa Makuyuni - Ngorongoro. Aidha, miradi ambayo ilikuwa inaendelea wakati *TANROADS* inaanzishwa na ambayo ilikuwa na matatizo kwa mfano miradi ya ujenzi wa barabara ya *Wazo Hill*- Bagamoyo na barabara za Mjini Mwanza haikuhamishwa kwenda *TANROADS*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara pia imekuwa ikisimamia ujenzi wa miradi maalum ambao ujenzi wake unatekelezwa kwa kutumia fedha za ndani mradi Maalum wa Barabara kuu unajumuisha Nangungukulu – Mbwemkuru, Mbwekuru – Mingoyo, Dodoma- Manyoni na Manyoni – Singida. Miradi hii imekuwa chini ya utekelezaji wa Wizara kwa vile wakati inaanza mwaka 2001 ndiyo *TANROADS* pia ilikuwa inaanzishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiacha miradi niliyoitaja hapo juu miradi mingine yote ya upembuzi yakinifu, usanifu wa kina na ujenzi inayoendelea hivi sasa nchini inasimamiwa na *TANROADS* kwa vile hivi sasa wana uwezo wa kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi karibuni Wizara ilitangaza zabuni ya ujenzi wa barabara ya Ndundu – Somanga ambayo inafadhiliwa na *Kuwait Fund* na ni mradi pekee mpya chini ya usimamizi wa Wizara kutokana na matatizo makubwa ya mkopo kwa upande wa mfadhili yaliyopelekea sehemu ya barabara ya Mkuranga - Kibiti kukarabatiwa kwa fedha za ndani badala ya mkopo kutoka Kuwait. Baada ya zoezi la kumpata Mkandarasi kukamilika Wizara inatarajia kuhamishia mradi huu *TANROADS* kwa utekelezaji wa awamu ya ujenzi kwa vile matatizo na mfadhili *Kuwait Fund* yatakakuwa yamekwisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maana hiyo, mwelekeo wa sasa wa Wizara ya Miundombinu, hasa baada ya *TANROADS* kuimarika kiutendaji na kiutawala ni kuachia wakala huo shughuli zote za utekelezajiwa miradi ya matengenezo na ujenzi wa barabara zote zilizo chini yake, ili Wizara ibaki kama mtoa sera kuhusu masuala yote ya ujenzi na matengenezo ya barabara nchini na Msimamizi na mwangalizi wa shughuli za wakala wa *TANROADS (oversight).*

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA:** Nashukuru Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kunipa kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri ambayo yameniridhisha sana, sana, sana hasa hasa pale aliposema kwamba kuanzia sasa barabara zote zitakuwa zinasimamiwa na Wakala wa Barabara *TANROADS.* Nina maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa miradi yote iliyosimamiwa na Wizara toka mwaka 2001 ya Dodoma-Manyoni, Manyoni-Singida, Dar es Salaam-Mingoyo, Mingoyo-Mbwemkuru, miradi hiyo imeingia kwenye migogoro mikubwa sana ambayo imeipelekea Serikali na wakandarasi kupelekana kwa *arbitrator*

na ambako kuna ada kubwa sana anayolipwa *arbitrator* mwenyewe na Mawakili wanaoiwakilisha Serikali kwa *arbitrator* huyo. Je, pamoja na mashinikizo ya hao wafadhili nani aliyelipa ada za *arbitration?* Pili, Mheshimiwa Naibu Spika, Naibu Waziri wa Miundombinu mwaka jana alikuja Chunya ambako aliwaahidi wananchi wa Chunya kwamba barabara kutoka Mbeya-Chunya-Makongorosi ingeanza kujengwa mwaka jana na barabara hiyo tenda zake zimefunguliwa tarehe 2 mwezi wa tatu. Je, ujenzi wa barabara hii utaanza lini ili wananchi wa Chunya wapate nafuu kwa kumsikia Naibu Waziri? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA):** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuna baadhi ya miradi ambayo ilikuwa na migogoro lakini si kweli kwamba miradi yote iliyosimamiwa moja kwa moja na Wizara imekuwa na migogoro. Kwa mfano, Daraja la Mkapa, barabara ya Makuyuni kwenda Ngorongoro, barabara za mjini Mwanza, hizi zote hazikusimamiwa na *TANROADS* lakini zilitekelezwa vizuri. Kwa hiyo, migogoro hii kwa kiasi kikubwa haina uhusiano wa moja kwa moja na kusimamiwa ama na Wizara ama na *TANROADS.* Lakini ni kweli kulikuwapo na migogoro. Sasa kuhusu kwamba nani alilipa *abitration fees.* Ukweli ni kwamba katika mkataba mambo yote hayo huwekwa wazi kama inabidi muingie kwenye *abitration* kati ya Wizara na Mkandarasi basi vipengele vipo vinavyoeleza nani atalipia nini na kubwa ni yule ambaye anaamua kwenda. Kwa hiyo, hili ni suala la kimkataba na wala sidhani kwamba lina matatizo yoyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali la barabara ya Mbeya-Chunya-Makongorosi. Ni kweli kwamba tenda ya barabara hiyo ilishatangazwa na kama alivyosema mwenyewe mimi nilikuwa Mangorosi na tulihutubia wananchi tukiwa pamoja naye na kuahidi na kama nilivyoahidi kweli tenda imetangazwa na nimhakikishie tu kwamba kazi ya ujenzi itaanza mara tu baada ya kukamilika kwa *evaluation* ya hizo tenda. Kazi ya ujenzi itaanza mara tu baada ya kukamilika kwa *evaluation* ya hizo tenda na mikataba kusainiwa na yule atakayekuwa ameshinda. *(Makofi)*

Na. 91

**Ujenzi wa Maabara Mashuleni**

**MHE. PASCHAL C. DEGERA** aliuliza:-

Kwa kuwa, katika Bajeti ya mwaka 2006/2007, Serikali ilitenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa maabara na kwa kuwa, shule zote za sekondari katika jimbo la Kondoa Kusini, hazina maabara:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga maabara hata moja katika jimbo hilo?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. LUDOVIC J. MWANANZILA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Paschal Constantine Degera, Mbunge wa Kondoa Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika B ajeti ya mwaka 2006/2007 Serikali ilitenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa maabara 42. Maabara 2 zilipangwa kujengwa katika kila Mkoa. Makubaliano yalikuwa kila Mkoa kuchagua shule moja ambayo itapatiwa fedha za ujenzi wa maabara hizo 2. Mikoa yote iliwasilisha mapendekezo ya shule hizo na tayari fedha zote zilishatengwa kwa ajili hiyo zimekwishatumwa. Katika Mkoa wa Dodoma Sekondari ya Kiwanja cha Ndege iliyopo Manispaa ya Dodoma ilipewa jumla ya shilingi milioni 28 kwa ajili ya ujenzi wa maabara hizo.

Serikali inaendelea na juhudi ya kutafuta fedha zaidi kwa ajili ya ujenzi wa maabara. Fedha itakapopatikana, tutaomba tena Mikoa ituletee shule ambazo zitakuwa zimechaguliwa kujengewa maabara kwa wakati huo. Ni matarajio yetu kuwa Mkoa wa Dodoma pia utaleta mapendekezo yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa shule za sekondari ni nyingi, mahitaji ya maabara ni makubwa kuliko uwezo wa Serikali. Tunawaomba wadau wote wa elimu waendelee kusaidiana na Serikali kutafuta vyanzo vingine vya fedha kwa ajili ya ujenzi wa maabara hizi.

**MHE. PASCHAL C. DEGERA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Aidha, namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake. Naomba niulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa katika jibu lake ametoa wito kwamba wadau wa elimu wajitokeze kusaidiana kujenga maabara hizi ili kukidhi mahitaji ya maabara katika shule zetu za sekondari na kwa kuwa wananchi wa Tarafa ya Goima kwa kutambua hilo wamekwishajitolea na wajenga vyumba viwili kwa ajili ya lengo hilo.

Lakini wameshindwa kukamilisha kwa sababu uwezo wao ni mdogo lakini majengo yamekwishakamilika. Je, Wizara itatusaidiaje ili kuweza kukamilisha lile jengo kwa maana ya kupatiwa vifaa yaani *fitings* ili vyumba hivyo viweze kutoa huduma ya maabara kwa shule hiyo ya Soya?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. LUDOVIC J. MWANANZILA)**: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza labda nichukue nafasi hii kuwapongeza wananchi wa Kondoa kwa jinsi wanavyojitolea katika ujenzi wa Shule za Sekondari. *(Makofi)*

Pia niwapongeze wananchi wote wa Tanzania, nchi nzima kwa jinsi walivyojitolea katika ujenzi wa madarasa na ujenzi wa maabara. Hizi ni juhudi ambazo wananchi wanazionyesha na Serikali inazitambua sana lakini kama nilivyoeleza katika swali la msingi, fedha tunazopewa kwa ajili ya ujenzi wa maabara ni chache.

Lakini pale ambapo wananchi wameshajitolea, wameshajenga vyumba vya maabara kama wananchi wa Goima, Serikali itaangalia ni jinsi gani kwanza zikaguliwe hizo maabara zilizojengwa kama zimejengwa kwa kiwango kile kinachotakiwa ili badala ya kujenga maabara nyingine basi fedha iwekezwe katika majengo hayo ambayo ni imara ili yaweze kukamilishwa na tuweze kupunguza gharama ya ujenzi wa maabara zetu. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nina maswali saba (7) na ni lazima yaishe. Kwa hiyo, muda ulioko hautoshi.

Na. 92

**Mpango wa MMEM na Kiwango cha Elimu kwa Watoto wa Kike**

**MHE. ZAYNAB M. VULU** aliuliza:-

Kwa kuwa mpango wa MMEM ulianzishwa nchini kwa lengo la kuinua kiwango cha elimu na kuboresha elimu kwa ujumla, lakini matatizo ya elimu yamekuwa yakimwathiri zaidi mtoto wa kike:-

(a) Je, mpango huo wa MMEM umemsaidiaje mtoto wa kike katika kuboresha na kuinua kiwango chake cha elimu?

(b) Je, ongezeko la kufaulu kwa mtoto wa kike limefikia kiwango gani?

(c) Kama kuna ongezeko la kufaulu kwa watoto hao. Je, Serikali ina mipango gani ya kuongeza shule za sekondari za wasichana?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Zaynab Vulu, naomba kwa idhini yako nitoe salam za pole na rambi rambi kwa ndugu jamaa ambao wamepoteza wapendwa wao katika ajali ya *Bus* la *Buffalo* ambapo wanafunzi kadhaa walikuwemo wakirejea shuleni baada ya mapumziko mafupi. Mwenyezi Mungu aziweke roho za marehemu mahala pema na kuwapatia nafuu ya haraka majeruhi wote, amin. Baada hapo naomba kujibu swali la Mheshimiwa Zaynab Matitu Vulu, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Mpango wa Maendeleo ya elimu ya Msingi (MMEM) ulianzishwa mwaka 2002, ulikuwa na malengo ya kuongeza nafasi ya elimu ya msingi, kuongeza ubora wa elimu na usawa wa uandikishwaji

katika ngazi hiyo. Mpango huu umemsaidia mtoto wa kike katika kuinua kiwango chake cha elimu kama ifuatavyo:-

Kuongeza uandikishwaji wao kulikotokanana kuondolewa kwa ada na michango mingine shuleni. Mfano, mwaka 2001 kabla ya MMEM, idadi ya Wanafunzi katika shule za msingi walikuwa 4,845,185 kati ya hao wasichana walikuwa 2,385,995. Uandikishwaji wa watoto wote ulikuwa asilimia 84.4. Mwaka 2002 baada ya MMEM kuanza idadi iliongezeka hadi kufikia 5,981,338 kati yao wasichana walikuwa 2,929,320 ambapo uandikishwaji ulifikia asilimia 98.6. Mwaka 2006 kulikuwa na jumla ya wanafunzi 7,959,884 kati ya hao wasichana ni 3,908,208 ambapo uandikishwaji umefikia asilimia 112.7.

Kuboresha mitaala ya mbinu za ufundishaji kwa kuhusisha mbinu shirikishi zikiwemo zinazomjali mtoto wa kike yaani *girls friendly teaching methods.* Kiwango cha kufaulu kwa mtoto wa kike kimekuwa kikiongezeka kila mwaka tangu MMEM ulipoanza.

MEMKWA unatoa mpango wa elimu ya msingi kwa waliokosa unatoa fursa ya Elimu kwa watoto walioacha shule kwa sababu mbalimbali kuendelea na masomo wakiwemo wasichana. Kupitia mpango huu kuna jumla ya wanafunzi 221,479 wakiwemo wasichana 91,634.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, ufaulu wa mtoto wa kike mwaka 2001 kabla ya MMEM, ulikuwa asilimia 21.39. Kwa mujibu wa matokeo ya mtihani wa Darasa la Saba ya Desemba 2006, kiwango cha ufaulu kwa mtoto wa kike umefikia 64.6.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kwa kushirikiana na wananchi, wanaendelea kujenga shule nyingi za sekondari ili kuchukua wanafunzi wengi na hatimaye wote wanaofaulu mtihani wa darasa la saba wakiwemo wanafunzi wa wasichana, ahsante. *(Makofi)*

**MHE. ZAYNAB M. VULU:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Spika. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina swali moja la nyongeza. Pamoja na jitihada za Serikali za kumkwamua mtoto wa kike kielimu, lakini bado mtoto wa kike huyo huyo anapatwa na matatizo mengi ya kijamii.

Je, Serikali haioni sasa wakati umefika wa kujenga angalau shule moja ya wasichana ya bweni ili kuwanusuru wasichana hao na matatizo ya kijamii ikiwemo mimba za utotoni? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA):** Mheshimiwa Naibu Spika, awali nampongeza kwa kuwa na *concern* kubwa sana kwa elimu ya wasichana. Naomba nikiri kwamba mpango huo anaoutaka tutaufanyia kazi, tunakubali ushauri wake na pale Bajeti itakaporuhusu, tutalifanyia kazi suala hilo.

Hata hivyo, Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu kwa kushirikiana na *NGO* mbalimbali imetoa upendeleo mkubwa sana kuwanusuru wasichana hawa kwa kupitia mpango ambao ulikuwepo na unaendelea hivi sasa uliokuwa unaitwa *Girls Secondary Education Support* ambao umeshasomesha wanafunzi 4,075 na pia kuna mpango mwingine wa *Campain for Female Education* ambao wenyewe umeshasomesha wanafunzi 104 na pia Mheshimiwa Mke wa Rais, Mama Salma Kikwete naye amewekeza kuwasomesha watoto wa kike ili kuwanusuru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tukubali kwamba wasichana wanahitaji kusaidiwa zaidi na sisi tunalifahamu tutalifanyia kazi. Ahsante. *(Makofi)*

Na. 93

**Soko la Kimataifa Namtumbo**

**MHE. VITA R. KAWAWA** aliuliza:-

Kwa kuwa Wilaya ya Namtumbo ni Wilaya inayozalisha mazao ya chakula kwa wingi yakiwemo mahindi, mpunga, maharage, ufuta, alizeti, soya na kadhalika na kwa kuwa mazao hayo hayana soko la uhakika, na Halmashauri imeanza kujiandaa kufuata taratibu za mpango wa masoko ya mazao ya kilimo:-

Je, Serikali inaweza kuwahakikishia wananchi wa Namtumbo kuwa wakikamilisha taratibu hizo wanaweza wakajengewa soko la kimataifa la mazao yao kupitia programu ya *AMSDP* au njia nyingine?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa, Mbunge wa Namtumbo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kuchukua fursa hii kuwapongeza wakulima wa Wilaya ya Namtumbo kwa juhudi zao za uzalishaji wa mazao mbalimbali. Kutokana na juhudi hizo, Wilaya iliteuliwa kuwa moja ya Wilaya zinazotekeleza Mpango ya Kuendeleza Mifumo ya Masoko ya Mazao ya kilimo yaani *Agricultural Marketing Systems Develpment Program (AMSDP)* ambayo pamoja na mambo mengine, inajihusisha na uimarishaji wa miundombinu ya masoko ya mazao kwa kujenga au kukarabati masoko, barabara za vijijini, madaraja na maghala. Ujenzi wa barabara kutoka kijiji cha Mlilayoyo hadi Hanga yenye umbali wa km 26 ni moja ya juhudi za Programu ya kuendeleza miundombinu ya Masoko katika Wilaya ya Namtumbo na Songea Vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo imeanza mchakato wa kuendeleza miundombinu ya masoko kupitia mpango wa Programu ya Kuendeleza Mifumo ya Masoko ya Mazao nchini, Serikali itaendelea kushirikiana na kuunga mkono juhudi za Halmashauri hiyo katika kufanikisha azma yao.

Kinachotakiwa ni Halmashauri kuwasilisha kwenye Programu hiyo aina ya miundombinu wanayotaka iendelezwe na uteuzi utafanyika kulingana na vigezo vilivyowekwa. Miundombinu inayohusika ni pamoja na masoko ya mazao, barabara za vijijini na maghala ya kuhifadhia mazao.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa wito kwa Mheshimiwa Mbunge kushirikiana kwa karibu sana na Halmashauri yake ya Wilaya ya Namtumbo ya kuandaa mikakati ya kuwezesha kutumia fursa mbalimbali za kuendeleza miundombinu ya masoko ya mazao yao. Kwa kufanya hivyo, Serikali haitasita kushirikiana nao katika utekelezaji wa kujengewa soko la mazao Wilayani Namtumbo.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Spika kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwanza kabisa naomba nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko, kwa majibu yake mazuri. Kwa kuwa mwaka jana tuliomba Serikali kupitia Kitengo cha Hifadhi ya Chakula *SGR* kununua baadhi ya mazao yetu hususan mahindi Wilayani Namtumbo na walifanya hivyo. Kwa kuwa hatuna soko ya manunuzi ya mazao ya nafaka, walinunua zaidi ya tani 2,200 mahala pa wazi kwa kutandika maturubai na kwa kuwa Halmashauri ya Namtumbo imeshajiandaa kimkakati. Je, Serikali inaweza kutuhakikishia kutuweka katika Bajeti ya mradi huo mwaka huu ili tuweze kushirikiana tujenge soko la mazao mchanganyiko?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kwa mara nyingine niwapongeze sana wananchi wa Wilaya ya Namtumbo kwa juhudi zao mbalimbali za kujiandalia mipango ya kuhudumia wakulima wao ikiwa ni pamoja na hili suala la mipango ya ununuzi wa mazao waliyolima mwaka jana. Kuhusu suala la soko mahsusi kwa ajili ya mazao mchanganyiko kwa Bajeti inayokuja napenda nimshauri Mheshimiwa Mbunge kwamba kama tulivyojibu katika swali la msingi kwamba mpango huu unaoandaliwa wa kujenga soko la kimataifa kwa ajili ya mazao mbalimbali kule Namtumbo ukitekelezwa huo bila shaka hata azma hii ya kutaka kuwe na soko mahsusi kwa ajili ya mazao mchanganyiko itakuwa imekwishakukidhi haja hiyo. Lakini niongeze tu kwamba vile vile uko mpango mwingine, wa stakabadhi ya mazao ghalani ambao ulikwishapitishwa hapa Bungeni kwa kupitia sheria ya mwaka juzi nao huo ukianza kutekeleza nina hakika suala zima la kuuzia mazao nje litakuwa limetafutiwa ufumbuzi.

Na. 94

**Soko la Uhakika la Kuuza Bidhaa**

**MHE. MGENI J. KADIKA** aliuliza:-

Kwa kuwa wanawake wengi wamejiunga katika vikundi vidogo vidogo vya uzalishaji nchini lakini Wanakosa Soko la uhakika la kuuza bidhaa zao kama vile mafuta ya mdarasini kusindika matunda *juice* asali na bidhaa nyinginezo:-

(a) Je, ni lini Serikali itawapatia soko la nje wananchi hawa?

(b) Je, ni lini Serikali itawasaidia wazalishaji hawa wadogo wadogo ili waweze kuendelea na kazi zao za uzalishaji?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba nianze kwa kutoa pole na salamu za rambi rambi kwa wananchi wa Mkoa wa Kilimanjaro na mikoa mingine iliyoathirika na ajali ya *bus* na ambayo iliua zaidi ya watu 30 huko Mwanga, Kilimanjaro.

Pili, kwa niaba ya wanawake wa Mkoa wa Kilimanjaro na wananchi kwa ujumla, nitoe pole kwa familia ya marehemu Dr. Chiduo pamoja na wananchi wa Gairo na wa Mkoa wa Morogoro.

Pia niwapongeze Waheshimiwa Mtutura na Kyendesya kwa kujiunga na Bunge hili. Baada ya hayo, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika, Mbunge wa Viti Maluum, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli wanawake wengi wamejiunga katika vikundi vidogo vidogo vya uzalishaji nchini na wanakabiliwa na tatizo la soko la uhakika la kuuza bidhaa zao kutokana na sababu mbalimbali, mojawapo ikiwa ni ushindani kibiashara hasa katika soko la nje.

Serikali inalo jukumu la kuwezesha wanawake kupata soko la nje kwa kuwajengea uwezo wa kushindana kibiashara. Jitihada zimefanywa za kuwawezesha wanawake wafanyabiashara kushiriki katika maonyesho ya kibiashara ya ndani na nje ya nchi, kwa lengo la kutangaza bidhaa zao na kutafuta masoko.

Kwa mfano Serikali imeshirikiana na mashirika yasiyo ya kiserikali kuwezesha ushiriki wa wanawake katika Maonyesho ya Kimataifa ya Dar es Salaam yanayofanyika kila mwaka. Baadhi ya wanawake wamewezeshwa kushiriki katika Maonyesho ya Kibiashara ya nchi za *SADC.*

Mafunzo kwa vitendo yamekuwa yakitolewa kwa vikundi vya wanawake wafanyabiashara kabla ya kushirii katika maonyesho ya biashara ya kikanda, kimataifa na ndani ya nchi kupitia maonyesho hayo wanawake wameweza kupata masoko ya bidhaa zao, kujifunza mbinu mbalimbali mpya, kubadilishana uzoefu kutoka kwa wafanyabuiashara wengine na hivyo kuweza kuongeza ubora wa bidha wanazozalisha.

(c)Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuwasaidia wanawake wazalishaji wadogo wadogo kuzalisha kwa ubora na kwa viwango vya masoko ya ndani na nje, Serikali kwa kushirikiana na wadau pia imewezesha mafunzo ya ujasiriamali.

Mafunzo hayo ni pamoja na yale yanayotolewa na Shirika la Kuendeleza Viwanda vidogo vidogo *(SIDO)* kwa wanawake wasindikaji bidhaa za vyakula na yale ya Wakala

wa Maendeleo ya Kiufundi *(ADAT),* kwa wanawake wazalishaji bidhaa za nguo vile vile Vyuo vya Elimu ya Ufundi *(VETA)* hutoa stadi mbalimbali zikiwemo za ujasiriamali na uzalishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea kuwasaidia wanawake wazalishaji wadogo wadogo kwa kuwapatia mikopo yenye masharti nafuu kupia Mfuko wa Maendeleo wa Wanawake *(WDF).*

Pia katika kuhakikisha kuwa wanawake wengi zaidi wanapata mikopo, Serikali kupitia Maafisa Maendeleo ya Jamii na Maafisa Ushirika inaendelea kuwahamasisha wanawake kujiunga na vyama vya Ushirika vya kuweka na kukopa *(SACCOS)* na vikundi vya uchumi.

Iwapo wanawake watajiunga na *SACCOS* watapata pia fursa ya kupata mikopo kutokana na fedha ambazo Mheshimiwa Rais amezitenga kwa mikoa yote kwa wafanya biashara wadogo wadogo na wa kati ili kukuza mitaji yao. Kwa njia hii pia wanawake wataweza kuendeleza na kuimarisha shughuli za uzalishaji mali.

Aidha, pamoja na jitihada hizo Serikali imeendelea kuweka mazingira mazuri kwa asasi mbalimbali za kiserikali na zisizo za kiserikali ili ziweze kutoa mikopo yenye masharti nafuu. Mazingira hayo ni pamoja na kuwepo kwa Sera ya Mitaji Midogo *(Micro-finance Policy)* na Programu ya Huduma za Mitaji Midogo Midogo Vijijiji *(Rural Finance Services Programme),* inayoratibiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu. Ahsante.

**MHE. MGENI J. KADIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, napenda kuuliza swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kuna mpango wa kufungua benki ya wanawake Tanzania Bara. Je, kuna mpango gani wa kufungua Matawi Zanzibar kwa maana ya Unguja na Pemba ili wanawake walioko huko wapate kufaidika kwa kuweza kuzalisha zaidi miradi yao?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kwa kusema kwamba mchakato wa benki ya wanawake ulianza mwaka 99 wakati walipokuwa katika maonyesho ya *Dar es Salaam International Trade Fair* na wakaamua kwenda kumwona Mheshimiwa Rais wa Awamu iliyopita, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, baada ya hapo kazi hii ilikabidhiwa Wizara ya Fedha pamoja na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, kuangalia ni jinsi gani mchakato wa benki nzima uanze.

Kwa namna hiyo ilipofika mwaka 2005 tulitengeneza *road map* yaani mwelekeo wa namna ya kufikia azma hiyo. Kamati ya kutengeneza *road map* hiyo ilishirikisha kwanza Wizara yetu, Benki Kuu ya Tanzania, Wizara ya Ushirika na Masoko wakati huo, TAMISEMI na Wizara ya Fedha. Baada ya hapo Wizara iliteua.........

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, anachouliza ni kwamba na Zanzibar wamo? Historia ndefu muda hautoshi.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, benki hii kwanza itakuwa na mtazamo wa kibiashara na itaenea mikoa yote. Na hii tutakwenda awamu kwa awamu kama ambavyo benki nyingine za biashara ambavyo zinaanzishwa.

Ni matumaini yetu basi kwa kuwa Tanzania Visiwani ni sehemu ya Tanzania na huko nako kutakuwa na utaratibu wa kuanzisha matawi ya Benki hiyo. Ahsante Mheshimiwa Naibu Spika. *(Makofi)*

Na. 95

**Uhaba wa Daktari wa Meno – Morogoro Vijijini**

**MHE. HAMZA A. MWENEGOHA** alijibu:-

Kwa kuwa Morogoro Vijijini hakuna Daktari wa Meno hali inayosababisha wananchi kuhudumiwa na wanganga pamoja na manesi wa zahanati ambao hawana ujuzi wa matibabu ya meno:-

(a) Je, ni lini Serikali itapeleka madari wa meno katika vituo vya afya vya Tawa, Duthumi na Kisaki-gomero?

(b) Kwa kuwa Morogoro Vijijini hakuna hospitali ya Wilaya. Je, Halmashauri inaweza kuruhusiwa kuazima mara kwa mara Daktari wa meno kutoka hospitali ya Mkoa kutembelea vijiji vya Jimbo la Morogoro Kusini?

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Hamza Mwenegoha, Mbunge wa Morogoro Vijijini, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Kwa mujibu wa Ikama *(Staffing Level)* ya vituo mbalimbali vya kutolea huduma za afya, Madaktari wa Meno kwa maana ya *(Doctor of Dental Surgery)* wanatakiwa kuwepo kwenye hospitali za Wilaya, Mikoa na Rufaa tu. Hata hivyo kutokana na uchache wa wataalamu hawa katika soko la ajira Serikali bado haijafaniikiwa kuwa na madaktari wa Meno wa kutosha katika hospitali zote kama inavyotakiwa. Hivyo basi, kwa sasa haitawezekana kuwapeleka madaktari wa Meno yaani *(Dental Surgeon)* kwenye vituo vya afya vikiwemo vile vya Tawa, Duthumi na Kisaki-gomero vilivyoko Morogoro Vijijini. Hata hivyo kada ya matabibu wasaidizi wa meno *(Dental Assistants)* ni stahili kupelekwa katika vituo vya afya pale wanapopatikana. Napenda kumshauri Mheshimiwa Mbunge kwa kushirikiana na Halmashauri yake kutenga nafasi za ajira kwa ajili ya matabibu wa Meno *(Dental Assistant)* na Wizara

yangu itasaidia upatikanaji wa watumishi hao mara baada ya kuidhinishwa kwa nafasi hizo. Nimshauri Mheshimiwa Mbunge na Halmashauri ya Wilaya.

Lakini ningependa nizishauri Halmashauri zote kwamba tunaposema kutenga nafasi maana yake kukasimia na kuweka katika makadirio ya bajeti. Nimeona niliseme hilo kwa sababu utaratibu wetu kwa sasa hivi ni kwamba watalaam wetu wanapohitimu kwenye vyuo tunawapeleka moja kwa moja kwenye Halmashauri. Lakini imejitokeza wengine wakienda wanarudi kwa sababu hakuna mishahara ambayo iliwekwa kwenye bajeti, kwa hiyo, tusaidiane kwa hilo.

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, upo utaratibu maalumu wa *Out reach Service* ambapo wataalamu mbalimbali wa afya wakiwemo madaktari wa meno kutoka Hospitali za Wilaya na Mikoa wanajiwekea utaratibu wa kupeleka timu za wataalamu mbalimbali katika zahanati au vituo vya afya kwa mzunguko. Wakifika kwenye vituo wanakuta tayari wenyeji wamewaandaa wagonjwa ambao ushauri wao unahitajika. Huu ni mpango mzuri na natoa rai kwa mikoa yote, ukiwamo mkoa wa Morogoro, kukasmia huduma hii (posho, usafiri, n.k.) katika mipango kabambe ya afya ya Mkoa au Wilaya *(Comprehensive Regional or Council Plans).* Hii itawezesha kutumia wataalamu wachache tulionao kuwahudumia wananchi wengi zaidi. Mpango huu upo katika miongozo ya Wizara, kinachohitajika ni kusimamia na kuikasimia.

Na. 96

**Kilimo cha Umwagiliaji – Songwe**

**MHE. DR. GUIDO G. SIGONDA** aliuliza:-

Kwa kuwa katika bonde la Ziwa Rukwa upande wa Jimbo la Songwe Wilayanji Chunya kuna maji ya kutosha kwa kilimo cha kiangazi; na kwa kuwa Ilani ya Uchaguzi ya CCM inasisitiza kilimo cha aina hiyo kwa maeneo yenye mabonde yenye maji kama Jimbo la Songwe; na kwa kuwa wananchi wa maeneo hayo hawana uwezo wa kuanzisha kilimo cha umwagilaji cha aina yoyoe ile:-

(a) Je, Serikali haioni ni wakati muafaka sasa kuanzisha Mradi wa kilimo cha Umwagiliaji katika bonde hilo hasa wakati wa kiangazi?

(b) Kwa kuwa wakati wa kiangazi wananchi wa maeneo hayo hupata shida sana ya maji yaliyo bora jirani na maeneo wanayoishi: Je, Serikali inaweza kuwapunguzia wananchi hao kero ya maji kwa kuwawekea miradi ya maji kwa kuchimba hata visima vifupi?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO CHAKULA NA USHIRIKA (MHE. DK. DAVID M. DAVID)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Guido Gorogolio Sigonda, Mbunge wa Songwe, lenye sehemu (a) na (b) napenda kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango wa kuendeleza sekta ya Kilimo (*ASDP*) ambao umeanza kutekelezwa mwaka 2006/07 ni mahsusi kwa ajili ya kuboresha sekta ya kilimo nchini.

Chini ya mpango huo, Wilaya zote nchini zinatakiwa kuandaa mipango ya Kilimo ya Wilaya *(District Agricultural Development Plans).* Wilaya ya Chunya kama ilivyo kwa Wilaya nyingine, inatazamiwa kuingiza katika mipango yake miradi ya umwagiliaji maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Sigonda lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Chunya, na wananchi wa Jimbo la Songwe, itafikiria uwezekano wa kuanzisha mradi wa kilimo cha Umwagiliaji katika bonde la Ziwa Rukwa, na kugharamiwa na *ASDP (basket fund)* iwapo wananchi wa eneo hilo wataibua Mradi wa Umwagiliaji Maji. Iwapo raslimali za Wilaya, zitakuwa pungufu kutekeleza mpango mkubwa wa Umwagiliaji, Serikali kwa kutumia wataalamu wake wa umwagiliaji waliopo kwenye Kanda watakuwa tayari kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya katika uchunguzi na hatimaye kutekeleza mradi huo.

Napenda kumshauri Mheshimiwa Mbunge kuwahamasisha na kuwashirikisha wakulima, kuibua miradi ya umwagiliaji katika mipango ya maendeleo ya Kilimo ya Wilaya ya Chunya na kuiombea fedha za utekelezaji kutoka Serikalini kupitia Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo kwa mwaka 2007/08 au hata baadaye.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uchimbaji wa visima vifupi kwa ajili ya maji ya kunywa, ni muhimu kwanza kufanya utafiti wa kiasi na ubora wa maji yaliyopo chini ya ardhi kabla ya kuchimba visima vifupi.

Kwa kuwa shughuli hizo zinahitaji fedha, wananchi wa Chunya wanashauriwa kupitia Halmashauri ya Wilaya yao kuibua miradi ya maji ya kunywa kwa utaratibu uliowekwa na Serikali chini ya Programu ya Kuendeleza Sekta ya Maji inayotekelezwa na Serikali kati ya Mwaka 2007-2025.

**MHE. DR. GUIDO G. SIGONDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwanza kabisa nimshukuru Naibu Waziri kwa kumtamka vizuri jina langu, kwa sababu limekuwa likikosewa kila wakati.

Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kuwa Serikali imekubali kwamba ina mpango wa kuanzisha mradi wa umwagiliaji katika Bonde hilo, kutokana na rutuba ambayo ipo huko kwenye bode hilo......!

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa uulize swali!

**MHE. DR. GUIDO G. SIGONDA:** Nashukuru sana, nilitaka nieleze tu kwamba sasa hivi rutuba ya bonde hilo linavutia sana mapanya, na kwa sababu tuna mpango huu Serikali imekwishaamua.

Je, hivi sasa Serikali inaweza kuanza kupambana na hao mapanya ambao huwa wanaharibu mazao wakati wa kiangazi?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA (MHE. DK. DAVID M. DAVID):** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumthibitishia Mheshimiwa Sigonda kwamba hivi sasa tunazo taarifa katika Wizara kuhusu madhara mbalimbali yanayotokea, si kwa ajili ya mapanya tu bali pamoja na ndege kwerea kwerea na wadudu waharibifu na kila taarifa zinapofika Wizarani tunashughulikia mara moja. Kwa hiyo, taarifa za Chunya kama zimekwishafika Wizarani nina hakika tayari wataalamu wamekwishapelekwa huko kuanza kuchunguza, na kama bado basi tutapeleka taarifa mara moja na kuwaagiza waende huko.

**NAIBU SPIKA:** Tunaendelea! Tulikuwa na hati za kuwasilisha mezani nyingi.

Na. 97

**Kuwaelimisha Wanawake Juu ya Kilimo**

**MHE. MARTHA UMBULLA** Aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali ya awamu ya Nne imedhamiria kuboresha sana sekta ya kilimo nchini; na kwa kuwa washiriki na watenda kazi wakubwa katika shughuli za kilimo ni wanawake:-

Je, Serikali imeweka mikakati gani ya makusudi ili wanawake waelimishwe zaidi na kujengewa uwezo zaidi kuitikia malengo hayo ya uboreshaji.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA (MHE. DAVID M. DAVID)** Alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Martha Umbulla, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:

Ni kweli kwamba wanawake wanachangia sehemu kubwa ya nguvu kazi katika shughuli za kilimo. Inakisiwa kuwa wanawake wanachangia asilimia 75 ya nguvu kazi katika kilimo.

Kupitia Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya, wadau wa kilimo wakiwepo wanawake hujengewa uwezo wa kuibua na kupanga miradi ya kilimo ambayo inalenga kujitosheleza kwa chakula na kupunguza umaskini kama malengo makuu ya programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo na MKUKUTA. Kazi hizo hufanywa na vikundi kazi vya wawezeshaji katika wilaya na kata

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo kubwa linalokikabili kilimo chetu na wakulima ni kutofuata kanuni za kilimo bora. Wakulima wetu wengi wakiwemo wanawake hawatumii mbolea wala mbegu bora. Matokeo ya hali hiyo ni uzalishaji wa mazao kwa kiwango cha chini.

Ili kuondokana na hali hiyo, Wizara yangu kwa kushirikiana na TAMISEMI, imekamilisha mkakati wa kuimarisha huduma za ugani. Chini ya mkakati huo, wataalam wapya 2500 wakiwemo wasomi wa Chuo Kikuu, wataajiriwa na kusambazwa nchini kote, ili wawe chachu ya kufikisha maarifa ya kilimo kwa wakulima. Aidha, kila mwaka vyuo vitapokea wanafunzi wapatao 3000 ili ifikapo 2011/12 kila kijiji, kata na kila tarafa itakuwa na mtaalam wa kilimo.

Wizara yangu inaendelea na mpango wa kusambaza mbolea, mbegu bora na madawa kwa ruzuku ili kuwawezesha wakulima kupata mbolea, mbegu bora na madawa kutegemea na mahitaji ya mazao.

**MHE. MARTHA UMBULLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, asante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba kuuliza maswali madogo kama ifuatavyo:

Tatizo kubwa la wataalamu wa kilimo na malalamiko makubwa ya wakulima vijijini, ni wataalamu kutowafikishia huduma inavyopaswa, kutokana na tatizo la nyezo za kufanyia kazi. Sasa sambamba na ajira hiyo aliyotaja Mheshimiwa Naibu Waziri ya kuajiri wataalamu 2500, kuna mikakati gani ya kuwa na nyezo za kutosha ili waweze kufikisha huduma hiyo kwa wakulima?

Kwa kuwa ametaja kwamba wakulima watapewa ruzuku kwa ajili ya kununua mbolea madawa na kadhalika, lakini ninavyoelewa hiyo ruzuku inaweza isitoshe na kwa kuwa tuna mfuko huu wa MKUKUTA ambao wakulima pia wamepewa fursa ya kukopa; na kwa kuwa vyombo vya fedha sasa hivi vinasita kuwakopesha wakulima, Wizara ina mikakati gani ya kuwawezesha wakulima hao wadogo ili nao waweze kukopa?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO CHAKULA NA USHIRIKA (MHE. DK. DAVID M. DAVID):** Mheshimiwa Naibu Spika, katika masuala ya nyezo ni kwamba sambamba na kuajiri maafisa ugani pamoja na kuleta mafunzo mapya kila mwaka, Serikali imejiandaa pia kununua pikipiki 2500 kwa ajili ya kata na tarafa. Baiskeli 9000

kwa maana ya kusema kwamba kila kijiji kitapata baiskeli kwa afisa ugani, kila kata itapata pikipiki na maeneo ambayo hayafiki baiskeli maeneo ya vilimani pia watapata pikipiki kwa ajili ya maofisa hao wa ugani. Sambamba na hilo kuna nyumba ambazo zitajengwa ama kukarabatiwa kwa ajili ya maafisa ugani katika ngazi ya kata vijiji na tarafa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika suala la mikopo ningewashauri na tunawahimiza akinamama na wakulima kujiunga na *SACCOS* kwa sababu ndiyo njia pekee ya kuweza kujipatia mikopo ukiachilia mbali mabenki yanayofanya kazi kwa kibiashara.

Na. 98

**Usajili wa NGOs Nchini**

**MHE. AMEIR ALI AMEIR** Aliuliza:-

Kwa kuwa imebainika kuwa kuna sheria nyingi zinazohusu usajili wa *NGOs* zilizopo chini ya Wizara mbalimbali jambo ambalo linasababisha usumbufu wa ufuatiliaji wa mwenendo, uwajibikaji pamoja na takwimu halisi za *NGOs* zilizopo nchini, mfano Sheria ya Vyama vya Siasa Na.337 ya Wizara ya Katiba na Sheria, Sheria ya Makampuni sura ya 212 (BRELA) ya Viwanda na Biashara na Sheria ya *NGO's* Na. 24 ya 2002:-

(a) Je, Serikali haioni kuwa kuna haja *NGOs* zote kuwa mahali pamoja na kufuata sheria moja chini ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto ambayo ndiyo imekabidhiwa jukumu la *NGOs*?

(b) Je, *NGOs* ngapi zilizosajiliwa katika sheria hizo?

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** Alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kujibu swali la Mhe. Ameir Ali Ameir (Fuoni), napenda kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Sheria ya NGOs Na. 24 ya Mwaka 2002, *NGO* zote husajiliwa chini ya msajili mmoja wa *NGOs* na huongozwa na masharti ya Sheria hiyo. Sheria hii inatoa fursa kwa mashirika ambayo yamesajiliwa kwenye sheria nyingine alizozitaja Mheshimiwa Mbunge, lakini anazo sifa za *NGO* kuomba cheti cha ukubalifu chini ya sheria ya *NGOs*.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia mwezi Machi, 2007 jumla ya *NGOs* 1346 zilikuwa zimesajiliwa. Kati ya hizo *NGOs* 378 zilitokana na kuomba cheti cha ukubalifu *(Certificate of Compliance)* kwa kuwa tayari zilikuwa zimesajiliwa chini ya sheria za huko nyuma.

**MHE. AMEIR ALI AMEIR:** Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Naibu Waziri kwa majibu yake ambayo yamenielimisha. Pia naomba nimuulize masuala mawili ya nyongeza. Katika idadi ya hizi *NGO* alizotueleza ni kati ya zilizokuwepo pamoja na Tanzania Visiwani au ni Tanzani Bara peke yake?

Mheshimiwa Naibu Spika, tegemeo la wengi *NGO* hizi zisaidie kuleta maendeleo ya jamii katika miji na vijiji, katika nchi nzima, na hakuna malalamiko ya kuwa *NGO* hizi nyingi zimejikita sehemu za mijini. Je, Mheshimiwa Waziri anaweza kutuambia mahali zilipo *NGO* hizi, na maendeleo gani yamepatikana hadi sasa?

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria hii ya *NGO* Na. 24 ya Mwaka 2002 si ya Muungano, kwa hiyo, taarifa nilizompa ni kwa *NGO* ambazo zipo Tanzania Bara. Ni kweli kwamba *NGO* nyingi zipo mijini, lakini hili linatokana na ukweli kwamba wanaoanzisha hizi ni watu binafsi si Serikali. Kwa hiyo, mgawanyo inategemea wale waanzishaji na wanataka kufanya shughuli gani pale walipozianzishia, ingawaje najua zipo *NGO* ambazo zinafanya kazi vijijini.
Lakini kwa sasa kwa sababu umeniomba namba nashindwa kuzitoa namba kwa sasa hivi lakini namwahidi Mheshimiwa Mbunge kutafuta *NGO* zipi zipo wapi na zinafanya nini nitampatia taarifa hizo hapo baadaye.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali yamekwisha na muda umekwisha. Waheshimiwa Wabunge mtakuta kwamba tumefanya ukatili kuna maswali ya msingi, halafu kuna maswali ya nyongeza.

Tukienda maswali ya nyongeza yakizidi basi tutaishia maswali nane ya msingi hayaulizwi, na Bunge lina siku mbili. Kwa hiyo, na majibu yanakuwa marefu sana na maswali yanakuwa marefu sana, sasa tumeanza tabia ya kutomaliza maswali yanayokuwa kwenye *Order Paper.* Naomba sana unapouliza swali usitupe habari, na Mawaziri wanapojibu wasitupe historia watupe majibu. Naomba sana tuzingatie. Baada ya kusema hayo, Waheshimiwa Wabunge nina matangazo mengi kidogo.

Kwanza, tunaonao wageni wetu Wabunge kutoka Bunge la Denmark, wakiongozwa na Mheshimiwa Piar Lansen, *Among them we have another Member of Parliament*, John Peterson, Linse Voneslin, Hon. Matern Hagon Peterson, *and we have the Member of* Parliament Hon. Rahar Baford, *I' m not sure if I' m not mistaken your good pronunciation for names*. *Then we have some staff of Parliament of* Denmark, Cenlda and Marken Clauzen.

Wamekuja hapa kwa ajili ya kutembelea, tumeanzisha utaratibu wa Mabunge kutembeleana, kwa hiyo, wamekutana na Spika, na wamekutana na Kamati inayohusika na ratiba zao watakaa hapa mpaka tarehe 20.

*So you are very much welcomed to our Parliament. Unfortunately we are forced to speak in our own language, may be you could not follow quite a number of issues which has been happened in this House, but we will give you some briefing when we are meeting in other meetings, welcome to Tanzania and to our House*. (*Makofi*)

Pamoja na sisi tena wapo wanafunzi kutoka chuo cha mipango, naomba wote wasimame, tena sio chuo cha mipango tu, chuo cha mipango vijijini, *you are all welcome*. Halafu tuna wanafunzi wa sekondari ya Dodoma, karibuni tunataka na nyie msome kwa bidii mwende Chuo cha Mipango.

Halafu ninayo matangazo mengine. Kuna Waheshimiwa, Prof. Mwakyusa na Mheshimiwa Waziri Wasira, wana wageni wao, kwanza, kuna mgeni Pascal Yakobo Gadi, kutoka Morogoro, kuna Pascal Eliasi Kasuka, kutoka Morogoro, halafu kuna Ibrahim Alex Juma, hawa wageni ni wa Mheshimiwa Wassira na Mheshimiwa Prof. Mwakyusa.

Mheshimiwa Mwijage ana wageni wake waamuzi wa mpira wa miguu wawili, kutoka Bukoba na mmoja Mwanza, kuna Lulu Mushi, kutoka Bukoba wameshatoka na Doris Fedelis kutoka Bukoba, na Lanusi Seruwano kutoka Mwanza, hawa ni waamuzi wa mpira. Mheshimiwa Mwaka anataka tuwatambue wageni wake, Zawadi Jafa, na Mwaka Mtile, ni dada zake na Mheshimiwa Mwaka. Mheshimiwa Killimbah, ameniomba niwatangazie wageni wake Mbaruku Mpanda, msaidizi wake, na Samweli Shilla Katibu wa CCM kata ya Ulemi, karibuni!

Kuna Mheshimiwa Shibuda anaomba nimtambulishe mgeni wake mama Kazimoto, Mama Kazimoto ana historia, ni Muasisi wa TANU na CCM na ni mke wa hayati Mzee Abeid Kazimoto wa Maswa, hayati Kazimoto ndiye aliyekuwa Mwenyekiti wa nyumba ya kuzaliwa TANU mwaka 1958, mwaka ambao TANU iliingia rasmi wilaya ya Maswa, Meatu, Bariadi. Sasa mama yeye amefuatana na watoto wake Hawa Kazimoto na Sauda Kazimoto na wengine wanaosoma Dodoma basi wametambulishwa pamoja na wenzao.

Mheshimiwa Tatu Ntimizi, yeye anataka tuwatambue wageni wake wanaotoka Tabora, kwanza, yeye ni Mwenyekiti wa Wabunge wa kutoka Tabora. Mheshimiwa Tatu Ntimizi, wana wageni wao kutoka mkoa wa Tabora ambao ni Waheshimiwa Madiwani wa Viti Maalum wilaya ya Tabora Mjini, naomba wasimame wote. Maana yake kama viti maalum ni akinamama karibuni sana!

Baada ya hapo naomba nisome matangazo ya kazi. Makamu Mwenyekiti Kapteni George Mkuchika, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati ya Ulinzi na Usalama wa Taifa kwamba Kamati itakutana leo tarehe 18 asubuhi baada ya maswali saa tano katika chumba 219. Mheshimiwa Shellukindo, Mwenyekiti wa Kamati ya Uwezeshaji na Biashara anaomba niwatangazie Wajumbe wake kwamba leo tarehe 18/4/2007 kutakuwa na kikao cha Kamati kitakachofanyika saa saba mchana katika ukumbi wa Na. 133. Gorofa ya kwanza.

Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda, Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi, anawatangazia wajumbe wake kwamba leo tarehe 18/4/2007 kuwa kutokuwepo na kikao cha Kamati kitakachofanyika chumba Na. 227, ghorofa ya pili, jengo la utawala.

Mheshimiwa Dr. Raphael Chegeni Mwenyekiti wa Tawi la CPA anawatangazia Wajumbe wa Kamati ya Utendaji wa *CPA* kuwa leo tarehe 18/4/2007 saa nne na nusu naona imeshapita, asubuhi ukumbi wa 432. Halafu naomba niwatangazie pia bwana Mrope, yeye sijui ni Mwenyekiti wa nini lakini anawatangazia wenzake waliohudhuria mkutano wa gesi ya *Mnazibay* wakutane kwa maelezo zaidi.

Tangazo la mwisho ni kwamba tunawatangazia Waheshimiwa Wabunge kwamba leo tarehe 18/4/07 kampuni ya simu za mikononi *ZANTEL*, itafanya maonyesho ya huduma mbalimbali inazozitoa kwa wananchi, kwa hiyo, wanakaribishwa kwenda kuziona kwenye uwanja wa tafrija za Bunge na kwamba jioni baada ya kuahirisha Bunge kutakuwa na tafrija fupi ambayo kutakuwa na mambo mengine huko, baada ya kuharishwa Bunge. Hii ina maana kati ya saa moja na nusu au saa mbili kasoro robo, kwa hiyo, kuna maonyesho sasa hivi lakini jioni pia wamewakaribisha kutangaza biashara ya *ZANTEL*, kutakuwa na mambo mengi huko pamoja na mambo ya bahati nasibu. Kwa hiyo mnakaribishwa, wenye bahati wanaweza wakapapata vitu huko, dansi na muziki yote yapo.

Baada ya hapo nasikitika Waheshimiwa Wabunge tumekuwa na matangazo marefu lakini tunaendelea na shughuli.

## MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

### Muswada wa Sheria ya Barabara wa Mwaka 2007
### (The Roads Bill, 2007)

*(Kusomwa Mara ya Pili)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, huu Muswada mlipewa siku nyingi upo katika nafasi ya kitabu hiki! Kwa hiyo, nategemea kitabu hiki ndio Muswada wenyewe. Sasa ukiangalia Muswada huu, Muswada wenyewe una kurasa chache sana, kwa hiyo majedwali yakawa ndiyo yaliyobakia. Wizara imebadilisha lile jedwali litasambaza jedwali dogo, ili mnapozungumza muwe na uhakika mna jedwali dogo namna hii. Kwa hiyo, hii ya huku mnaweza kuiacha mbali ya kurasa zile za mwanzo.

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa hii ni mara yangu ya kwanza kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu katika Mkutano huu, awali ya yote na mimi napenda kuungana na Wabunge wenzangu waliotangulia kusema kuwapongeza kwa dhati Wabunge wapya waliojiunga na Bunge lako Tukufu nikianzia na Mheshimiwa Florence Kyendesya, Viti Maalum CCM, na Mheshimiwa Mbunge mpya wa Jimbo la Tunduru, Mheshimiwa Mtutura Abdallah Mtutura, CCM, tunawakaribisheni sana katika Bunge na tunawatakia yote yaliyo mema.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, napenda nitoe salaam zangu za rambirambi kwa familia ya marehemu aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Kilosa na baadaye Gairo, Marehemu Dr. Aaron Chiduo, na familia za Watanzania wenzetu zilizoathirika kutokana na ajali ya basi iliyotokea katika eneo la Lembeni wilayani Mwanga. Tunaomba

Mwenyezi Mungu azipe familia za marehemu hao moyo wa ujasiri na uvumilivu katika kipindi hiki cha majonzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maneno hayo ya utangulizi, naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria ya Barabara wa Mwaka 2007 yaani *The Road Bill,* 2007 pamoja na marekebisho yaliyomo kwenye orodha ya marekebisho, sasa usomwe mara ya pili.

Mheshimiwa Naibu Spika, madhumuni ya Muswada huu ni kutunga sheria mpya ya barabara ambayo itafuta sheria inayotumika hivi sasa yaani *the Highway Act* Sura ya 167 ya Sheria za nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria inayotumika sasa hivi ilitungwa mwaka 1932 kwa lengo la kuendeleza na kufanyia matengenezo mtandao wa barabara nchini. Tangu mwaka huo sheria hii imefanyiwa marekebisho kabla na baada ya uhuru mwaka 1939, 1942, 1959, 1992 na marekebisho ya mwisho yalifanyika mwaka 1993.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada wa Sheria ya Barabara umeoanishwa na sera mpya zilizopo, sera hizo ni pamoja na Sera ya Uchukuzi ya mwaka 2002 na Sera ya Ujenzi ya mwaka 2003.

Kama itakavyokumbukwa Sera ya Taifa ya Uchukuzi inatoa mwongozo na dhamira ya jinsi Sekta ya Uchukuzi itavyoendelezwa hususan kwenye usafiri na usafirishaji kwa njia ya barabara. Aidha, Sera ya Taifa ya Ujenzi inafafanua vizuri kuhusu Sekta ya Ujenzi ikiwa ni pamoja na shughuli za ujenzi wa barabara zitakavyotekelezwa kwa kuzingatia viwango na taratibu, hivyo, Muswada huu iwapo utapishwa na Bunge lako Tukufu utakuwa ni nyanzo muhimu itakayowezesha utekelezaji wa misingi iliyomo kwenye sera hizi kwa kuipa nguvu za kisheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia Muswada huu mkazo unawekwa katika ushirikishwaji wa sekta binafsi katika ujenzi, usimamizi na matengenezo ya barabara na madaraja. Hatua hii inaendana na Sera ya Uchukuzi ya mwaka 2002 na Sera ya Ujenzi ya mwaka 2003, ushiriki wa sekta binafsi kwa njia mbalimbali pamoja na utaratibu wa *Build Operate Transfer BOT* na *Build Old Operate and Transfer BOOT,* utasaidia kuboresha mtandao wa barabara kwani fedha za Serikali peke yake hazitoshelezi kwa kazi za ujenzi na matengenezo ya barabara nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu umegawanyika katika sehemu 10 pamoja na majedwali 5 kama ifuatavyo. Sehemu ya kwanza inaweka masharti ya awali kama jina la sheria, tafsiri ya maneno mbalimbali yaliyotumika katika Muswada (*Application of Interpretation).* Katika kipengele hiki masuala mengi ya msingi

yametafsiriwa ili kurahisisha uelewa na utekelezaji wa sheria yenyewe. Tafsiri hizi zipo katika kifungu cha tatu cha Muswada huu ikiwa ni pamoja na tafsiri ya maneno barabara binafsi na barabara za umma, maneno bod*i* za barabara za mikoa, maneno barabara kuu, barabara za mikoa na barabara za wilaya. Yapo pia maneno mamlaka ya barabara (*Road Authority)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, tafsiri ya mamlaka ya barabara ni pana na inajumuisha Halmashauri za Wilaya, Miji, Majiji, Vijiji pamoja na Wakala wa Barabara nchini (*TANROADS).* Pia maneno thamani za barabara yamepewa tafsiri ambazo zinajumuisha taa za kuongozea magari barabarani, alama za barabarani, ukuta, uzio wa barabara ambazo kwa pamoja zinaelekeza matumizi sahihi ya barabara zetu. Maneno Wakala wa Barabara yamefafanuliwa kwa maana ya *TANROADS,* ni wakala ambao Waziri mwenye dhamna ya barabara amekasimu mamlaka yake kwa jukumu la kusimamia ujenzi na matengenezo ya barabara za Kitaifa ambazo ni barabara kuu pamoja na barabara za mikoa. Vile vile maneno Mamlaka za Mitaa yamefafanuliwa (*Local Government Authorities)* ambazo zitakasimiwa na Waziri mwenye dhamana ya barabara jukumu la kusimamia ujenzi na matengenezo ya barabara za wilaya, miji, majiji pamoja na barabara za vijijini kama ilivyofafanuliwa katika kifungu cha 12 cha Muswada huu. Neno tozo na lenyewe limefafanuliwa miongoni mwa maneno mengi ambayo yamefafanuliwa kwa ajili ya matumizi ya barabara (*User Charges)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya pili ya Muswada inaweka masharti kuhusu usimamizi wa barabara kwa kuanisha majukumu ya Wizara ya Miundombinu, uteuzi wa Mamlaka za Barabara na uanzishajiwa bodi za barabara za mikoa na majukumu ya bodi hizo. Aidha sehemu hii inaelezea majukumu ya mamlaka za barabara, jukumu la msingi la mamlaka hizi litakuwa kujenga, kukarabati na kusimamia barabara ambazo zimekasimiwa kwa mamlaka hizo. Kupitia Muswada huu suala zima la usimamizi na uongozi katika sekta ndogo ya barabara (*Road Management)* limeboreshwa ili lilingane na mabadiliko ya kisera yanayoendelea hapa nchini, mabadiliko hayo ni pamoja na kuanzishwa kwa mfuko wa barabara na wakala wa barabara yaani *TANROADS*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia mfuko wa barabara uwezo umejengwa na utaendelea kujengwa na Serikali kwa kuzihudumia barabara kwa njia ambayo ni endelevu. Wakala wa barabara *TANROADS* nao utaendelea kuimarishwa ili uweze kutoa huduma kwa ufanisi zaidi. Vile vile *board* ya *TANROADS* itaundwa upya ili kushirikisha sekta binafsi na wadau wengine muhimu wa barabara. Aidha, majukumu ya Wizara yamewekwa bayana ambayo ni pamoja na kuandaa na kusimamia sera, kuandaa miongozo na viwango kwa kazi za barabara, kuandaa mipango mikakati ya kuendeleza barabara nchini (*Strategic Plans*) kuhamasisha ushiriki wa sekta binafsi katika ujenzi, usimamizi na matengenezo ya barabara nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu hii pia inampa Waziri mwenye dhamana ya barabara jukumu la kuteuwa mamlaka ya barabara. Hii ina maana kwamba Waziri mwenye dhamana ya barabara anaendelea kuwa mmoja lakini amepewa uwezo wa kukasimu majukumu ya uendelezaji na usimamizi wa barabara kwa taasisi au mamlaka

nyinginezo. Kama nilivyosema hapo awali mamlaka hizo ni kama vile Serikali za Mitaa, *TANROADS* yenyewe, *TANAPA* na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya tatu ya Muswada inafafanua barabara za umma na zile ambazo ni za binafsi (*Private Roads*). Aidha, sehemu hii inaweka wazi masharti kuhusu kutangazwa kwa barabara za umma na pia madaraja yaani *classification* ya barabara hizo. Madaraja na mtandao wa barabara nchini (*Classification of Roads)* yameainishwa kwa uwazi katika kifungu cha 12 cha Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, madaraja hayo ni kama ifuatavyo: kwanza, barabara za Kitaifa zinazojumuisha barabara kuu ambazo zinaunganisha nchi yetu na nchi jirani au barabara zinazounganisha Makao Makuu ya Mkoa mmoja na Makao Makuu ya Mkoa mwingine au zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kundi la pili ni barabara za mkoa ambazo zinaunganisha Makao Makuu ya Wilaya na Makao Makuu ya Mkoa au zinazounganisha barabara kuu na Makao Makuu ya Mkoa au Makao Makuu ya Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kundi la tatu ni barabara za Wilaya ambazo zinaunganisha Makao Makuu ya Wilaya, Tarafa na Tarafa, Tarafa na Kata, Kata moja na Kata nyingine, Kata na Kijiji, Kijiji na Kijiji pamoja na barabara za Mijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, jedwali la kwanza la Muswada huu linatoa hali halisi ya mtandao wa barabara uliopo hivi sasa kwa upande wa Tanzania Bara kwa maana ya barabara kuu na barabara za mkoa zinazohudumiwa na *TANROADS* na barabara za wilaya zinazosimamiwa na TAMISEMI. Jedwali hilo limefanyiwa kazi na kama ulivyosema sasa hivi ni sehemu ya orodha ya marekebisho yaliyogawiwa kwa Waheshimiwa Wabunge na jedwali hilo litaendelea kufanyiwa kazi ili kuingiza barabara zote hasa barabara za wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunawaomba Waheshimiwa Wabunge watusaidie katika kuhakiki daftari yaani *inventory* ya mtandao wa barabara zetu. Baada ya sheria hii kuanza kutumika barabara hizo zitawekwa kwenye madaraja kulingana na vigezo viliainishwa kwenye kifungu cha 12 cha Muswada huu. Baada ya hapa Waziri mwenye dhamana ya barabara atatangaza barabara hizo pamoja na upande wa hifadhi ya kila barabara kupitia gazeti la Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba jedwali hili kwa sasa halijumuishi maombi mbalimbali ambayo yamepokelewa Wizarani kutoka mikoani. Kama nilivyosema maombi hayo yatashughulikiwa kulingana na vigezo vilivyowekwa katika kifungu cha 12 cha Muswada huu pindi sheria mpya ya barabara itakapoanza kutumika. Aidha Waziri mwenye dhamana ya barabara atashauriana na Waziri mwenye dhamana ya TAMISEMI ambaye amekasimiwa mamlaka ya kusimamia barabara za wilaya wakati wa kuziweka katika madaraja mbalimbali, hili ni suala la msingi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri mwenye dhamana ya barabara anapaswa kushauriana na Waziri mwenye dhamana ya barabara za wilaya wakati wa kuziweka katika madaraja hayo kwa sababu suala la kupandisha au kushusha daraja mara hizo ni suala la msingi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha sehemu hii ya tatu ya Muswada inaweka kifungu kuhusu fidia ya mali itakayochukuliwa kwa ajili ya upanuzi wa barabara au ujenzi wa barabara mpya. Fidia hii ni kwa mali yoyote endapo barabara itapanuliwa kutoka daraja moja kwenda daraja lingine kwa maana ya kwamba hifadhi ya barabara hiyo itasogea kutoka upana wa awali wa hifadhi hiyo ya barabara na hivyo kuingilia mali ya mtu. Pili, mtu yeyote atakayeingilia hifadhi ya barabara kwa maana ya kukiuka barabara atatakiwa kuondoa mali zake kwa gharama zake na endapo ataondolewa mamlaka husika basi itabidi mtu huyo alipe gharama za kufanya kazi hiyo au kushtakiwa kwa mujibu wa sheria hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya nne inahusu masuala ya upimaji wa eneo la ujenzi wa barabara, utafutaji wa vifaa vya ujenzi, ujenzi wa kambi kwa ajili ya kuanza kazi za ujenzi, matumizi ya eneo la ziada la barabara na kadhalika. Mfano, katika kifungu cha 29 matumizi ya usimamizi wa hifadhi ya barabara yamezingatiwa. Muswada unaweka bayana kuwa matumizi mahsusi ya hifadhi ya barabara ni kwa ajili ya upanuzi wa barabara na si vinginevyo. Mamlaka husika inaweza kutoa kibali kwa ajili ya matumizi ya muda ya vibao vya matangazo, minara ya simu, nguzo za umeme na kuandaa au kutandaza mabomba ya maji na nyaya za simu. Hata hivyo, mwombaji atapaswa kuondoa kwa gharama zake miundombinu aliyojenga ndani ya hifadhi ya barabara endapo mamlaka husika itakuwa inapanua barabara hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya tano inaweka mkazo kwenye masuala ya usalama wa barabarani hususan matumizi ya alama za barabarani, kiwango cha mwendo wa kasi na usalama wa watumiaji wa barabara. Masuala haya ni pamoja na kuweka alama za usalama barabarani, kuweka njia za watembea kwa miguu na kuweka viwango vya uzito wa mizigo barabarani kwa lengo la kulinda barabara zisiharibiwe, faini kali zinapendekezwa zitozwe kwa watakaozidisha uzito wa mizigo. Maudhui ya sehemu hii ni kulinda usalama wa wananchi pamoja na barabara zenyewe ambazo tunazijenga kwa gharama kubwa, fedha za umma ambazo zinatumika katika kuzijenga barabara hizi na hivyo lazima tuzitunze kwa gharama yoyote barabara hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya sita inahusu ujenzi wa barabara za pembeni (*Excess Roads*), pia sehemu hii inatoa masharti kuhusu maombi ya namna ya kushughulikia maombi ya ujenzi wa barabara za pembeni na haki ya kukata rufaa kwa mwombaji ambaye hataridhika na uamuzi wa mamlaka husika. Ufafanuzi wa jinsi ya kufanya maombi umetolewa katika jedwali la pili la Muswada.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya saba ya Muswada inazipa Mamlaka za Barabara nchini uwezo wa kuweka masharti kuhusu matumizi ya barabara, masharti hayo ni pamoja na wakati wa kufanya matengenezo ya barabara ambapo barabara inaweza kufungwa, kuweka mchepuo ili kupisha matengenezo. Aidha, mamlaka husika inapewa

uwezo kisheria wa kuweka masharti ya kudhibiti mwendo wa kasi wa magari, kudhibiti uzito wa mizigo na upana wa mzigo unaoruhusiwa barabarani kwa madhumuni ya kuhakikisha usalama wa watumiaji wa barabara zetu na pia kulinda hali ya barabara. Adhabu zilizowekwa chini ya sheria ya usalama barabarani ya mwaka 1973 zitatumika kwa mtu yeyote atakayekiuka masharti yatakayowekwa na mamlaka husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, na hapa niseme Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Usalama wa Raia tunakamilisha sera ya usalama barabarani na hatimaye tutawasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu Muswada wa kusimamia suala zima la usalama barabarani na hasa kutokana na ajali mbaya ambazo zinaendelea kutokea nchini mwetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya nane inahusu vyanzo vya fedha za ujenzi na matengenezo ya barabara. Aidha, taratibu za ukaguzi wa mahesabu na uwasilishwaji wa taarifa za hesabu Bungeni zimeainishwa, viwango vya fedha za ujenzi na matengenezo ya mtandao wa barabara nchini ni pamoja na bajeti ya Serikali, mfuko wa barabara, misaada na mikopo, mapato ya Serikali za Mitaa na ushiriki wa sekta binafsi kama sera zilizopo zinavyoelekeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, vyanzo hivi vinaendana na mabadiliko ya sera yanayoendelea nchini nimeelezea sera ya uchukuzi ya mwaka 2002 na sera ya ujenzi ya mwaka 2003 na kuanzishwa kwa mfuko wa barabara pamoja na wakala wa barabara (*TANROADS)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya tisa inaainisha makosa mengi na adhabu mbalimbali dhidi ya ukiukwaji wa sheria hii, kwa mfano, itakuwa ni kosa kwa mtu yeyote kuharibu daraja au kuweka mawe, kokoto, mchanga au majani barabarani kama gari lako limeharibika halafu unayaacha hapo hapo, au kuendesha gari la aina yoyote hasa haya madaladala kwenye njia za watembea kwa miguu, au kumwaga mafuta kama vile petroli au dizeli kwenye barabara za umma. Aidha, sheria inaipa mamlaka inayohusika na usimamizi wa barabara hizi ya kufidiwa gharama iliyotumika katika kufanya marekebisho ya barabara kutoka kwa mtu aliyefanya uharibifu wa barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya sasa ni kwamba mtu anaweza kufanya uharibifu lakini hakuna uwezo wa kisheria wa kumbana mhusika ili arejeshe gharama za uharibifu uliotokea, ni kifungo tu na faini lakini faini haiendi kutengeneza barabara hiyo sasa unarejesha gharama za uharibifu uliotokana na kazi yako hiyo. Sheria hii inampatia mamlaka ya kisheria Waziri mwenye dhamana ya barabara kutayarisha kanuni za kutekeleza sheria na kuzirekebisha kanuni hizo pale inapohitajika kulingana na mahitaji ya wakati. Kanuni hizo ni pamoja na programu za kuelimisha umma kuhusu sheria hii ili kurahisisha utekelezaji wake. Pili, kuweka miongozo ya ushiriki wa sekta binafsi katika shughuli za barabara na tatu kuweka *classification* yaani madaraja ya barabara na mipaka yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala zima la utunzaji wa samani za barabara (*Roads furniture)* limezingatiwa katika Muswada huu. Litakuwa kosa kwa mtu yeyote kuharibu

thamani za barabara kama vile madaraja, vyuma vya pembeni mwa barabara, mawe ya mipaka ya barabara au kuchukua michanga kama nilivyosema, kokoto na mawe kutoka kwenye hifadhi ya barabara, kumwaga mafuta na kutupa takataka barabarani na atakayetenda kosa hili au makosa yaliyoonyeshwa katika sehemu ya tisa ya Muswada atatozwa faini isiyopungua Sh.1,000,000/= au kifungo kisichozidi miaka mitatu au vyote viwili kwa pamoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya 10 inahusu masharti ya jumla kama mamlaka ya Waziri kuweka kanuni na kinga za watumishi wa mamlaka za barabara pale wanapotekeleza majukumu yao kwa nia njema. Aidha, Muswada wa sheria mpya ya barabara unampa Waziri mwenye dhamana ya barabara mamlaka ya kuweka kanuni zitakazofafanua masuala mbalimbali yaliyomo chini ya sheria hii na hivyo kurahisisha utekelezaji wa sheria yenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo limepewa msisitizo kupitia Muswada huu ni lile la matumizi ya nguvu kazi *(labour base technology)* katika ukarabati matengenezo na ujenzi wa barabara na hasa barabara za vijijini. Utaratibu huu utawezesha matumizi ya raslimali za ndani katika ujenzi na matengenezo ya barabara zetu utatoa ajira na hivyo kusaidia kupambana na umaskini hasa katika maeneo ya vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu una majedwali matano kama ifuatavyo: sehemu ya kwanza ni daftari yaani, *inventory* ya barabara zote nchini pamoja na madaraja ya barabara hizo, jedwali hili linaonyesha barabara zote za Kitaifa na Wilaya. Waziri wenye dhamana ya barabara anapewa mamlaka ya kuongeza mtandao wa barabara za Kitaifa kupandisha au kushusha daraja la barabara husika kadri itakavyoonekana inafaa kulingana na vigezo vilivyowekwa katika kifungu cha 12 cha Muswada. Kama nilivyotangulia kusema kwa barabara za wilaya Waziri Mwenye hamana ya barabara atashauriana na Waziri anayehusika na Serikali za Mitaa wakati wa kuweka kwenye madaraja barabara hizo, au wakati wa kuongeza barabara hizo, au wakati wa kupandisha, au kushusha daraja barabara za Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, jedwali la pili linahusu maombi ya kujenga barabara pembeni *(Application for Leave to Construct a road of Access)* na kibali cha kujenga barabara ya pembeni, hizi ni fomu maalum za kuomba na kuruhusiwa kujenga barabara za pembeni. Mwombaji atatakiwa kujaza fomu na kuiwasilisha kwa mamlaka ya barabara husika ambapo mamlaka hiyo ikiridhika itajaza fomu (b) kutoa kibali kwa mwombaji ili ajenge barabara ya pembeni ya kuunganisha na barabara ya umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, jedwali la tatu linahusu hati ya kushikilia au kuuza mali *(form summary warrant)*. Hati hii itatolewa na hakimu kumtaka dalali wa mahakama kukamata mali inayohamishika kutokana na ukiukwaji wa sheria ya barabara. Aidha, hakimu anaweza kumuamuru dalali kuuza mali hiyo ili kufidia gharama au faini kutokana na ukikwaji wa sheria ya barabara. Katika shauri la kufidia gharama ya matengenezo ya barabara iliyoharibiwa kutokana na ukiukwaji wa sheria hii hati ya

mamlaka ya barabara husika kuhusu gharama za matengenezo itachukuliwa kama ushahidi tosha wa madai hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, jedwali la nne linahusu taratibu na mwenendo wa mikutano ya bodi ya barabara ya mikoa *(constitution and proceedings of regional roads board)*, jukumu kubwa la bodi hizi ni kumshauri Waziri wenye dhamana ya barabara juu ya masuala yote yanayohusu ujenzi, usimamizi na matengenezo ya barabara katika mkoa husika. Mwenyekiti wa bodi hiyo atakuwa Mkuu wa Mkoa kama ilivyo sasa na Waheshimiwa Wabunge wa Majimbo na pia Wabunge wawili wa viti maalum au wanaoteuliwa na Mheshimiwa Rais wanaoishi katika mkoa husika, bodi itakuwa na wajumbe watatu kutoka sekta binafsi ili kutekeleza dhana ya ushiriki wa sekta binafsi. Jedwali la tano linahusu bodi ya *TANROADS* ambayo inaundwa upya kwa kuingiza sura hiyo, jukumu kubwa la bodi hii ni kumshauri Waziri Mwenye Dhamana ya Barabara kuhusu utendaji wa *TANROADS* katika kusimamia ujenzi na matengenezo ya barabara kuu na barabara za mikoa, mwenyekiti wa bodi hii atateuliwa na Rais kutoka sekta binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni matumaini yangu kuwa Muswada wa Sheria ya Barabara utakidhi mabadiliko ya kisera, kiuchumi na kiteknolojia yanayoendelea kutokea nchini na Duniani katika masula ya barabara. Kwa mantiki hiyo ujenzi, matengenezo na usimamizi wa mtandao wa barabara nchini utafanyika chini ya sheria iliyo bora na hivyo utatoa tija kwa jamii na katika ukuaji wa uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kumaliza hotuba yangu niruhusu nichukue nafasi hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa wadau mbalimbali walioshiriki kutoa maoni yao wakati wa *public yearly* iliyofanyika mjini Dar es Salaam iliyofanyika tarehe 04 Aprili, 2007 na tarehe 05 Aprili, 2007. Maoni na ushauri wao umesaidia sana kuboresha Muswada huu, tunawashukuru sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, nitakuwa mchoyo wa fadhila nisipotambua mchango wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu chini uenyekiti wa Mheshimiwa Mohamed Hamis Missanga, Mbunge wa Singida Kusini kwa ushirikiano wa karibu walionipa wakati wa *public yearly* na pia wakati wa kuchambua Muswada huu. Uchambuzi wa kina wa Muswada huu uliofanywa na Kamati ya Bunge ya Miundombinu ndio umewezesha Muswada huu uweze kuwasilishwa leo hii mbele ya Bunge lako Tukufu, ninaishukuru sana Kamati ya Miundombinu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia nitoe shukrani zangu za dhati kwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mwandishi Mkuu wa Sheria kwa kuandaa Muswada huu pamoja na orodha ya marekebisho iliyogawiwa kwa Waheshimiwa Wabunge hivi punde. Ninawashukuru sana Naibu Mawaziri wa Wizara yangu Mheshimiwa Dr. Maua Abeid Daftari na Mheshimiwa Dr. Milton Makongoro Mahanga pamoja na watendaji wote wa Wizara ya Miundombinu kwa ushirikiano wao katika kuandaa Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya ninayo heshima ya kuwasilisha Muswada wa Sheria ya Barabara wa mwaka 2007 ( *The Roads Bill 2007)* ambao utafuta

sheria iliyopo sasa ijulikanayo kama *The Highways Act*, Sura ya 167 ya sheria za nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa unyenyekevu mkubwa naliomba Bunge lako Tukufu lijadili na kisha liupitishe Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Hoja hiyo imeungwa mkono, lakini kabla sijamwita Mwenyekiti wa Kamati iliyohusika na Muswada huu napenda kutangaza tangazo hili lilichelewa. Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Maliasili na Mazingira anaomba wajumbe wake wa Kamati hiyo wakutane saa 7 katika Ukumbi wa Msekwa.

Sasa nitamwita Mwenyekiti au Mwakilishi wake aliyeshughulikia hoja hii. Naona anakuja Mwakilishi wake.

**MHE. HAFIDH ALI TAHIR:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nashukuru kupata fursa hii ili niweze kutoa maoni ya Kamati ya Bunge ya Miundombinu kuhusu Muswada wa Sheria ya Barabara ya mwaka 2007 (The Road Bill 2007) kwa mujibu wa Kanuni za Bunge Kanuni ya 70 (2), Toleo la mwaka 2004.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote naomba niitumie fursa hii kutoa salamu zangu za rambirambi kwa familia, ndugu, jamaa na marafiki wa Marehemu Dr. Aaron Chiduo, aliyefariki tarehe 13 Aprili, 2007. Marehemu alikuwa Waziri wa Afya kwa miaka mingi katika Serikali za Awamu zilizopita na tunamkumbuka kwa utendaji wake na mchango wake katika taifa hili. Mwenyezi Mungu ailaze Roho ya Marehemu Pahali Pema, Amin!

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, naomba niitumie fursa hii pia kumpongeza Mheshimiwa Mtutura Abdallah Mtutura kwa ushindi alioupata katika kinyang'anyiro cha uchaguzi mdogo wa Jimbo la Tunduru, ushindi uliompa uhalali kuwa Mbunge wa Jimbo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kuanza kwa Mkutano huu wa Saba wa Bunge, Kamati yangu ilipewa kazi ya kuupitia na kuujadili Muswada wa Sheria ya Barabara 2007 ambao unafuta Sheria ya Barabara *The High Way Act,* Sura ya 167, Sheria ya Barabara inayotumika sasa iliyotungwa mwaka 1932 ambayo haikidhi mahitaji ya sasa ya barabara.

Napenda kuchukua fursa hii kuliarifu Bunge lako tukufu kuwa Kamati yangu ilitekeleza kazi hiyo kikamilifu kwa kushirikiana na Waziri wa Miundombinu pamoja na watendaji wa Wizara husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 69 (2) ya Kanuni za Bunge, Toleo la 2004, Kamati ilipata fursa ya kukutana na wadau husika wa Muswada wa Sheria ya Barabara 2007 na kupata maoni na mapendekezo yao. Maoni ya wadau hao

yaliwasilishwa mbele ya Kamati Aprili, 2007 katika vikao vilivyofanyika Ofisi Ndogo ya Bunge pale Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inawapongeza kwa dhati wadau wote muhimu kwa ushiriki wao katika kuandaa Muswada huo ambao ni kutoka Sekta ya Taasisi mbalimbali za Kiserikali na zisizo za Kiserikali kama vile Wakala wa Barabara Tanzania *TANROADS*, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Chuo cha Teknolojia Dar es Salaam, Bodi ya Wasajili na Wakadiriaji Majengo, Bodi ya Wahandisi, Bodi ya Wakandarasi, Baraza la Taifa la Ujenzi, KUWATA, TAZAMA, Chama cha Wenye Mabasi Yaendayo Mikoani, Baraza la Taifa la Udhibiti Mazingira, Mamlaka ya Udhibiti na Usimamizi wa Usafiri wa Majini, Anga na Nchi Kavu, Shirika la Reli Tanzania, Mfuko wa Taifa wa Barabara, Washirika wa Maendeleo wakiwemo Ubalozi wa Norway, *European Union*, Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo Afrika pamoja na wengine wengi ambao kwa wakati huu sitaweza kuwataja wote lakini wameshiriki kwa namna moja ama nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati kwa kutambua umuhimu wa kushirikisha Wizara mbalimbali katika maandalizi ya Muswada huu chini ya Wizara husika ya Miundombinu Ofisi zifuatazo nazo tumeshirikiana katika kufikia muafaka ambao tunauleta mbele ya Bunge hili Tukufu. Ofisi zenyewe ni pamoja na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji, Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI, Wizara ya Usalama wa Raia na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuleta Muswada huu ambao utawezesha kuwepo kwa Sheria mahususi itakayokidhi mahitaji yaliyopo katika Sekta ya Barabara Tanzania. Vilevile Sheria hii inakusudia kuboresha masharti kuhusu uendelezaji, usimamiaji na ukarabati wa Mtandao wa Barabara Tanzania ambayo itaendana na mabadiliko ya kiuchumi, kisayansi na kiteknolojia.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote Kamati inaipongeza Serikali kwa kukubali kufanya marekebisho ya Sheria hii ambayo yameenda sambamba na sera mpya zilizopo sasa kama vile Sera ya Ujenzi ya 2003 na Sera ya Taifa ya Uchukuzi 2002, hii italeta ufanisi katika utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo hususan Barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, malengo ya Muswada huu ni mzuri kwa manufaa ya maslahi ya Maendeleo ya Taifa la Tanzania. Kamati inaishauri kuwa Serikali itoe kipaumbele katika kutenga fedha za kutosha kwa ajili ya miradi ya barabara, kuwepo kwa sera za Sheria nzuri za barabara hakutakuwa na maana yoyote iwapo hakutakuwa na fedha za kukamilisha malengo yanayokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuzungumzia masuala ya marekebisho na uboreshaji masharti kuhusu utekelezaji, usimamizi na ukarabati wa mtandao wa barabara nchini, Kamati imeona kuwa fedha zinazotengwa kwa shughuli hii ni kidogo mno na haziwezi kukidhi matarajio ya Sheria hii.

Tukichukua mfano wa fedha zinazotolewa kwa Mfuko wa Barabara ni shilingi bilioni 78 tu kwa mwaka ambazo ni sawa na 35% ya mahitaji ya shilingi bilioni 221 zinazotakiwa. Serikali ikiendelea na mtindo huu hatuwezi kuwa na barabara nzuri na matatizo sugu ya usafiri hayawezi kutatuliwa.(*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 44 cha Muswada kinaelezea Vyanzo vya Mapato kwa ajili ya kugharamia matengenezo ya barabara, lakini lipo tatizo sugu la ukosefu wa fedha za uhakika katika miradi ya barabara na Kamati inaishauri kuwa Serikali iwe na mikakati madhubuti na kudumu na kuimarisha mifuko yaani vyanzo vya fedha kama vile Mfuko wa Bodi ya Barabara *(RFB)* na tozo yaani kodi mbalimbali kama vile kuanzisha ada ya mwaka ya kutumia barabara kwa wenye magari, kuongeza kodi kwa wanaosajili magari mapya yenye injini kubwa, kuongeza ada ya uandikishwaji magari mpaya na hii itapunguza kuwa tegemezi wa fedha za wafadhili na kukamilisha miradi ya maendeleo kwa wakati unaotakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Bodi ya Mfuko wa Barabara *(RFB)* ndiyo Mhimili wa uhai wa barabara zetu kwa kutoa fedha za matengenezo muhimu ya barabara Kamati inaishauri kuwa RFB iruhusiwe kuongeza kiwango cha tozo ya mafuta kwani kiwango cha sasa cha shilingi 100 kwa lita ni kidogo mno na hakitoshi kutunisha mfuko huo. Kwa kufanya hivyo itaisaidia kuhudumia matengenezo ya awali ya barabara kabla uharibifu haujawa mkubwa na kusababisha gharama zaidi katika kukarabati kwake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hivi sasa Serikali inapitia mikataba ya uwekezaji katika Sekta ya Madini, kwa hiyo basi, Kamati inaishauri kuwa Serikali iangalie uwezekano wa kuwafanya wawekezaji hao walipe kodi ya mafuta kwani kusafirisha mafuta kwa wingi kwenda migodini na kwa wakati huo huo ni watumiaji wakuu wa barabara. Kwa kufanya hivyo, hiyo kodi itakayopatikana itasidia kutunisha Mfuko wa Barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuiwezesha Tanzania kuingia katika ushindani wa masoko ya kiuchumi ya Afrika Mashariki na Nchi za *SADC.* Serikali iweke mikakati ya kuibua vyanzo vya fedha za miradi ya barabara na kuikamilisha mapema pale ujenzi unapoanza kwani nchi jirani zinazotuzunguka zina barabara nzuri na za kisasa hivyo haitakuwa busara kwa Tanzania kubaki nyuma na kuendelea kuwa na barabara mbovu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuleta maendeleo ya dhati na maisha bora kwa kila Mtanzania Kamati inashauri kuwa sasa umefika wakati wa kukuza mtandao wa barabara nchi nzima na si kujenga barabara zilezile siku zote. Aidha, mtandao huo uendane sanjari na miundombinu ya Reli pamoja na usafiri wa majini kwani Sekta hizo hutegemeana katika kufungua njia za kiuchumi na kuunganisha mikoa na nchi jirani za maeneo yetu.

Kama ambavyo tumeshuhudia athari wanazozipata wananchi kutokana na barabara mbaya na nyingine kutokamilika kumekuwepo na ajali nyingi katika nchi yetu. Lakini hiyo haitoshi kuna upotevu wa maisha ya watu na raslimali zao pamoja na kupoteza muda mwingi wa kuchangia katika kuinua maendeleo ya Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutambua nafasi muhimu waliyonayo wadau katika kuchangia maendeleo ya Barabara, Kamati ba inaishauri kuwa Serikali iweke utaratibu maalum wa kutengeneza Kanuni utakaowawezesha wadau wengi zaidi kushiriki katika ujenzi wa barabara hapa nchini. Ushirikishwaji wa Wataalam, Washauri, Waelekezaji na Wadau wengine utaleta mabadiliko halisi na ya haraka mno.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 44 cha Muswada huu vilevile kinatoa fursa kwa kuwashirikisha watu binafsi katika Sekta ya Barabara ili rasilimali zao zitumike, Kamati inapendekeza kuwa Kanuni na Taratibu zitakazotungwa ziainishe bayana na kuruhusu utaratibu wa kuwashirikisha *Private Public Partners* katika Miradi ya Barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inasikitishwa na miradi mingi ya Barabara kusuasua na kutokamilishwa kwa wakati, Kamati inaishauri kuwa Serikali kupitia na kuangalia upya mikataba ya ujenzi wa barabara hususan miradi maalum ili kubaini kwa nini miradi hii imechelewa kukamilika kulingana na Mikataba na Taarifa iwasilishwe hapa Bungeni.

Kamati inaishauri kuwa Wizara ya Miundombinu iongeze juhudi katika kuwasimamia Makandarasi ili miradi hii iweze kukamilishwa kwa wakati na kwa watakaoshindwa kukamilisha miradi kwa mujibu wa Mkataba wachukuliwe hatua kali. Aidha, hatua kali zichukuliwe kwa watakaobainika kuhusika na kutoa au kupokea rushwa wakati wa kusaini mikataba.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 31 kinazungumzia usalama barabarani ikiwa ni pamoja na alama za barabarani. Kamati inapendekeza kuwa pamoja na Muswada huu wa barabara kuwa na mapendekezo mazuri kuhusu masuala ya usalama barabarani na matumizi ya alama za barabarani bado juhudi za makusudi zinahitajika katika kuelimisha jamii. Wizara ya Miundombinu iwe na *Program* maalum na za mara kwa mara katika kutoa elimu kwa umma kwa lengo la kutunza na kuhifadhi barabara zetu ambazo hujengwa kwa gharama kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu umeainisha vyema masuala ya utunzaji na hifadhi za barabara. Kamati inasisitiza kuwa hatua kali ziwe zikichukuliwa kwa wale ambao watakiuka Sheria na taratibu zitakazowekwa hasa kwa wanaozidisha uzito wa magari au kupitisha magari kwenye barabara ambazo zinaruhusu uzito mdogo.

Kamati inatoa wito kwa vyombo husika ikiwa ni pamoja na Askari wa Usalama wa Barabarani wasimamie Sheria ipasavyo na kuwachukulia hatua kali wanaohusika na kukiuka Sheria na utaratibu wa barabarabni.

Aidha, kitengo cha mizani kiimarishwe, viongezwe vituo vingine na kupatiwa vifaa vya kisasa ili kuongeza ufanisi na kuwa sahihi katika suala la upimaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inasikitishwa na utamaduni uliojengeka wa kutokarabati barabara kwa wakati muafaka, barabara inaweza kuanza na shimo dogo na hatimaye kuwa handaki kana kwamba hakuna wahandisi, wakaguzi wala anayeona mashimo hayo.

Kamati inapendekeza kuwa Wizara ya Miundombinu iwe na utamaduni au utamaduni maalumu wa kufanya ukarabati na ukaguzi wa barabara wa mara kwa mara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Hitimisho. Naomba nitumie nafasi hii kwanza kumshukuru Mheshimiwa Andrew John Chenge, Waziri wa Miundombinu, Mheshimiwa Dr. Maua Abeid Daftari Naibu Waziri wa Miundombinu na Mheshimiwa Dr. Milton Makongoro Mahanga, Naibu Waziri wa Miundombinu, halikadhalika Ndugu Enos Bukuku, Katibu Mkuu Wizara ya Miundombinu pamoja na Watalaalamu na Watendaji wote wa Wizara hii walioshirikiana na Kamati katika kuandaa na kutoa maelekezo ya kina pale palipohitajika.

Pia napenda kutoa shukrani za pekee kwa Mheshimiwa Johnson Mwanyika, Mwanasheria Mkuu wa Serikali pamoja na Watalaamu wake kwa kutoa ufafanuzi wa vipengele mbalimbail kwa Kamati yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inawashukuru Wadau wote niliokwisha kuwataja hapo awali kwa ushiriki wao katika *Public Hearing* na kutoa maoni yao ambayo kwa kiasi kikubwa yamesaidia katika kukamilisha na kuuboresha Muswada huu. Ushirikiano na kazi nzuri ya wadau hao umesababisha Muswada uandaliwe na kuwasilishwa kwa ufasaha na kufanya kazi ya Kamati kuwa rahisi mno. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee napenda kutoa shukrani za dhati kwa Wajumbe wa Kamati ya Miundombinu ambao walishiriki kikamilifu katika kuujadili kwa ufasaha na kuuboresha Muswada huu, naomba niwatambue kwa majina Wajumbe hao kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mohamed Hamisi Missanga, Mwenyekiti, Mheshimiwa Joyce Martin Masunga, Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Khadija Salum Ally Al-Qassmy, Mjumbe, Mheshimiwa Said Amour Arfi, Mjumbe, Mheshimiwa Paschal Constantine Degera, Mjumbe, Mheshimiwa Bakari Shamis Faki, Mjumbe, Mheshimiwa Felix Ntibenda Kijiko, Mjumbe, Mheshimiwa Paul Peter Kimiti,Mjumbe, Mheshimiwa Mkiwa Adam Kimwanga, Mjumbe Mheshimiwa Rosemary Kasimbi Kirigini, Mjumbe.

Wengine ni Mheshimiwa Suleiman Omar Kumchaya, Mjumbe, Mheshimiwa Ephraim Nehemia Madeje, Mjumbe, Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, Mjumbe, Mheshimiwa Mhe. Masolwa Cosmas Masolwa, Mjumbe, Mheshimiwa Balozi Getrude Ibengwe Mongella, Mjumbe, Mheshimiwa Dr. James Alex Msekela, Mjumbe, Mheshimiwa James Philipo Musalika, Mjumbe, Mheshimiwa Sigifrid Seleman Ng'itu, Mjumbe, Mheshimiwa Richard Said Nyaulawa, Mjumbe, Mheshimiwa Mwaka Abdulrahaman Ramadhan, Mjumbe, Mheshimiwa Prof. Philemon Mikol Sarungi,

Mjumbe, Mheshimiwa Peter Joseph Serukamba, Mjumbe Mheshimiwa Godfrey Weston Zambi, Mjumbe, Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir, Mjumbe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimalizie kwa kutoa shukrani kwa Katibu wa Bunge, Ndugu Damian Foka pamoja na Watendaji wote wa Ofisi ya Bunge kwa kuiwezesha Kamati yangu kutekeleza majukumu yake. Vilevile napenda kumshukuru Ndugu Justina Shauri ,Katibu wa Kamati hii pamoja na Makatibu Wasaidizi, Ndugu Zaynab Issa na Ndugu Patson Sobha, kwa kuweza kuihudumia vyema Kamati na kukamilisha maandalizi ya taarifa hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaunga mkono kwa dhati kuwasilishwa kwa Muswada huu na kujadiliwa Bungeni. Kwa niaba ya Kamati ya Miundombinu, naunga mkono hoja na ninaomba kuwasilisha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Ahsante sana!

**MHE. BAKAR SHAMIS FAKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani napenda kuwasilisha maoni ya Kambi kuhusu Muswada wa Sheria ya Barabara ya mwaka 2007 (The Road Act 2007) kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Kanuni ya 43(5)( c) na 70 (2) Toleo la 2004.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa sina budi kumshukuru Mungu kwa kuniwezesha kusimama mbele ye Bunge lako tukufu na kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Muswada wa Sheria ya Barabara ya mwaka 2007. Pia nashukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Mzee wetu Phares Kashemeza Kabuye kwa kuchaguliwa na Chama chake kuwa Makamu Mwenyekiti, ama kweli nafasi hiyo imepata mwenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mambo mengine yaliyoainishwa na Muswada huu, madhumuni makuu ya Muswada huu ni kuweka miongozi, taratibu na usimamizi wa uendeshaji wa ukarabati wa barabara kulingana na madaraja ya barabara hizo kwa maendeleo ya kiuchumi kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika para ya pili ya madhumuni ya uanzishwaji wa Sheria hii inasomeka kuwa,"Pamoja na marekebisho hayo sheria hii bado haikidhi mabadiliko ya kisera, kijamii, kiuchumi na kiteknolojia yanayoendelea kutokea nchini na duniani kote."

Kambi ya Upinzani inamtaka Mheshimiwa Waziri atoe ufafanuzi ni kwa namna gani marekebisho ya Sheria hii yatakidhi haja ya suala zima la kusimamia na uendeshaji wa barabara nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Pili ya Muswada huu inahusu matunzo ya barabara, kifungu cha 6(2), kinaeleza kazi za Mamlaka ya Barabara kulingana na kazi zilizoainishwa bado upo uzembe unaosababishwa na watendaji pale inapotokea kuwa Mkandarasi wa Mabomba ya Majitaka ama Majisafi amebomoa barabara ambayo ilikwishakuwa katika hali nzuri lakini baada ya kazi ya kubadilisha Miundombinu ya

Majitaka au Safi, haitengenezi ikarudi katika hali yake ya mwanzo. Kambi ya Upinzani inadhani hapa kama siyo uzembe basi kuna mchezo mchafu unafanywa kati ya Watumishi na Wakandarasi unaosababisha Serikali kupata hasara ya matengenezo ya barabara ya mara kwa mara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 7 kinazungumzia kuhusu Uundwaji wa Bodi za Barabara za Mikoa yaani *Regional Road Board*. Bodi hizi za Mikoa zimetoa nafasi chache za wadau wa Barabara katika Mikoa Kambi ya Upinzani inaona kuwa ni vema kuongeza idadi ya Wawakilishi wa Wadau wa Barabara kwa mfano hakuna Mwakilishi kutoka katika Kikosi cha Usalama Barabarani. Kwa hali ya kawaida huyu japokuwa ni kutoka Serikalini lakini vilevile ni mdau muhimu sana katika matumizi ya barabara. Aidha, kuna Idara ya Ujenzi wanaojihusisha na *Road Furniturers* kama ilivyoelezwa katika tafsiri ya maneno katika Muswada huu na ni wadau muhimu sana katika matumizi endelevu ya barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, uwezo wa *TANROADS* haujafikia hatua inayoridhisha, kwa hiyo, Serikali ijizatiti kufanya *TANROADS* kiwe chombo ambacho kitakidhi haja kama vile kuipatia wataalamu wa kutosha pia na fedha za uendeshaji. Ni vema mamlaka mpaka zile za vijijini zipewe dhamana kamili za kusimamia na matengenezo ya barabara lakini lazima ijulikane wazi suala la uwezo wa mamlaka hizo kifedha na kiutaalamu. Pia mamlaka hizi zipewe uhuru wa utendaji bila kuathiri usimamizi wa karibu wa Wizara (*Ministry Oversight)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 16 cha Muswada huu kinahusu utoaji wa fidia kwa wale wamiliki wa ardhi iliyoendelezwa au kumilikiwa kimila bila kuendelezwa walipwe fidia. Hapa Muswada unapendekeza fidia ilipe kwa kutumia sheria mbili tofauti, pamoja na ambazo zipo yaani the *Written Laws*.

Kambi ya Upinzani inaona hii itakuwa si kwa kuwatendea haki waathirika wa sheria hii kwani jambo la msingi katika kutoa fidia ni kuangalia bei ya soko kwa wakati uliopo pamoja na kuangalia eneo. Kitu kinachosababisha bei ya ardhi kupanda au kushuka ni eneo husika ilipo ardhi hiyo yaani *Land Allocation.* Sheria itakayotokana na Muswada huu ni vema iangalie na Sheria nyingine kama zile Sheria za Mipango Miji ili kuzuia maingiliano na utatanishi katika utekelezaji wake hasa katika suala la fidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, ardhi ni rasilimali, hivyo kwa yeyote mwenye kumiliki ama ikiwa imeendelezwa au hapana. Ni vema apewe fidia yake kwani hiyo ndiyo hazina yake, suala la kulipwa kidogo ama kingi litokane na vigezo kama ambavyo nimevitaja hapo juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, umefika wakati sasa tuangalie sana ubora wa barabara zetu ili tuepukane na matengenezo ya mara kwa mara, suala ambalo linaigharimu Serikali yetu fedha nyingi sana. Inasikitisha kuona barabara iliyojengwa kwa lami lakini katika matengenezo mashimo yake yamefukiwa kwa changarawe yaani kifusi au udongo baadala ya kutengenezwa kwa lami, hapa ubora upo wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara za mijini, manispaa na *City* tangu urudishwe kwa Mamlaka za Miji hali zake zimeendelea kuwa mbaya na kasi ya matengenezo yake ni ndogo sana. Kwa maoni yetu, mamlaka hizo zimeshindwa kusimamia na kutengeneza barabara, tunapendekeza barabara hizo zijumuishwe katika barabara za Mkoa.

Pamoja na kwamba Muswada huu katika vifungu vya 4(e) na 6 (2) (e) na 60(2) (t) vimeeleza kushirikishwa kwa sekta binafsi katika suala la ujenzi wa barabara nchini, vifungu hivi havitoi Mamlaka kwa sekta binafsi kuwa sehemu ya mpango mzima wa kushughulikia barabara zetu zaidi ya kufuata maagizo ya Serikali tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo basi, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali iingize kipengele katika Muswada huu ambacho kitaipa *TANROADS* Mamlaka ya kuingia Ubia na makampuni binafsi ya ndani na nje ya nchi yaani *Public Private Partnership (PPP)* katika kujenga na kuhudumia mtandao wa barabara zetu nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nirudie sehemu hii: "Kwa hiyo basi, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali iingize kipengele katika Muswada huu ambacho kitaipa *TANROADS* Mamlaka ya kuingia Ubia na makampuni binafsi ya ndani na nje ya nchi yaani *Public Private partinership (PPP)* katika kujenga na kuhudumia mtandao wa barabara zetu nchini."

Mheshimiwa Naibu Spika, tunamwomba Mheshimiwa Waziri atupatie maelezo mahususi juu ya vigezo alivyotumia katika kuweka madaraja ya barabara, kwa mfano, barabara ya Bunge *CBE* ipo daraja la sita, wakati barabara ya Msalato Lugala ipo daraja la tatu na barabara zote hizo zipo katika Wilaya moja. Uzito wa magari yanayoruhusiwa kutumia barabara zetu kwa ubora wa kiwango cha sasa uwekwe bayana, itamkwe wazi katika Muswada huu kwamba magari yanayozidi uzito unaoruhusiwa hayapaswi kuingizwa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 31 (3), kinaeleza kwamba mtumiaji wa barabara asiyetii ujumbe uliopo kwenye alama za barabara atakuwa amefanya kosa. Ili kuwasaidia watumiaji wa barabara wasifanye makosa Kambi ya Upinzani inapendekeza kwamba alama ziwekwe mwanzoni mwa barabara hasa kuhusiana na uzito ambao barabara husika inaweza kubeba na siyo alama kuwekwa tu karibu na madaraja ya barabara hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho lakini si kwa umuhimu napenda kuwapongeza wadau wote ambao walishiriki katika kutoa maoni yao ambayo kwa namna moja au nyingine yameboresha Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naomba kuwasilisha, ahsante sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Naomba nishukuru sana kwa mawasilisho hayo.

Waheshimiwa Wabunge mpaka sasa hivi walioomba kuchangia wapo zaidi ya 25 yaani wapo 32 maana 25 ndiyo hii ninayo lakini bado tunaongeza hapa. Kwa hiyo, kwa vyovyote vile, hatuwezi kuzidi leo tu k hivyo tunachokifanya hapa wale waliochangia sehemu nyingine huko hawapati *priority* watapata kama itakuwepo nafasi lakini *priority* hawapati. Kwa hiyo, kuanzia hapo watakaoweza kuchangia asubuhi mpaka saa 7 ni wanne. Hivyo, namwita Mheshimiwa Paschal Constantine Degera, Mheshimiwa Mgana I. Msindai, Mheshimiwa Eustace Osler Katagira na Mheshimiwa Janet Bina Kahama.

**MHE. PASCHAL C. DEGERA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kwanza asubuhi hii na mimi niweze kuchangia Muswada huu ulio mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijachangia Muswada wenyewe naomba nifanye mambo mawili, kwanza niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kutoa salamu za rambirambi kwa familia, ndugu, jamaa na marafiki wa Marehemu Dr. Aaron Chiduo ambaye amekuwa Mbunge katika Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa muda mrefu sana. Naomba Mwenyezi Mungu aiweke roho yake mahali pema peponi. *Amin!*

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, niungane na Waheshimiwa Wabunge waliotangulia kumpongeza sana Mheshimiwa Mtutura Abdallah Mtutura aliyechaguliwa kwa kura nyingi sana kuwa Mbunge wa Jimbo la Tunduru. Ahadi yangu ni kwamba, nitampa ushirikiano wa kutosha..

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maneno hayo ya utangulizi, Naomba nichangie maeneo machache. Kwanza, nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu kwa kuzingatia sana ushauri na maoni ya Kamati tulipokuwa kwenye Kamati na mimi ni mjumbe wa Kamati ya Miundimbinu kama ilivyoelezwa katika taarifa yetu.

Kwa hiyo, napenda nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri pamoja na wataalamu wake kwa kufanya marekebisho na kuleta marekebisho makubwa sana ambayo yameweza kuboresha Muswada wenyewe. Kwa hiyo, sitakuwa na maneno mengi ya kuchangia kwa sababu marekebisho makubwa yaliyofanyika yameboresha sana Muswada uliopo mbele yetu. Aidha, napenda nitangulie kwa kusema kwamba naungana na maoni yaliyotolewa na Kamati kwa kuwa mimi ni mjumbe. Lakini nitaongeza mchango mdogo wa kwangu binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze sasa kuchangia Muswada wenyewe na nitaanza na kifungu cha 12. Kifungu cha 12 kinahusu mambo mawili. Kwanza, utaratibu wa kupandisha barabara zetu madaraja katika nchi nzima na pili, kuweka upana wa barabara katika barabara zitakazopangwa katika madaraja.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi langu ni kwamba kutokana na maelezo ya Mheshimiwa Waziri, amesema hivi: “Hivi sasa maombi ya Wilaya na Mikoa ambayo

yametumwa ili barabara ziweze kupandishwa madaraja hasa zile zinazotoka ngazi ya barabara za Wilaya na Mkoa kwenda ngazi ya juu zaidi bado hayajafanyiwa kazi."

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi langu ni kwamba, pindi Muswada huu utakapopita kuwa sheria, basi maombi yale yazingatiwe mapema ili barabara ziweze kupewa madaraja yanayostahili na upana nao utangazwe mapema.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivyo kwa sababu kupandisha barabara daraja, kila mtu atakuwa anafahamu nini ashughulikie. Kama barabara itakuwa bado katika daraja la ngazi ya Wilaya, basi mhusika atajulikana, kama barabara itapandishwa kuwa ya Mkoa, basi mhusika pia atafahamu na kama barabara itapandishwa kuwa barabara ya Taifa, basi mhusika pia atafahamu mapema. Kwa hiyo, naomba hayo madaraja yaweze kuwekwa mapema ili kila mmoja aweze kufahamu barabara iko katika daraja gani na aweze kuishughulikia kama inavyopaswa.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ni kuhusu kutangaza upana wa barabara. Muswada huu unampa mamlaka Waziri kwa kushirikiana aidha na Waziri wa TAMISEMI kuweza kuweka upana wa barabara katika ngazi zile za Wilaya, lakini barabara nyingine ngazi za Mkoa na Kitaifa zitawekwa na Waziri mhusika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba katika kutangaza huo upana wa barabara, basi utangazwe mapema. Kwa sababu kumekuwa na usumbufu mkubwa sana kule ambako barabara zinapita, wananchi hawafahamu upana wa barabara na matokeo yake wanajenga katika maeneo ya barabara na mwisho wa siku ni kuja kubomolewa majengo yao. Kwa hiyo, ili kuepuka hili suala la bomoa bomoa, naomba basi upana wa barabara uweze kutangazwa mapema.

Mheshimiwa Naibu Spika, niende eneo la pili ambalo ningependa kuchangia, nalo linahusu akiba ya barabara. Muswada wenyewe umezungumzia tu matumizi ya akiba ya barabara, lakini Muswada huu haukuzungumzii juu ya upana wa barabara kwa kila barabara. Matumaini yangu ni kwamba, hilo litakuja kujitokeza katika kanuni zitakazotungwa na Mheshimiwa Waziri.

Sasa ninachoomba ni kwamba, basi ukubwa au upana wa barabara pindi sheria hii itakapopita uweze kutangazwa mapema na pili, elimu itolewe kwa wananchi kuepuka jambo lile ambalo nimelisema katika upana wa barabara kuepuka bomoa bomoa ambayo inaendelea hivi sasa katika nchi nzima. Wananchi wanapata hasara kubwa, rasilimali nyingi zinaharibiwa kwa sababu tu wananchi hawajui upana wa kila barabara inapopita katika maeneo na upana wake ni kiasi gani. Matokeo yake wananchi wanajenga katika hiyo akiba ya barabara na pindi Serikali ama Wizara inapohitaji kutumia akiba hiyo ya barabara inawajibika kubomoa na kuwapa hasara wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa nchi nzima utakuta majengo mengi sana yamepigwa alama ya 'X'. Hiyo ndiyo ishara ya kuonyesha kwamba hatukuwa makini kutoa elimu kwa wananchi wetu na matokeo ndiyo haya kwamba wananchi wanaingia

hasara ya kubomolewa nyumba zao baada ya Serikali kuamua kutumia akiba ya barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, niende eneo lingine kifungu cha 30. Kifungu cha 30 cha Muswada huu kinazungumzia juu ya utunzaji wa mazingira wakati wa kutengeneza barabara. Hapa ningependa tu niseme kwamba, kwa kweli hatukuwa makini kuangalia suala ama kuzingatia suala hili. Naweza kutoa mifano mingi, lakini sina sababu ya kupoteza muda wa Bunge lako Tukufu.

Napenda niseme tu kwamba Wakandarasi wengi hatusimamii vizuri hasa wanapochimba vifusi na kokoto na labda mawe. Kwanza, wengi wao wanachimba katika eneo la akiba ya barabara, yaani *road reserve* ambayo ni uharibifu mkubwa sana wa mazingira na kuhatarisha hata maisha ama ubora wa barabara zenyewe hasa kule Mikoani na Wilayani, hawachimbi vifusi katika maeneo ya mbali, wanachimba vifusi katika eneo la akiba ya barabara na matokeo yake ni kwamba wanaharibu mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata wale ambao wanachimba vifusi nje ya akiba ya barabara bado wanatengeneza mashimo makubwa sana kutokana na uchimbaji wa vifusi na hawarekebishi ile sehemu yenyewe na matokeo yake uharibifu wa mazingira unakuwa kubwa sana. Tunaomba basi wakati tunapotoa kazi za kutengeneza barabara, suala la utunzaji mazingira nalo lizingatiwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, niende kifungu cha 32. Kifungu hiki kinapendekeza juu ya kasi ya mwendo wa magari ama vyombo vya usafiri na kifungu hiki kinapendekeza kwamba katika sheria hii, alama au viwango vya kasi ya mwendo utakwenda katika barabara zote ikizingatiwa madaraja na ubora wa barabara.

Napenda niipongeze Serikali ama Wizara kwa kuja na kipengele hiki. Wote tunafahamu kwamba tatizo kubwa la ajali katika nchi yetu linasababishwa na mwenendo wa kasi wa magari yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwa kuwa kipengele hiki kimewekwa katika sheria hii ya barabara, tunaomba basi kipengele hiki kisimamiwe vizuri ili ajali ziweze kupungua na maisha ya wananchi yaweze kuokolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, niende kwenye eneo lingine ambalo ningependa kulichangia nalo linahusu kifungu cha 44. Napenda niseme tu kwamba Kamati ya Miundombinu iliyopitia muswada huu, imetoa mapendekezo yake mazuri sana. Sasa mimi sina sababu ya kupoteza muda tena kuyaeleza kwa undani zaidi. Napenda niseme hivi kwamba vyanzo ambavyo vimetajwa katika kifungu hicho cha 44 ni vichache mno na ni vidogo mno kutokana ama kulingana na mahitaji ya fedha kwa ajili ya matengenezo ya barabara katika nchi nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tumeambiwa kwamba sana sana ukipata fedha utapata bilioni 78 tu peke yake, lakini mahitaji ya matengenezo ya barabara katika nchi yetu ni shilingi bilioni 221 kwa mwaka na tumeambiwa kwamba kiwango hiki cha bilioni 78 ni asilimia 35 tu ya mahitaji ya matengenezo ya barabara. Kwa hiyo, kiwango

hicho ni kidogo mno. Kwa hiyo, tunaomba Serikali itafute vyanzo vingine vya mapato ili kutunisha mfuko wa barabara na vile vyanzo ambavyo vimependekezwa na Kamati viangaliwe ili mfuko wa barabara uweze kutunishwa na tuweze kutengeneza barabara zetu kwa kiwango cha juu zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuchangia hayo, napenda nirudie tena kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kwanza leo na ninaomba nitamke kwamba ninaunga mkono Muswada huu. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi nichangie Muswada huu wa barabara. Kwanza, niipongeze Serikali kwa kuona umuhimu wa kubadilisha Muswada huu uliotengenezwa mwaka 1932 na kuleta Muswada mpya unaokwenda na wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, kwa niaba ya wananchi wa Mkoa wa Singida na Mkoa wa Tabora, ningependa kuipongeza sana Serikali kwa kazi nzuri iliyofanya wakati wa masika. Barabara hizo zilikuwa zimeziba kabisa, kuanzia Manyoni ilikuwa chemchem tupu, Singida na Iramba palikuwa hapapitiki. Lakini kwa kweli tunaishukuru Serikali iliona umuhimu huo ikatoa fedha ili kurahisisha usafiri kwa magari mengi yaliyokuwa yamekwama.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninampongeza sana Mheshimiwa Waziri na wataalam wake kwa jinsi walivyozichanganua barabara zetu, wameziainisha karibu barabara zote za Kitaifa, barabara za Mikoa, barabara za Wilaya na mimi ningewaomba tu waendelee kupokea. Kuna barabara nyingi hazikuunganishwa humu. T unaomba tuletewe ile orodha kwa sababu hii orodha ndiyo itakuwa changamoto ya kupandisha, kutengeneza na kufanya kazi zote zinazohusu barabara zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimwombe tu Mheshimiwa Waziri, sasa hivi ni kiangazi na barabara ambazo bado hazijakamilisha bado zimekwama ni ile iendayo Kusini na barabara ya Dodoma Manyoni, Manyoni-Singida na Singida –Shelui. Naomba kwa mwaka unaokuja wa fedha Serikali isiwe na kisingizio, imalize tatizo hilo. Kwa kweli wananchi wameteseka sana katika masika ya hivi karibuni. Kwa hiyo, tunawaomba hao Wakandarasi wahimizwe ili hizo barabara zimalizwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye Muswada huu zimeainishwa barabara zote, lakini mimi ningeomba nijikite na barabara zinazounganisha Mikoa na Mikoa. Mwaka huu tumepata taabu sana kwa sababu barabara inayounganisha Dar es Salaam na Mikoa ya Bara ni moja tu, hakuna barabara nyingine ambayo ingekuwa *alternative* wakati wa shida watu wapite huko. Lakini kuna maeneo ambayo Serikali ikiyafanyia kazi nzuri ndogo tu hatutapata matatizo makubwa kama tunavyoyapata sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikichukua barabara Na.R226 ya Kidarafa - Ikungi hii ni barabara ya Mkoa na inaunganisha Mkoa wa Singida na Mkoa Manyara na Arusha. Kilomita zilizopo hapo ni 20, lakini barabara ile wakati wote wa mwaka mzima huwa ni mbovu. Kwa hiyo, ningeiomba Serikali barabara hiyo itengenezwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara nyingine R224 Uremo -Ngumaga, Ngumaga Mkarama - Mkarama Sibiti hii ni barabara inayounganisha Mikoa ya Singida - Dodoma - Dar es Salaam na Mikoa ya Shinyanga - Mwanza na Mara. Ukiichukua barabara hii kuanzia Singida mpaka Mto Sibiti, hii barabara ni ya Mkoa. Lakini haitengenezwi kwa kiwango kinachotakiwa. Ukivuka ukaingia Shinyanga, hii barabara siyo ya Mkoa ni ya Halmashauri na kikwazo kikubwa kilichopo kwenye barabara hii ni daraja la Mto Sibiti.

Lakini nashukuru Mheshimiwa Waziri ameniandikia barua na kuwapa nakala Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwamba mwaka huu wa fedha hilo daraja litawekwa kwenye bajeti. Sisi tunachoomba kwa kuanzia litengenezwe hilo daraja na kilomita kama 20 zinazojaa maji. Kwa kweli wakitengeneza hiyo barabara watakuwa wamefanya ukombozi mkubwa sana kwa Mikoa yote ya hapa nchini. Kwa sababu barabara hiyo inaunganisha Mikoa ya Kanda ya Ziwa na Mikoa ya Arusha, Dodoma na Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ninawaomba sana hilo litiliwe maanani na kwa kweli ningeomba kwa niaba ya wananchi wa Mkoa wa Shinyanga, barabara ya kutoka Bukundi kwenda Mwanuzi ambapo barabara ya Mkoa inaishia hapo ipandishwe daraja mapema iwe barabara ya Mkoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niongelee kidogo juu usalama wa barabara. Tunayo matatizo makubwa sana juu ya utunzaji wa barabara zetu. Barabara za Iramba Mashariki na Iramba Magharibi zilipata ufadhili zikatengenezwa kwa kiwango cha changarawe na barabara ni imara sana. Tatizo tulilonalo ni madaraja. Madaraja yaliyopo kwenye barabara hizi yanaruhusu magari mpaka tani 10 na kwa kweli ujenzi wa madaraja hayo hakupewa *contractor* aliyejenga hizo barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, yalijengwa yalikuwa mabovu na wakati wa mvua yote yalikatika. Lakini ninaishukuru Serikali kwa sababu ilitoa fedha madaraja yaliyoko kwangu kama daraja la Kinyagiri litengenezwe upya.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tunaomba sana kuwe na ushirikiano wa karibu kati ya Wizara ya Miundombinu na Wizara ya Usalama wa Raia. Mheshimiwa Mohamed Missanga ni Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu, barabara ya kupita kwake ilitengenezwa kuanzia Singida kwenda mpaka Kizanga. Lakini kwa sababu magari makubwa yalikuwa yanapita kule bila kuzuiliwa, ile barabara sasa hivi haitamaniki na barabara ya kutoka Singida kuja Dodoma kupitia Kwamtoro, hizi ni barabara ambazo zinasaidia sana kwa usafiri.

Lakini barabara inayoruhusiwa kutumia magari ya tani 10 yanapita magari ya tani 40 na kuendelea, kwa kweli barabara inaharibika na katika hili kunakuwa hakuna ushirikiano wa Wizara ya Miundombinu na Wizara ya Usalama wa Raia. Kwa sababu ni rahisi sana kwa watu wa Wizara ya Usalama wa Raia kuweza kusaidia. Lakini wanashindwa kuzuia hayo magari! Kwa hiyo, ninawaomba sana washirikiane ili watunze barabara zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna daraja la Mto Ndurumo linaloingia kwangu nalo limekatika. Yapo madaraja mawili katika Tarafa ya Kinyagiri na Tarafa ya Nduguti. Haya madaraja yako katika barabara za Mkoa na kwa sababu hakuna usimamizi wa barabara hizi, magari makubwa yamepita huko, madaraja yamekatika. Kwa hiyo, nawaomba waiweke kwenye mipango ya kutengeneza madaraja hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, wenzangu wameshalizungumza, lakini nami niliwekee umuhimu suala la alama za barabarani. Sasa hivi alama za barabarani karibu zote zinang'olewa. Mimi pamoja na elimu watakayoitoa kwa raia wetu, ningependekeza Wizara ya Miundombinu ishirikishe vijiji ambapo alama hizo zipo. Tukishirikisha Serikali za vijiji kwa kweli hizo alama zitadumu. Ni kutokana na kukosekana kwa alama hizo ndiyo maana magari yanaanguka na kutia hasara Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile upande wa utunzaji wa mazingira ameshazungumza mwenzangu. Inatisha sana tunapoona kila mahali hao wakandarasi wamechimba vifusi, lakini hawafukii mashimo na wanachimba pembeni mwa barabara hasa wale wa Wilayani na mvua ikinyesha yale mashimo walipotoa vifusi yanajaa maji na kubomoa barabara hiyo waliyotengeneza. Kwa hiyo, naomba sana hili lizingatiwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, mimi ningeikumbusha Serikali sasa hivi wanajenga barabara ya kutoka Singida kwenda Shelui, ile barabara zamani ilikuwa inapita kwenye Mji mdogo wa Iguguno. Lakini sasa hivi ile barabara inapita pembeni mwa Mji mdogo wa Iguguno. Lakini Serikali iliahidi kwamba ile barabara inayoingia Iguguno na kwenda kuunganisha upande wa pili, Serikali ingeitengeneza kwa kiwango cha lami nyepesi ili wananchi wa mji huo mdogo wasiendelee kupata taabu. Kwa hiyo, nawakumbusha wasije wakasahau ahadi waliyoitoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hayo machache, naomba niishie hapo, nipishe na wenzangu. Naunga mkono Muswada huu mia kwa mia. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. EUSTACE O. KATAGIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kuniruhusu na mimi nichangie katika Muswada huu. Awali ya yote, napenda nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa kuwasilisha Muswada huu vizuri kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitajielekeza katika barabara za Wilaya ya Karagwe. Wilayani na Mkoani wameshaleta maombi tayari, nafahamu wameomba barabara kadhaa zipandishwe daraja kutoka katika kuhudumiwa na Halmashauri ziweze kuhudumiwa kama barabara za Mkoa au barabara za Taifa. Lakini pia na mimi katika kuchangia *speech* ya bajeti katika kikao cha bajeti kilichopita, niliongelea masuala hayo ya kuomba barabara kadhaa zipandishwe daraja, badala ya kuhudumiwa na Halmashauri zihudumiwe na ziwe barabara za Kimkoa. Ni muhimu kwa sababu ya suala hilo na uzito wake ili wananchi waweze kufarijika na hizo barabara zipandishwe daraja.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara mojawapo ni barabara ya kutoka Omugakorongo kupitia Kigarama kwenda Murongo na kuunganisha nchi yetu na nchi ya Uganda. Katika kitabu kipya kilichogawiwa, iko ukurasa wa 64 na inaonekana na

inaoneshwa kwamba ina urefu wa kilomia 105, ingawa vyanzo vingine vinasema barabara hii ina urefu wa kilomita 124.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii inaunganisha nchi yetu ya Tanzania pamoja na nchi ya Uganda, na ninaona hicho ni kigezo tosha na ninapendekeza iweze kupandishwa daraja badala ya kuhudumiwa na Halmashauri iwe barabara ya Kimkoa. Lakini pia barabara hiyo inaunganisha nchi ya Uganda pamoja *Trunk Road* nyingine ambayo inatoka Kyaka kupitia Bugene kufika sehemu inaitwa Kasuro. Kwa hiyo, umuhimu wa barabara hiyo unaonekana.

Lakini pia barabara hiyo ni barabara muhimu kiulinzi. Wanajeshi waliopigana vita vya Iddi Amin watakumbuka pamoja na kutumia barabara ya kutoka Bukoba kwenda Kyaka mpaka Uganda, lakini pia wengi waliitumia barabara hiyo. Kwa hiyo, ni muhimu kwamba barabara hii tusiache ikawa barabara mbaya, tuipandishe daraja itengenezwe. Hatufahamu kesho na kesho kutwa tunaweza tukaihitaji kiulinzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia barabara hii ni muhimu kwa uchumi wa nchi yetu, kwa sababu inaunganisha Tanzania na sehemu ya Uganda na tulivyoingia katika mchakato wa Shirikisho la Afrika Mashariki tunalaumiana kwamba hatufanyi biashara na nchi jirani. Lakini mimi ninawahakikishia barabara hii ingetengenezwa ikawa nzuri na kwa kuwa barabara hii inapita katika Kata ambazo zina mazao mengi ya kilimo na kwa jinsi jiografia ya Wilaya ya Karagwe ilivyo, mazao mengi ambayo ni *perishable* nikimaanisha ndizi, maharage na matunda mengine haviwezi kwenda vikauzwa katika miji kama Mwanza au Dar es Salaam kwa sababu ya *logistics* zenyewe jinsi zilivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ni rahisi kwa wananchi hao kuweza kuuza *perishable goods* zao katika sehemu na Miji ya nchi ya Uganda, kama Mbarara kuna mahitaji mengi na Kampala. Hii imekuwa inajidhihirisha wakati Halmshauri ilipokuwa inakusanya nguvu kidogo, inarekebisha barabara hii ndefu, basi bei ya ndizi ilikuwa inapanda kwa mkulima. Pia bei ya maharage ilikuwa inapanda. Simaanishi yale maharage ambayo unaweza kuyatunza ukayaleta mpaka Dar es Salaam au Shinyanga kuyauza. Namaanisha maharage ambayo yanaliwa sana katika hoteli za watalii, maharage ambayo bado ni machanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nina uhakika barabara hii ikitengenezwa vizuri itafanya Kata za Bugomora, Mabila, Kamuli ambazo ni wakulima wakubwa katika Wilaya ya Karagwe na Mkoa wa Kagera kuweza kuzalisha ndizi, maharage na nyanya na tukaweza kuviuza katika nchi ya Uganda ambako vinahitajika na ambapo ni sehemu ya karibu na Kata hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pamoja na faida zote hizo, barabara hii ni mzigo mkubwa kwa Halmashauri. Barabara hii mara nyingi haitengenezwi yote kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, huwa Halmashauri inatengeneza sehemu ndogo inapopata uwezeshaji kidogo, basi inatengeneza kilomita 25 au 30, na kwa hiyo,

Halmashauri ikijituma kwamba itengenezwe barabara huwa inaitengeneza kwa kuacha barabara nyingine fupi fupi ambazo zingewafaidisha wananchi wa Wilaya ya Karagwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ni muhimu kwamba barabara hiyo, na ni ombi la wananchi wa Karagwe nzima, kwamba, barabara hii ingeondolewa katika kuhudumiwa na Halmashauri ichukuliwe na ifanywe barabara ya Kimkoa, ili sasa Halmashauri iweze kuwa na uwezo wa ziada wa kutengeneza barabara fupi fupi za kuwasaidia wakulima.

Nidokeze kwamba, pamoja na maombi yangu haya na wananchi wa Karagwe kwamba barabara hii ichukuliwe na ipandishwe daraja, naomba pia Wizara ione kwamba, ikipandisha barabara hii daraja, pia kwa bajeti inayokuja itenge fedha kiasi cha kuweza kuitengeneze vizuri, maana kwa sasa hivi barabara hii ipo katika hali mbaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba barabara hii itengenezwe kwa mara moja, *major rehabilitation,* na baada ya hapo wananchi waweze kuitumia vizuri. Wataweza kupitisha mazao yao na wataweza kufaidika na matengenezo hayo na baada ya hapo, basi inaweza ikawa inatengenezwa matengenezo ya kawaida madogo madogo. Lakini kwa sasa hivi naomba maombi yangu mawili, kupandisha daraja, lakini pia na kuweka sehemu ya fedha katika bajeti ijayo ili ifanyiwe *rehabilitation* na iweze kufaidisha wananchi wa Wilaya ya Karagwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna barabara nyingine iko ukurasa wa 64, ni Kigarama -Mabira- Kyerwa. Barabara hii pia ni barabara ndefu lakini zaidi ni kwamba barabara hii inapitia katika *Terrain* ambayo ni ngumu ya milima na yenye mawe makubwa. Kwa hiyo, inakuwa ni vigumu Halmashauri kuwa na makandarasi na uwezo wa kutengeneza barabara hii. Ninaomba iunganishwe na barabara hizi mbili zote zipandishwe daraja na ziweze kuhudumiwa kama barabara za kimkoa. Hapa ni muhimu kuangalia ili shida moja isizae nyingine. Wilaya ya Karagwe tuna shida ya kuwa ni wilaya ambayo ni kubwa sana na tumeshaomba Wilaya igawanywe, lakini bado maombi yetu yanafikiriwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ukiwa na Wilaya kubwa, kwanza una shida. Kuwa na Wilaya kubwa inafanya mambo na huduma nyingine zote ziwe mbali. Lakini pia huu ukubwa wa wilaya unazaa shida nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, utakubaliana nami kwamba Wilaya ndogo, barabara za kukatisha katikati ya wilaya zinakuwa kilomita tano au 12. Lakini ukishakuwa na Wilaya kubwa kutoka sehemu moja ya Wilaya kwenda sehemu nyingine ya wilaya inakuwa ni tatizo kwa sababu wilaya ni kubwa na kwa hiyo, barabara za kukatisha mle pia zinakuwa na zenyewe ni ndefu. Kwa hiyo, tunaomba kwamba, kwa kuwa tuna wilaya haijagawanywa, sasa lisituzalishie matatizo mengine ya barabara. Tunaomba barabara hiyo ichukuliwe na mkoa itengenezwe kama barabara ya Mkoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, niongelee pia barabara, iko ukurasa wa kumi wa jedwali jipya, ni barabara ya kutoka Kyaka Bugene, Kyanyamisa mpaka Kasulo mpakani

mwa Rwanda na Burundi. Wananchi wanaomba hii barabara itengenezwe katika kiwango cha lami, kwa sababu kwanza hii ilikuwa ni ahadi ya Mheshimiwa Rais alipokuja kutembelea Karagwe. Lakini pia barabara hii inaunganisha nchi ya Tanzania na nchi jirani za Burundi na Rwanda, lakini pia barabara hii ni muhimu kwa uchumi. Nawahakikishia kwamba na dalili zipo, kama barabara hii ikitengenezwa, ikiwa nzuri, Wilaya ya Karagwe ina uwezo wa kuzalisha chakula kwa wingi.

Sisi tunaweza tukailisha kwa kiwango kikubwa nchi ya Rwanda na nchi ya Burundi. Lakini sasa lazima Serikali itusaidie tuweze kusafirisha vyakula hivi kupeleka mpaka katika nchi hizo tukauze na sisi na tukachumia uchumi wa Tanzania. Lakini tunahitaji barabara nzuri ya kuweza kusafirisha vyakula hivyo.

Alipopita mtu mmoja kutoka nje ya nchi alisema: "Karagwe *has the capacity of being the granary of Rwanda and Burundi",* na alikuwa hadanganyi. Kwa hiyo, naomba Serikali itengeneze barabara hiyo kwa kiwango cha lami, pamoja na ahadi ya Mheshimiwa Rais, lakini pia ili tuweze kusafirisha mazaoya kilimo na mifugo. Sisi tuna bahati ya kuwa na ardhi kubwa ya kuweza kufuga na wenzetu jirani ambao tunapakana nao wanahitaji maziwa, nyama, wanahitaji ng'ombe na uwezo wa kuzalisha hivyo vitu tunao, lakini tunaomba Serikali ituwezeshe, itupatie nguvu, ili tuweze kusafirisha mazao hayo pindi tutakapoyazalisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kukushukuru tena kwa kunipatia nafasi niweze kuchangia katika Muswada huu na niseme kwa matumaini makubwa katika Wizara ya Miundombinu kwamba naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. JANETH B. KAHAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kuchangia asubuhi hii. Naomba kwanza nitoe pongezi sana kwa Wabunge wenzetu wawili, Mheshimiwa Florence Kyendesya, ambaye ni Mbunge wa Viti Maalum na Mheshimiwa Mtutura Abdallah ambaye ameshinda hivi karibuni akitokea Jimbo la Tunduru.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya wanawake wa Mkoa Dar es Salaam ambao ndiyo Jimbo langu, naomba nitoe rambirambi zangu kufuatia kifo cha Mheshimiwa Dr. Aaron Chiduo ambaye tulikuwa naye hapa Bungeni, familia yake Mwenyezi Mungu awajalie subira na aipokee roho yake Peponi. Amina.

Mheshimiwa naomba kwanza kabisa nimpongeze Mheshimiwa Andrew Chenge kwa kazi nzuri aliyoifanya na kuwasilisha muswada huu leo na ninahakika muswada huu umengojelewa na wengi na ndiyo maana kukawa na *list* ya watu wengi wa kuchangia. Nina hakika muswada huu utatuletea maendeleo kama utafuatiliwa na hasa katika eneo la vijijini ambapo watu wana matatizo ya kupata barabara nzuri ili waweze kupeleka mazao yao katika masoko mbalimbali.

Muswada huu pia kama utapitishwa na Bunge hili, basi mimi ninaomba kama wazo kwamba Wizara hii itayarishe vijitabu vidogo vidogo ili viweze kuonesha kila barabara katika kila Mkoa vizuri kwa wananchi wenzetu wote waweze kujua barabara

zao.  Naomba sasa nianze kuchangia maeneo ambayo mimi kwa kweli sikuweza kuzungumza na Mheshimiwa Katagira aliyemaliza kuzungumza, lakini nimejikuta nilijitayarisha nizungumzie eneo hilo hilo la Karagwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue katika nafasi hiyo hiyo ya *classification* ambayo iko katika fungu la 11 na 13 na nimeona katika kiambatanisho cha *first schedule* kimezipanga barabara hizi zote katika madaraja matatu, *Trunk Roads, Regional Roads na District Roads* ambazo ni Halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaelewa katika hizi barabara hasa za Halmashauri ni kwamba katika Halmashauri hatulingani uwezo. Wengine haulingani kwa mapana ya eneo, haulingani kwa mapato na kwa maana hiyo, nafikiri kuwa Wizara itaangalia sana eneo hili ili kuweza kusawazisha maeneo mbalimbali katika Mikoa yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kuanza kuzungumzia barabara ambayo imegusiwa pia na msemaji aliyetoka, barabara ambayo iko Karagwe ya kutoka Ngakorongo - Kigarama - Mrongo hadi kuingia Uganda. Urefu wa barabara hii ni kilomita 105.8 tu katika Wilaya hii.  Naomba sana barabara hii iangaliwe kwa sababu inatakiwa iwe katika daraja la *Regional Roads* ambapo sasa hivi haijawekwa katika daraji hilo. Ndiyo ombi langu kuwa la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la pili ni lile la barabara zinazounganisha nchi za jirani.  Barabara hizo hazijaonyeshwa sana kwenye *first schedule*. Lakini mapendekezo yangu ni kwamba, barabara zote zinazounganisha nchi za Afrika Mashariki na vile vile barabara zote za *NEPAD* na zenyewe ziwekwe katika *schedule* ili kusudi wananchi, viongozi, Madiwani na Waheshimiwa Wabunge waweze kuzielewa vizuri.

Pendekezo lingine ni lile la kupandisha barabara ya Hio - Kyaka ambayo inaelekea Kasulu. Kama tunavyojua, ukitoka Kasulu unakwenda Rwanda.  Barabara hii ni muhimu sana Kasulu inaunganisha mpaka Rwanda. Lakini pia barabara hizo zinaunganisha barabara nyingine inayokwenda katika nchi zote hizi nne.  Kwa mfano Uganda kupitia Kyaka, Rwanda kupitia Kasulu na Burundi ni kupitia Ngara. Sasa zote hizo zinapita pia katika eneo la Benako ambako unaelekea Karagwe. Barabara hii kwa kweli inastahili kabisa kuwekwa katika *National Trunk Road* bila kuchelewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Mheshimiwa aliyepita alivyozungumzia, pia iwe katika kiwango cha lami nzuri sana. Nchi nne ni nchi ambazo wote tunajua zinaingia katika Jumuiya ya Afrika Mashariki hivi karibuni.  Kutakuwa na magari mengi sana na vile vile itaweka eneo hili la Kyaka likapandishwa hadhi likafikiriwa pia kwa *Special Economic Zone*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tunavyoelewa, mazoa mengi sana yanayotoka katika Mikoa ya Kagera tusisahau sukari.  Si muda mrefu tulipiga kelele kuhusu sukari, lakini pia Mkoa wa Kagera unazalisha sukari.  Lakini kuna michele sehemu zinazokuja mpaka Kahama, wakilima mpunga wote wanategemea barabara hiyo. Lakini pia tuna *ranch* Karagwe ambayo nyama, maziwa yote yanahitaji kusafirishwa. Kwa maana hiyo, tunaomba sana barabara hii ipandishwe hadhi iwe katika kiwango cha juu.

Naomba nizungumzie pia kidogo tu kuhusu *maintenance*, ambao ni utunzaji wa barabara. *PWD,* zamani wengine walikuwa wakiita Panya Wengi Duniani. Kwa kweli mimi naona ilifanya kazi nzuri sana, iliangalia sana barabara zetu, mifereji yetu na iliangalia sana madaraja yetu. Tusipokuwa na *PWD* ya zamani angalau ikabadilika ikawa ya leo, kwa kweli hatutakuwa na barabara nzuri.

*Prevention is better than cure.* Tusiwe tunatengeneza barabara tu siku zote huku zina bomoka. Juzi juzi nimepita barabara ya Bongoyo Jijini Dar es Salaam, ina mashimo hatari kabisa mpaka mwisho unaona afadhali utafute barabara nyingine ya kawaida kuliko kuingia barabara yenye lami, maana mashimo yake huumiza zaidi. Naomba nizungumzie eneo la Jiji la Dar es Salaam.

Nazungumzia sasa kitu tofauti, Jiji la Dar es Salaam halina anuani kabisa za makazi *(physical addresses)*. Kitu ambacho kinafanya kuwa watu wanashindwa kabisa kwa mfano kumetokea moto, unataka kuita gari la Zimamoto hakuna *physical address* kabisa. Mgonjwa akiita *ambulance* usiku haiwezi kuja na hata ikija itakuja ikiwa imechelewa. Hata *DHL* na zenyewe zinapata taabu sana kupitishwa kwenye majumba na mitaa katika Jiji la Dar es Salaam.

Kwa hiyo, tulikuwa tukifikiria hili nalo liangaliwe na pamoja na hili majina tumeyaona leo katika kitabu hiki, ni mengi sana. Mimi nilipoangalia majina ya Dar es Salaam nilishangaa sana. Kuna barabara nyingine zimeandikwa kwa ajili ya majina ya *JK Saloon,* jina lingine Betty au Hadija, jina la Mtaa.

Sasa unashangaa, tuna Machifu ambao wamefanya kazi kubwa nchini kwetu, wengine walipigania uhuru wakati wa ukoloni, wengine waliuawa akina Mkwawa, wengine bado wako hai ndio wanamalizikia, lakini pia tuna waasisi wetu waliokuwa viongozi wa nchi, wapo hawana majina na hawajabandikwa popote, tuna wanawake maarufu wengi sana waliopigania uhuru katika nchi hawajawekwa mahala popote!

Kwa hiyo, nafikiri pamoja na kuwa barabara zipo na tumezizungumzia, tufikirie maeneo haya, kwa sababu barabara bila kuwa na majina haya inakuwa sawa sawa na mtu ambaye hajavaa vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa nataka niongee zaidi, lakini naona nisije nikachukua muda zaidi. Naomba kidogo niangalie katika hii *amendment* iliyoletwa, naomba kunukuu *Clause ya 7 (b) "relating paragraph (c) and substituting for (8) the following paragraph. Constituent Members of Parliament and (d) not more than two Members of Parliament from sits in the respective regions."* Sasa mimi najiuliza hivi tunapoanza, sisi wote ni Wabunge, kuna kigezo gani kimetumika kuwekwa kuwa wanawake wawekwe wawe wawili? Kuna kigezo gani? *(Makofi)*

Mimi mnaanza kunitia wasiwasi kwa sababu mimi naamini uwe wa Jimbo uwe wa Viti Maalum wote ni Wabunge na tuna kazi sawa kabisa na humu wala haikusema

Wabunge wakuteuliwa, sijui kama wamo ama hawamo. Nilikuwa nataka tu kupata ufafanuzi huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hapo, nawapongezeni kwa kazi nzuri mliyoifanya. Naomba kumalizia kwa kuunga mkono hoja hii kwa *percent* mia kwa mia. *(Makofi)*

**MHE. BENSON M. MPESYA**: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwanza nikushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi nichangie katika Muswada huu wa Sheria kama ulivyoletwa na Waziri wetu wa Miundombinu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kwa kuipongeza Serikali kwa sababu katika hesabu za harakaharaka ni karibu miaka 75 sasa toka sheria hii ilipokuwa imetungwa na kuletwa leo rasmi ndani ya Bunge letu tena kwa marekebisho makubwa sana. Ninaamini Sheria hii imeletwa kwa kipindi hiki ambacho sasa ni kizazi kipya kabisa, inakidhi haja na mahitaji ya kizazi hiki tulichopo na bila shaka hizi ni juhudi za dhahiri za Serikali yetu ya awamu ya nne katika kuhakikisha kwamba inayafungua maeneo mbalimbali na kuimarisha uchumi wa wananchi wetu na hatimaye tupunguze umaskini uliokithiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kuchangia na sehemu ya pili ya *road management*. Sehemu hii ina vipengele (a) mpaka (f) kwa ajili ya majukumu ya Wizara katika suala zima. Lakini mimi sijaona ni wapi ambapo Wizara inajipa jukumu la ku-*re-design* baadhi ya barabara ambazo kwa kipindi hiki haziwezi kukidhi mahitaji yaliyokuwepo hapo mwanzo. Nilifikiri wangeongeza kipengele cha ku-*re-design* baadhi ya barabara na nina sababu kubwa ya kuzungumza hivi. Katika barabara kubwa ya kutoka Cape Town kwenda Cairo ni bahati nzuri inapita katikati ya jiji langu Mbeya. Eneo la Mafiati ni eneo ambalo *design* yake ilikuwa ni ya muda mrefu ambayo kwa sasa inapaswa kabisa katika barabara ile kufanyiwa *re-design. (Makofi)*

Nayazungumza haya kwa sababu mwaka 2006 tumepoteza zaidi ya watu 16 kwa ajali za pale. Nilikuwa naingalia hii barabara kwa sababu bahati nzuri nimebahatika kusafiri kutoka Cape Town mpaka Mbeya jinsi ilivyoshughulikiwa kwa kipande cha Zambia na kipande cha Afrika ya Kusini. Ni tofauti kabisa na sisi Tanzania hapa.

Ninaomba Wizara iangalie hii ni barabara kuu, pale mahali kwa kweli *design* iliyotangulia haikidhi matakwa ya sasa hivi ambavyo magari yameongezeka sana katika jiji la Mbeya na bahati nzuri upande wa pili kuelekea katika eneo Iyela ile ndiyo Kata inayoongoza kwa idadi kubwa ya watu katika Jiji la Mbeya. Kwa sababu Kata moja ina zaidi ya watu 30,000, na kule kuna Taasisi mbalimbali za Serikali pamoja na Shule za Sekondari. Kwa hiyo, eneo hili kuvuka kwenda ng'ambo inakuwa ni hatari kubwa sana. Kama nilivyosema, kwa takwimu za mwaka 2006 peke yake watu zaidi ya 16 wamepoteza maisha kwenye eneo hilo hilo la mzunguko wa Mafiati. Nimejaribu kuuliza Bunge lililopita na sasa hivi, ninawaomba, hebu mliingize hili suala katika ku-*re-design* upya, kuangalia ni namna gani litaokoa maisha ya watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niingie sasa sehemu ya tatu ambayo ni *Roads Classification and Declaration.* Lakini nitajikita zaidi katika fungu la 16 juu ya fidia kwa wale ambao maeneo yao yatakuwa yamechukuliwa kwa ajili ya ujenzi au upanuzi wa barabara. Ninashukuru kwamba muda mrefu watu wetu wamekuwa masikini kwa sababu baadhi yao maeneo na nyumba na vitu kadhaa vimeharibiwa kwa ajili ya kupisha ujenzi wa barabara, lakini hawakuweza kupata fidia ya aina yoyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, ingawa tunazungumza hapa kwamba tunatengeneza barabara kwa ajili ya faida ya *public*, lakini *public* inaanzia wapi? Inaanzia kwa mtu mmoja mmoja. Tusipomjali huyu mtu ambaye leo amefanya kazi karibu miaka 35, nyumba yake tumeamua kuibomoa ili kupisha barabara kiuchumi, mimi sioni faida ya moja kwa moja ya huyu anayoipata anayebomolewa nyumba kwa ajili ya barabara inayokwenda Ng'omba ambayo inakwenda kuwakomboa wale wa ng'ambo. Huyu tunamweka katika nafasi gani? *(Makofi)*

Nashukuru Sheria hii sasa angalau inatoa nafasi, ina *accommodate.* Lazima tuangalie, wakati mwingine sio lazima Sheria ziandikwe, lakini kuna sheria kubwa ambayo ni *common sense*. Huyu mtu amefanya kazi miaka 30, amejenga nyumba yake na hiyo ndiyo mali pekee aliyonayo, halafu bahati mbaya anabomolewa!

Mheshimiwa Naibu Spika, nitatoa mfano kwenye kipande kinachotoka Mbeya Mjini kwenda Makongorosi. Kwanza, niipongeze sana Serikali ya Chama cha Mapinduzi, imeanza kutekeleza ilani yake kwa vitendo. Kaka yangu Mwambalaswa aliuliza hapa asubuhi juu ya barabara ya Mbeya - Makongorosi. Kipande cha kwanza cha kilomita 36 tumeambiwa kinaanzwa kujengwa kuanzia mwezi wa saba mwaka huu. Ni juhudi nzuri sana. Lakini kinachojitokeza Sheria hii ya mwanzo tuliyokuwanayo ni ya mwaka 1932. Watu wengine waliopo katika maeneo haya wapo hapo kabla ya mwaka 1932 toka 1840, hata hile Sheria, ile mnayoiita *acquire sense*, kwamba kama huyu mtu alikuwepo pale na yeye ana haki ya msingi kama inavyokuwa na haki barabara.

Sasa ninaomba, kwa kutumia Sheria namba nne ya ardhi ambayo inasema kutakuwa na fidia ya haki na kwa wakati, wananchi wa eneo la Isanga, Iganzo na Mwansenkwa, wale wote ambao nyumba zao zitabomolewa kwa ajili ya kupitisha barabara ya kwenda Makongorosi Serikali iwe na jicho la huruma, wengine ni wazee sana, ni Babu zangu mimi hawana mahali pa kwenda, walikuwepo kabla ya Sheria hii ya barabara.

Ninaomba Serikali iwatupie jicho la huruma na iwalipe fidia ya haki na kwa wakati ili waangalie mahali pengine pa kwenda. Sina shaka na Serikali hii, sina shaka na Ilani ya Chama hiki ambacho kiko madarakani, lakini hawa watu ni watu wenu tuwatendee haki, tuwape nafasi. Tukiwapa fidia kwa wakati, ninaamini wataanza kutafuta maeneo mengine na bahati nzuri katika hili nimshukuru Meya wa Manispaa wa Jiji la Mbeya, ameahidi kuwapa viwanja bila masharti. Sasa ninaomba basi, Serikali nayo kwa upande wake iwape fidia watu hawa wa maeneo yote ya Isanga, Iganzo mpaka Mwansenkwa ili kupisha maendeleo ya barabara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nije kwenye eneo lingine ambalo ni sehemu ya nne ambalo ni *Execution of Roads Work*. Hasa kifungu cha 18 na 20. Kipengele hiki kinataka wakati wana-*survey* kwa ajili ya kupitisha barabara, wana uwezo wa kwenda kuingia kwenye eneo wakati wowote na kufanya shughuli zao labda za *survey* au kuweka alama mbalimbali kama tunavyojua. Lakini naomba tubadilike, siku hizi kuna haki za binadamu.

Mahali pengine mimi nimeshuhudia watu wameingia kwenye eneo la mtu wanafyeka migomba wanasema tuna-*survey*. Yule mtu bila kupewa *notice* za kuambiwa kwamba bwana kuna shughuli hii itafanyika ndani ya eneo lake.

Sasa mimi nilitegemea kipengele hiki mnaposema 14 *notice to the authority,* hivi *authority* vipi kama mnawaarifu watu wa jiji la Mbeya wana uhusiano gani na mali yangu niliyonayo mimi ambayo mimi ndiye *land lord?* Kwanini msinipe taarifa moja kwa moja kwamba tuna *intend* kufanya hivi ndani ya eneo lako, *please* tunakuja huko, kuliko kufika mahali mmefyeka na kwa sababu katika *survey* huwezi ukaweka vipimo vyovyote bila kufyeka, sasa huu ulikuwa ni mtazamo wa zamani wa sheria ile ya mwaka 1932 ya ukoloni ambapo Mtanzania alikuwa hana haki wala hana *say*. Kwanza akiwaona hawa *surveyors* yeye mwenyewe anaanza kukimbia na leo hii ndugu zangu *after 75 years* tunataka turudie mtazamo huo huo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hamjui kwamba migomba, miti mmetuhamasisha katika kuhifadhi mazingira, ni mali kwa watu wengine? Kwa nini unaingilia *privacy* yangu kuingia kwenye eneo langu bila kuniarifu, unasema tutaziarifu *authorities*. Mimi ndiyo *authority* katika eneo langu. Mimi nilifikiri mta-*inform authorities,* lakini pale kuwe na eneo kwamba *land lord* maana ndiyo *possession* yenyewe niliyonayo sina kitu kingine. Niliona hilo mliangalie m-*take into consideration* kwa sababu kwa kweli sio vizuri kuvamia eneo la mtu ukaanza kufyeka bila kumwarifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Naunga mkono hoja hii mia kwa mia. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Nakushukuru sana *land load. (Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge nina tangazo dogo tu kwamba Kamati ya Utendaji ya *APNAC* watakutana na wale Wabunge wa Denmark saa tisa katika Chumba Na. 133. Kwa hiyo, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa kumi na moja jioni.

*(Saa 7.03 mchana Bunge lilifungwa Mpaka Saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, wakati tunaanza kujadili Muswada huu, tulikuwa na wachangiaji 36. Pamoja na kwamba wengine walichangia, bado 31. Kwa hiyo, mimi nikawa nimetoa mwongozo kwamba waliojadili katika Miswada mingine katika Mkutano huu wa Saba, hawatapata nafasi. Baada ya kutafakari sana ikaonekana haina mantiki kwa sababu waliyojadili ilikuwa ni Miswada mingine, siyo

huu. Tunafanya hivyo zaidi wakati wa bajeti kwa sababu unaweza ukajadili mambo yale yale katika Wizara nyingine. Lakini kwa Miswada, kwa kweli hakuna mantiki na tutakuwa tunawakatisha tamaa wale ambao tunaweza kusema Wabunge ambao ni *active* kwamba, leo akisema hili, basi asiseme hili. Kwa hiyo, tunafikiri siyo sahihi.

Kwa hiyo, baada ya kujadili na viongozi, Spika pamoja na Kiongozi wa shughuli za Serikali, tunaendelea mpaka kesho. Lakini, hata hivyo bado kuna wengine wataachwa. Hakuna kitu kisichokuwa na mwisho. *(Makofi)*

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Nadhani uamuzi wako ni wa busara kwa sababu hoja hizi kwa kiingereza tunaziita ni *dry*. Kwa hiyo, wale wanaochangia hizo *dry*, wasipate adhabu. Nakushukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza sana Waziri wa Miundombinu - Mheshimiwa Andrew J. Chenge pamoja na wasaidizi wake kwa kuleta Muswada huu wa kutunga sheria ya barabara mpya ya mwaka 2007.

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria hii tumeingojea kwa muda mrefu sana na kuna matatizo mengi ambayo yalikuwa yanapelekwa kwenye Bodi za Barabara za Mikoa, lakini majibu yalikuwa ni kwamba tungojee mpaka sheria zibadilishwe. Kwa hiyo, nafarijika sana kuona kwamba sasa sheria hii imeletwa ili tuweze kuijadili na kuipitisha tuweze kutatua matatizo ambayo yamekaa hapo kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina maeneo machache tu ya kuchangia. Nitachukua muda mfupi ili watu wengine wengi wachangie. Kwanza nitazungumzia kifungu cha nane kinachohusu Bodi za barabara. Utaratibu huu ni mzuri sana. Kwa hiyo, nawapongeza Mawaziri waliotangulia kwa kuhusisha viongozi na watendaji wa Mkoa kwenye barabara hizi za Taifa na za Mikoa kwa sababu sisi tumekabidhiwa barabara za Wilaya. Hizi za Mikoa na za Taifa, *trunk roads* na kadhalika. Waziri yuko mbali sana, kwa hiyo, hawezi kuziona kwa urahisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kuna mambo ambayo tungependa Mheshimiwa Waziri ayatizame. Utaratibu huu ni mzuri sana na kwa kuwa ni mzuri na uko kwenye sheria, basi lazima uwe na kasma yake ya matumizi ambayo na Bodi yenyewe itaifahamu ili wanapopanga mipango, kwa kweli isizuiwe au isiingiliwe na mambo mengine kwa sababu barabara kwa kweli ni uhai wa mawasiliano katika maeneo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningesisitiza hasa kwamba, utaratibu wa kukagua barabara ungeingizwa. Siyo kujadili tu na kupata taarifa tu, basi ni vizuri Wajumbe wakapata nafasi ya kuona barabara kabla haijatengenezwa, wakati inatengenezwa na mwisho wa kutengenezwa. Itatusaidia sana hiyo kuhakikisha kwamba tunapata kile tunachoita *value for money* kwamab ile fedha iliyotumika pale, imetumika kihalali.

Mimi sioni kama ni busara sisi katika Bodi ya Mkoa, tuanze tena kulaumu kwamba kazi haikufanyika vizuri. Waziri hayupo pale. Kwa hiyo, tupewe hilo jukumu

na tuwe na madaraka hayo ya kusimamia kuhakikisha kwamba barabara zinatengenezwa kutegemea bajeti iliyotolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna hiki kitu kinaitwa *BoQ (Bills of Quantity)*. Hiki kitu kinatumiwa wakati mwingine kufanya hali iwe kwamba mwananchi asiulize ni kitu gani.

Mimi nadhani ifike wakati sasa Wahandisi wakishapitisha hizo *BoQ*, ni za kitaalam, zina mambo mengine ambayo kwa kweli kwa mtu ambaye ni wa kawaida, hana haja ya kuyajua. Lakini, aweze kujua kwamba katika barabara inayotengenezwa, inatakiwa kuinuliwa tuta, inataka kuwekwa changarawe, inataka kuwekwa makalvati au inataka kuwekwa daraja. Hayo mambo wananchi wanayajua sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ifike wakati na Mbunge akiulizwa na wananchi: "Hivi hapa wanajenga makalvati au wanafanya nini?" Tuwe wawazi kwenye kufanya hizi kazi za wananchi na tutapata ushirikiano mzuri sana kutoka kwa wananchi. Mambo matatau hapo. Bajeti kwa ajili ya kusimamia na kukagua na *BoQ* zielezwe kwa lugha nyepesi ili wakishapitisha kwenye *Tender Board* ambazo zimeachwa sisi tusiingie, basi tuelezwe ni nini kinafanyika kwenye barabara hiyo ili hata ukiulizwa maswali wewe Mbunge, huna haja ya kujibu. Kama daraja halijengwi, ujibu wazi wazi kwamba halitajengwa wakati huu, hakuna uwezo wa kujenga. Kama ni makalvati, basi ijulikane kwamba ni makalvati na yako mangapi, kwa sababu yanahesabika. Maeneo yenye makorongo yanajulikana.

Ningependa hili tulisisitize kwa sababu tuna uzoefu wa kutosha kwa sababu mimi ni mmojawapo ya waanzilishi wa hizi *Board*. Toka mwanzoni nimekuwepo na muda huu. Kwa hiyo, huo ni uzoefu ambao tunampa Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu kingine ambacho ninataka kukizungumzia hapa ni hiki kifungu cha 11 cha kupanga madaraja ya barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili suala ni la siku nyingi sana. *Board* za Mikoa zimekaa, zimependekeza, kwa hiyo, mapendekezo yako kwa Waziri. Mimi nadhani yangetizamwa, kama hayakidhi hivi vigezo vilivyowekwa, basi yarudishwe rasmi kwamba hayo mmeleta, lakini hayakidhi vigezo. Kama yanakidhi vigezo, basi hatua zichukuliwe ili yaweze kushughulikiwa.

Kwa mfano, katika Jimbo langu, mwaka 1998, Bodi ya Mkoa ilipendekeza na kupeleka kwa Mheshimiwa Waziri kwamba barabara inayotoka Mbelei – Baga – Mgwashi – Mayo – Bumbuli yenye kilomita 50, hiyo ingechukuliwa iwe barabara ya Mkoa kwa sababu ni barabara ya uchumi, ina mazao mengi sana kwenye eneo hilo; mahindi, viazi, nyanya na chai. Kwa hiyo, kuiachia Halmashauri peke yake, haiwezi kuihudumia barabara hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, katika vigezo hivyo, tusitazame vigezo tu. Kwa mfano, idadi ya magari katika barabara hiyo yanazidi 100 kwa siku. Je, hapo kigezo

kinasema nini kwa sababu kama yako magari 100 yanapita kwenye njia hiyo kwa siku, basi na matengenezo yake yanakuwa ni ya juu.

Kwa hiyo, tusije tukaangalia vile vigezo vya kompyuta tu, havitatupeleka mbali hasa kwenye maeneo ya milimani kule Lushoto kabisa ni maeneo ya tambarare. Kwa hiyo, mimi nadhani hayo maelezo yangechukuliwa, ni nini kilichukuliwa? Tusifanye kazi mara mbili, itatukatisha tamaa sana wajumbe kwamba kazi nzuri imefanywa, lakini inabidi irudiwe. Kama ni kurudia kwa vigezo, basi tuelekezwe vigezo hapa vinasema tufanye nini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu kingine ambacho nataka kuzungumzia ni cha 18 – 19; *Notice* ya siku 14. Hapa mnasema kwamba ukitaka kuingia kwenye eneo la mtu kwa sababu ya matumizi ya kitaifa ya kupitisha barabara au kuweka michoro, hapa wameandika maneno mengi kidogo yanasema: "Kuingia ili kufanya *trio-lines, surveys and to fix any post stone, mug or object on such land*, basi mtu huyo anapewa siku 14." Jamani siku 14 ni siku chache sana. Huyu mtu na ardhi yake unampa siku 14 ili upitishe, ufanye *survey*, kwa kweli haiji. Mimi nadhani muda ungetizamwa huu. Mpeni *notice* nzuri, huyu mtu asionekane kama ananyang'anywa, siku 30 kwamba tunataka kufanya hapa barabara inabidi tuibadilishe ipite hapa na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo ningependa kulizungumzia ni kwenye kifungu cha 29 kile cha eneo la akiba la barabara *(Road Reserve)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili kwenye maeneo ya milimani lina matatizo makubwa sana. Katika barabara inayotoka Mombo – Soni – Lushoto ya lami, kuna maeneo la akiba ni sifuri, yaani hakuna, huwezi kwenda popote. Sasa, unapozungumza kwa jumla, sheria imetoa maelezo haya kwa jumla au misingi kwa jumla. Kwa hiyo, utekelezaji lazima utumie akili. Isiende tu kwamba maadam sheria imesema hivyo, basi unakwenda hivyo hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye milima kule kwetu na nina hakika na kule kwa Mheshimiwa Anne Kilango na kwa Mheshimiwa Mwenzangu wa Marangu juu kule, kuna sehemu ni *zero reserve*, hakuna, yaani huwezi kutoka, huku ni korongo na huku ni mwamba. Sasa, ukizungumza hayo, lazima uangalie mazingira hayo, usije ukajiendea tu.

Halafu vile vile, kwenye maeneo ya milimani huko, watu wanajenga kwenye sehemu ambayo imeinuka, huku ni korongo na huku ni korongo, kwa hiyo, eneo hilo ndio la kujenga. Sasa ukitaka uwe na *reserve* ya mita 22.5 kila upande, ni kwamba unafuta watu walioko hapo kabisa. Lakini, barabara ina sheria kwamba njia inapita gari moja, basi utafute njia nyingine ya kupita, ni ya kwenda tu upande huo na nyingine ya kwenda upande mwingine. Kwa hiyo, katika kutekeleza hili lazima tuwe waangalifu, kule milimani kutaleta matatizo makubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna miji kama Soni, Bumbuli, Funta, vimejengwa kwenye sehemu ambazo huko ni korongo na huko ni korongo na ndio *shopping centre* zao. Sasa unapopima hizo mita 22 huku, 22 huku, ni kwamba hawa watu waondoke hapo. Sasa barabara inakwenda wapi? Inakwenda kuhudumia watu au inakwenda tu?

Mimi nadhani hapa tuwe waangalifu. Sheria ipite ilivyo, lakini utekelezaji utumie akili kwamba hapa mazingira, maumbile kwa maana ya *ecology* na *terrain*, haviruhusu upime pande hizi huku. Kwa hiyo, iweke utaratibu ambao utasaidia barabara ipitike vizuri, lakini vile vile usifukuze watu ambao wamekutwa hapo na barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kutumia *contactors*, nadhani Wizara isijioshe kwenye masuala ya kuweka alama za 'X'. Walipewa ma-*contractors* wa kuweka alama za 'X' kwenye nyumba, kitu cha kushangaza, kwa bahati mbaya mimi niko kwenye kijiji cha Bumbuli, nimezaliwa pale, barabara imetukuta pale. Nyumba yangu iko hapo kijijini kabisa. Sasa, katika kuweka zile 'X', nyumba za watu wengine 'X' zilikuwa ni ndogo, halafu ya kwangu ilikuwa *King Size!* Ilikuwa kubwa, tena inaudhi. Ikaudhi wananchi wakakasirika, wakaifuta usiku, wakasema waone huyo mwanaume anayekuja kuweka 'X' hii kubwa mno kwenye ukuta wa Mheshimiwa Mbunge. Sasa, utekelezaji wa namna hii ni wa matatizo. Lakini mtu huyu aliyepewa hii kazi hakusimamiwa. Mimi nadhani tuwe na utaratibu, watu wazungumze, waelezwe mnataka kufanya nini? Barabara ni yetu kuwe na *discussions*.

Kama barabara inapita mahali, watu wako tayari hata kusema nitaondoa nyumba yangu, lakini nipewe muda wa kutosha. Kwa hiyo, utekelezaji wa sheria hii utapendwa sana kama kutakuwa na watu kuzungumza. Siyo kutumia sheria tu, mtu unamwuliza kwa nini unafanya hivyo, anasema, sheria! Sheria, ndiyo, lakini sheria imetungiwa watu!

Mheshimiwa Naibu Spika, hayo ndiyo nilitaka kusema na ningeshangaa sana kama nisingepewa nafasi kwa sababu watu wa Bumbuli wamenituma kwamba hizi 'X', wanataka kujua kwamba kuna 'X' ya Mbunge halafu na 'X' ya watu wengine. Hilo jibu bado sijalipata. Nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. *(Makofi)*

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Kwa kweli nilikwishakata tamaa baada ya yale matangazo ya asubuhi. Nakushukuru sana pamoja na uongozi kwa kufikiri upya lile tangazo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri na Timu yake kwa Muswada huu ambao nafikiri ni muhimu sana kwa nchi yetu kwa maendeleo ya kiuchumi, kwa maendeleo ya kijamii na kimsingi, mimi sina tatizo na Muswada jinsi ulivyokaa. Lakini ningependa kuchangia maeneo machache kwa ajili ya kuuboresha.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la kwanza ambalo ningependa kuliongelea ni *section 19; Road Authority* ya kupata mawe, kokoto, mchanga, sijui na ghasia zote zile za vifaa vya ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilidhani kwamba kwenye kifungu cha 19(2), tunazungumzia *the Road Authority* pale mwisho: *"Minister responsible for Minerals may exempt the Road Authority from paying any levy royalty and fees for license.*"

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya uzoefu wetu wa barabara ya Makuyuni – Ngorongoro, sina hakika kama neno *"may"*, linatosheleza pale. Mimi nilidhani tunahitaji neno *"shall"* kwa sababu hizi ni barabara kubwa na nyingi ya barabara hizi ni za gharama kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu kubwa ya barabara hizi tunapata fedha za msaada, wala siyo fedha za mkopo tu. Lakini katika fedha za msaada, masharti mara nyingi ni sisi tuchangie na vifaa tunavyokuwa navyo nchini. Sasa, tatizo tulilolipata kwa mfano wakati ule, unakuta hata kama kuna kamlima, pamoja na nia njema ya kulinda mazingira yetu, lakini unakuta jamii iliyoko pale inakatalia kabisa kupata zile kokoto ama kifusi au hata kuchukua mchanga kwa ajili ya shughuli zote zile zinazoendana na ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kushauri hapa, tukubaliane kabisa kwamba neno *"may"* lisiwe ni hiari, tuweke neno *"shall"* kwa maana ya kwamba mchanga na kokoto ni rasilimali za Taifa, zitumike kwa miradi yote ya maendeleo bila tena sisi kwenda kulazimika kupiga magoti kwa watu wachache.

Mheshimiwa Naibu Spika, hilo ni ombi langu na kwa kweli tulipata tatizo kubwa sana katika ujenzi wa barabara ya Ngorongoro na nadhani wenzangu wengine pia wanafahamu matatizo ya aina hiyo. Lakini hii pia sio kwa hapa tu, hata kwa ujenzi wa shule na kwa ujenzi wa miradi yetu mbali mbali, tunapata matatizo sasa kwa sababu kila mahali wanaona hizi rasilimali ni mali yao. Kwa hiyo, ni lazima zilipiwe. Kwa hiyo, ninadhani hii ingekwenda katika sura pana. Lakini kwa maana ya hapa, basi tungeweka neno *"shall."*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilifikiri vile vile katika sehemu ya 32: Ni kweli leo tunaweka kifungu cha 32(2) kwa maana ya kuweka *speed limit* na kadhalika. Lakini, kwa wale wenzetu ambao tumetoka nje kidogo, tatizo kubwa ninaloliona ni kwamba, kwa leo tunaweza kuvumilia labda kwa sababu hatuna *resources*. Lakini kwa kila mji kila baada ya kilomita 30, mtu unasafiri kilomita elfu moja na kitu kwa siku, unawekewa kila wakati lazima urudi kwenye kilomita 50, usizidi. Nadhani kuna tatizo.

Kadri inavyowezekana, tuanze kuingiza kwenye barabara zetu *diversion* kila tunapofikia mjini. *Diversion* inasaidia wale wanaotaka kukimbia wakimbie wafike mapema kule wanakwenda kwa *speed* iliyoruhusiwa. Lakini, mtu yule ambaye anaingia kwenye mji, aingie kwenye mji kwa utaratibu unaotakiwa. Kwa hiyo, kuwe na *outlet* na kadhalika. Tuko kwenye karne ya kisasa, barabara tunazojenga leo ziwe za kisasa na kama tulivyosema tunazungumzia kujenga barabara ambazo zitadumu muda mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nataka kutoa tu kama tahadhari, tusifikirie tutaendelea hivyo kila siku kwa kuweka *bumps*, kwa kuingia na kusema kilomita 50, kilomita 25, kilomita 10 kila tunapoingia. Nadhani tuangalie na *speed limit,* inapaswa pia kwenda kwa ukubwa wa magari.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninataka nizungumzie kifungu cha 11. Nashukuru sana Mheshimiwa Waziri ameleta mapendekezo mapya katika *schedule of amendments,*

ameshirikisha katika kifungu cha 11(2) Waziri wa TAMISEMI. Barabara zetu nyingi sana zinafanya kazi kwa ushirikiano kati ya Wizara, *TANROADS* pamoja na TAMISEMI. Kwa hiyo, namshukuru kwamba ameona hiyo nia ya kushirikiana na TAMISEMI katika kupanga vile vigezo na TAMISEMI maana yake inakwenda mpaka chini zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba ushirikiano na TAMISEMI usiishie kwenye ngazi ya Taifa tu, lakini hata *Road Board* pia iweze kupokea mawazo kutoka chini. Kwa bahati mbaya sikuona kwenye ngazi ya *District* haya mawazo, kwa upande wa wilaya kama kulikuwa na *Min-Road Board* zamani. Kwa mfano, sisi wa Arusha tulikuwa na *Min-Road Board*. Nilitaka kujua kama *Min-Road Board* sasa zimekufa moja kwa moja au ziendelee kuwepo kwa sababu kwa kweli zilikuwa zinasaidia mahali fulani kuweka pamoja mawazo ya kiwilaya. Japo ni kweli Halmashauri ndiyo inafanya kazi ile, lakini nadhani tukitoka nje ya Halmashauri tukapata mawazo ya wadau kwa upana zaidi pia inasaidia. Sasa, nadhani ni la kuangalia tu kama liende sehemu ya *Road Board* ya Mkoa na kuwe na *extension* yake kwenye Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwa kutumia kifungu cha 11(2), pia nifikishe ombi langu ambalo nilikwishamwandikia Waziri kuhusu barabara ya *Oldian Junction*, kwa watu wengine wanaita Njiapanda kwenda Gandeg kwenda Matala na barabara hiyo kimsingi inakwenda mpaka Lalago – Shinyanga. Barabara hii ni barabara ambayo iko kwenye barabara ya lami ambayo inatoka Makuyuni kwenda Ngorongoro, ndiyo maana inaitwa *Oldian Junction*.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii kimsingi imekwishatolewa ahadi nyingi, Rais wa Awamu iliyopita, Rais wa sasa wakati wa kampeni na baada ya kampeni amekwishamtuma mpaka Waziri wake Mheshimiwa Chiza nadhani kule Karatu. Waziri amethibitisha na juzi Rais alikuwa kule, amethibitisha tena. Nilitegemea katika hatua ya awali kwamba ingekuwepo kweye *schedules* zilizowekwa hapa chini ya Mkoa wa Arusha na Wilaya ya Karatu. Lakini nimeona barabara zilizopo hapa ni zile zilizokuwepo kwenye utaratibu wa zamani, yaani barabara ya Karatu kwenda Kilimapunda.

Sasa, nilikuwa nafikiri kwamba kwa vile ilijibiwa mara nyingi hapa Bungeni na nadhani Mheshimiwa Naibu Waziri aliyekuwa anajibu bahati nzuri ni yule yule Mheshimiwa Dr. Milton M. Mahanga, kwamba barabara ile itapandishwa hadhi tutakapoletewa Muswada.

Leo tumeletewa Muswada nikategemea kwamba itakuwepo, lakini nimeridhika na maelezo ya Mheshimiwa Waziri kwamba vigezo hivi tutapanga baada ya sheria hii kupita na mimi naelewa kwa sababu tunahitaji *consultation* na Waziri wa TAMISEMI. Nadhani niridhike kwa sababu hiyo. Lakini, kutokana na umuhimu wa barabara hiyo, basi ninaomba kabisa barabara hiyo wakati wanafikiria hivi vigezo, basi ipate kipaumbele kwa sababu ahadi imekwishatolewa, tayari Serikali inajenga daraja kubwa katika Mto Barai, linaitwa Daraja la Barai limejengwa hata kabla barabara haijachukuliwa na *TANROADS*.

Sasa kama tumekwishaanza kazi na lile daraja kama barabara haijatengenezwa, itakuwa kazi bure, haipitiki tena. Daraja lile limegharimu Serikali zaidi ya milioni 128, lakini kwa jinsi barabara ilivyo, kwa wakati wote ile njia wakati wa mvua huwa inafungwa. Sasa mimi nilidhani ili tupate manufaa ya zile fedha Shilingi milioni 128, basi na ile barabara iwekwe kwenye hali nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii ni barabara ambayo iko kwenye *basin* ya kiuchumi. Bonde la Eyasi ni, bonde linalozalisha vitunguu vinatumika kila mahali. Ukienda Kariakoo,Tandale, Arusha, Shinyanga, Mombasa na Nairobi kote utapata vitunguu vya Eyasi. Sasa hivi taarifa niliyonayo, vinapelekwa mpaka nchi za Uarabuni. Kwa hiyo, ni eneo kubwa la kiuchumi kwa upande wa kwetu na ndiyo maana Rais alipokuwa kule wakati wa kampeni na baadaye wakati alipotembelea, aliahidi kwamba barabara hii kwa kweli itajengwa. Kwa hiyo, nadhani kuna sababu za kutosha za kiuchumi kwa barabara ile kwenda Gandeg – Dumbechani – Jiobaji – Matala, hii barabara kwa kweli inahitaji kwa hatua ya kwanza angalau iweze kupandishwa katika hadhi ya changarawe. Lakini, ninafahamu wakati huo kwamba Serikali imekwishafanya kazi ya *feasibility* na barabara hii wameishaweka *beacons*, nadhani mpaka Lalago.

Mheshimiwa Naibu Spika, *survey* iliyofanyika ya Lalago, nadhani kama sikosei ni kwa ngazi au kwa daraja la lami. Sasa, ningependa kujua tu, wakati wa ku-*windup* Waziri atufafanulie katika Bunge hili, kwa vile kazi hiyo imeshafanyika na ndani ya Bunge hili nilijibiwa kwamba: “Sasa hivi hatua tuliyonayo ni ya kutafuta wafadhili”. Lakini kwa bahati mbaya barabara hii haionekani tena kwenye *budget speech*. Ningependa kujua hatima ya barabara hii ni nini? Je, ule utaratibu wa kuwa na barabara ya *Oldian Junction* – Gandeg – Matala – Lalago, bado ipo au haipo? Kama ipo utaratibu wake sasa umefikia hatua gani na kama fedha zimepatikana, basi mfadhili ni kutoka wapi? Kama zimepatikana, basi kazi ya ujenzi inaanza lini?

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka pia kwa kifungu hicho hicho niongeze barabara ya pili ambayo pia maombi ya Mkoa yamekwishafika Wizarani, ni barabara ya Manyara ambayo inatokea kwenye barabara kuu inakwenda Kambi ya Simba – Shahamo – *Uper* Kitete – Lusitete – Selela, inaunganisha Wilaya ya Karatu na Wilaya ya Monduli.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini tunafikiri kwamba barabara hii ina umuhimu sana? Mwaka 1959, Serikali iliyokuwepo wakati ule, iliwaondoa ndugu zetu wa jamii ya Kimasai ikawaleta Wilaya ya Karatu eneo linaloitwa Lusitete. Eneo hili ni kama Kisiwa ndani ya Wilaya ya Karatu, limezungukwa na msitu, lakini ni eneo linalozalisha sana. Ngano nyingi za Karatu zinatokea pale, maharage mengi yanatokea pale. Lakini pia kuna mawasiliano na sehemu ya Selela katika Wilaya ya Monduli.

Lakini kutokana na jiografia ya eneo lile na hali ya barabara ile ilivyo, wenzetu hawa pamoja na kazi nzuri, nzito wanayoifanya ya kuzalisha, wanashindwa kupeleka mazao yao sokoni kwa sababu hali ya barabara ni mbaya na kwa sababu Halmashauri ya Wilaya haina nguvu kujenga barabara hii, tulifikiri kwamba kwa kuwa Wilaya ya Karatu itakuwa na barabara labda mbili tu za Kimkoa na hii ikiongezwa itakuwa barabara ya tatu

na kwa kuwa inakidhi masharti yaliyoelezwa ya barabara zinazounganisha Wilaya pamoja na Makao ya Mkoa, basi tulidhani barabara hii inastahili kuingizwa pale ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, sitaki nigongewe kengele, lakini nilidhani vile vile nisemee kidogo juu ya uwezo wa Serikali kuingia katika eneo ambamo inahitaji kujenga barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani tunapokuwa na mambo makubwa ya kitaifa namna hii, tusiweke urasimu mkubwa kwa sababu sisi kule kwetu tumepata tatizo kwenye eneo moja, kwa mfano Mwekezaji anakataza viongozi wa Serikali kabisa kupita kwenye eneo lake kufanya *survey* ya wananchi. Sasa, hii ni barabara inayotoka Mahoromba kuja Karatu. Unapopata watu wa namna hii, wanaweza kukwamisha maeneo ya nchi nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilidhani tunapokuja kusema kwamba kibali cha kuingia katika eneo… *(Hapa Kengele ililia kuashiria muda wa mzungumzaji kwisha)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami nikushukuru kwa kunipa nafasi hii niweze kuchangia Muswada huu muhimu sana wa barabara.

Kwanza, nami nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri na watu wake kwa kuleta Muswada huu mzuri sana. Hakika umekuja kwa wakati ingawaje umechelewa, maana ni miaka karibia 75 toka tulipokuwa na sheria ya barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukisoma Muswada huu una umuhimu wa mambo makubwa manne. Kusudio la kwanza, ni kuboresha barabara zetu katika uendelezaji kwa maana ya usimamiaji na ukarabati wa mtandao wa barabara. Hii ndiyo nia ya Muswada huu. Mimi nasema, sheria ni nzuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara kwa vyovyote vile ndiyo *backbone* ya *program* zote ku- *flourish* ili tuweze kuendelea, lazima tuwe na barabara nzuri. Mimi sijui ni nchi gani imefanya vizuri katika maendeleo bila kuwa na barabara nzuri. Hiyo mimi siifahamu. Sasa kama maana yake ndio hiyo na baadhi ya *research* wanasema *roads is a catalyst of development,* lazima tuweke kipaumbele namba moja kwenye barabara pamoja na miundombinu kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimewasikiliza Wabunge wengi sana, kila mtu anaongelea barabara yake na anajaribu kuonesha uchumi ulivyo kwenye hizo barabara, kilimo kilivyo kwenye hizo barabara, lakini watu hao hawana *access* kwenda kwenye masoko. Maana yake ni nini? Maana yake ni kwamba, barabara ndiyo itakayotufikisha kwenda kwenye masoko.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaweza tukafanya mapinduzi makubwa sana ya kilimo katika nchi hii, tukalima kila kona ya nchi yetu. Lakini kama hatutakuwa na

uwezo wa kufikisha hayo mazao kwenye masoko, bado wakulima wetu hatutawaondoa kwenye hali yao ya umaskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa naangalia *section* 44 ya Muswada huu imezungumziwa kwa kifupi sana. Wanasema *financial provisions, part* 8 ya Muswada huu. Inaongelea vyanzo vya fedha kwa ajili ya ku-*finance* barabara zetu. Mimi naomba leo niongelee hili la vyanzo vya pesa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunajua tunayo matatizo ya *resources*, lakini kwa sababu *resources* zetu ni kidogo, lazima tuamue tuzipeleke wapi ili ziweze kuzalisha kitu kingine. Naomba kama inawezekana tu-*finance* barabara zetu kwa fedha ya kutoka kwenye Bajeti ya *Road Funds*, kuna *donations, loans and grants, private funding and local government revenues.*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia bajeti yetu inayokwenda kwenye *Road Funds,* fedha inayotakiwa ili tuweze ku-*sustain* barabara tulizonazo sasa tunahitaji karibu Shilingi bilioni 221. Lakini kwa mwaka tunapeleka Shilingi bilioni 78 kwenye hizo barabara. Maana yake ni 35 ya *requirements,* ndiyo tunaweza tu. Ni kwamba, tusipokuwa waangalifu tutajenga barabara zile zile miaka yote, tutaendelea kufanya ukurabati wa barabara zile za miaka yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli kama ukarabati wa barabara hatuupi kipaumbele, hali yetu ya uchumi haiwezi kuboreka. Maana barabara ina ku-*detolarate.* Leo tukijenga barabara ya lami vizuri ya kilomita hata tano, kwa kawaida tunategemea ikae angalau kwa miaka 13 mpaka 15. Lakini ili iweze kufika miaka hiyo, lazima tuwe tunaifanyia *maintenance*. Lakini tumeshuhudia barabara zetu zinaanza shimo moja, linafuata la pili, linafuata la tatu, linafuata la nne, mpaka barabara inakufa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, siwalaumu wenzangu, ila ninachosema, tatizo lililopo ni fedha. Kwa hiyo, nataka niliombe Bunge hili tukubaliane kabisa kwamba tusipoongeza mfuko wa barabara ili kuweza kutengeneza barabara zetu tutakuja hapa ndani kila mtu ataomba barabara yake na bado haitafanikiwa na mwisho tutaanza kulaumiana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mtandao wa barabara wa nchi hii kilomita 85,000, kilomita 35,000 ndizo pekee ziko kwenye Wizara ya Miundombinu, kilomita 50,000 ziko kwenye *Local Government*. Lakini ukienda kwenye kwenye *Road Fund Board,* kiasi kinachokwenda kwenye *Local Government* ni asilimia 30. Sababu ni nzuri kwa nini wanafanya hivyo na ndiyo maana sasa kila mtu anatamani barabara yake ipandishwe ije kwenye Serikali Kuu kwa kuamini kwamba huku ndiyo kwenye fedha. Kumbe tukizipandisha zote tukazileta huku, mwisho wa siku naye hataweza. Tutaomba tena tuzirudishe. Mimi hapo ndiyo sielewi! Kwa hiyo, tatizo letu sisi siyo barabara iwe katika *Local Government* ama iwe kwenye Serikali Kuu. Tatizo letu ni fedha. *(Makofi)*

Mimi naomba sheria hii imekuja, na ili iwe na maana, lazima tufikirie namna ya kupata fedha za kufanya ukarabati wa barabara zetu. Hatuna njia ya mkato. Tumesema moja ya njia tutakwenda kuomba *development partners* wetu hawa, lakini wana maswali

magumu sana hawa. Mimi ninaamini watakwenda, watasema *fine.* Mnatuomba hela tujenge barabara mpya.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza ambalo hata mimi ningekuwa nakupa fedha ningekuuliza, ningeuliza, unajengaje barabara mpya wakati hata ulizonazo hujaweza kuzi-*manage*? Kwa hesabu za kawaida, kwa nini nikupe barabara nyingi ambazo *at the end* utashindwa kuzi-*maintain?*

Kwa hiyo, tukizubaa watakuja watasema basi mimi nakusaidia lakini ku-*maintain* zilizopo, siyo barabara mpya. Ndiyo! Lazima wenyewe tufikirie nani wa kuweka fedha zetu. Kupanga ni kuchagua, lazima tukubaliane hapa ndani kwamba tuanze na nini, tuiishie na nini. Lakini tukiamua kwamba tunataka kila sehemu tufanye, mwisho wa siku hakuna tutakachokifanya. Tutagusa kidogo kidogo, tunakwenda kwenye mchezo unagusa, kwenye muziki unagusa, kwenye barabara unagusa, kwenye kilimo unagusa, utakwenda kila sehemu mwisho wa siku *impact* haitaonekana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri Mkuu wa *Singapore* siku moja alikuwa anasema wameendelea kwa sababu ya *geographical location* yao. Sisi tunazo sababu kama hizo hizo za *geographical location,* lakini la pili, tunazo sababu pia za kihistoria, tuna amani nchi hii. *(Makofi)*

Kwa hiyo, kilichobaki sasa ni kwamba mipango yetu iwe mizuri. Leo tunapitisha sheria hii ya barabara, mimi sitaki kuamini unawezaje kuacha kupeleka barabara sehemu ambapo una hakika kesho yake utapata fedha kupeleka mambo mengine kwenye maendeleo. *(Makofi)*

Mimi sitaki kuamini, unaachaje kupeleka barabara Magharibi, unaachaje kuweka *priority* barabara ya kutoka Manyoni kwenda mpaka Kigoma? Kwani ukifika Kigoma tu kuna mzigo Kongo unakusubiri, kuna mzigo Burundi unakusubiri, kuna mzigo Rwanda unakusubiri na mizigo hii ukishaipata maana yake ni fedha tena za kigeni! Ukipata fedha za kigeni unakwenda sasa kufanya vitu vingine. Sasa tunapitisha sheria hii, lakini ukiangalia mambo haya mwisho wa siku tutalaumiana tu hapa ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata kusema nianze kuangalia hizi *schedule,* naona mwisho wa siku wala hazitusaidii sana. Nitamwambia Waziri *schedule* yangu hii hapa, barabara yangu hapa siioni na ziko ambazo sizioni, lakini hata nikiziona hana fedha huyu!

Kwa hiyo, tunapopitisha sheria hii, tuamue kwamba tunapitisha sheria ya barabara na tuwe na dhamira ya kweli ya kujenga barabara na iwe *reflected* kwenye bajeti, siyo sehemu nyingine. Ukiangalia watu wote humu ndani, kila mtu anatamani barabara nzuri. Kwa kaka yangu Mheshimiwa Kimiti, kuna vijiji ukienda kule Sumbawanga gunia la mahindi ni Sh. 2,000/= lakini gunia hilo hilo ukienda Mwanza linauzwa Sh. 20,000/=, lakini unalifikishaje kama huna barabara? *(Makofi)*

Lakini mtu huyu ukimjengea barabara, nawaambia atapata fedha, atajenga shule, atasomesha watoto wake, ataweza kujitibu kiafya. Kwa hiyo, naiomba Serikali kwamba, tunapitisha sheria hii lakini na *commitment* ya kujenga barabara iwepo.

Ni matarajio yangu kwamba *commitment* hii tutaiona kwenye bajeti ya mwaka huu. Lakini tunasema tunapitisha sheria nzuri namna hii, naamini hata Wazungu watatupenda kwa sheria hii, lakini sheria hii tutakaposhindwa kuitekeleza, itakuwa haitusaidii. *(Makofi)*

La mwisho nililotaka kusema ni suala la alama za usalama barabarani. Ukiangalia kwenye Muswada humu Na. 56 inasema: *"Road Authority* haitakuwa *liable*, mimi nakubali kabisa. Lakini basi tujaribu kuweka alama za barabarani. Tumepata ajali nyingi sana, nyingine zinasababishwa na kutokuwa na alama ya barabarani. Lakini nyingine zinasababishwa na kutofanya ukaguzi wa barabara zetu wa mara kwa mara angalau kupita tu. Lakini kuna barabara unakuta ni nzuri ya lami kabisa, linaanza shimo dogo, linakua, kama vile ma-*engineer* hawapiti hapo, Wizara haipiti hapo, matokeo yake, kesho gari inapita ulikuwa hujui kama shimo limekuwa kubwa unaingia kwenye shimo unapata ajali. *Yet Road Authority* haiko *liable*.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimalize kwa kusema, sheria tunayopitisha leo ni nzuri sana, naishukuru Serikali kwa kuleta sheria hii. Lakini naiomba Serikali, dhamira ya kupitisha sheria hii iendane na dhamira ya kuongeza fedha kujenga barabara zetu. Tusipopandisha mfuko wa *Road Fund*, tusipoongeza fedha za maendeleo, matumaini yetu ya kufika *semi industrialized* mwaka 2025 kwa kweli hayatafikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. CHACHA Z. WANGWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja hii muhimu ambayo Watanzania wote nadhani wametega masikio kusikia Wabunge wanasemaje kuhusu barabara. Kwa sababu nadhani katika Afrika hakuna nchi yenye barabara mbaya kama Tanzania. Wale wanaotembea wanafahamu, hii ni nchi ambayo huwezi kukatiza kutoka kona moja hadi kona nyingine ukitumia barabara.

Kwa wale tunaokaa pembeni, ukitaka kuja Dar es Salaam katika Makao Makuu ya nchi, ni lazima upite Kenya; kwa wale wanaokaa Kagera ukitaka kuja Dar es Salaam lazima upite Uganda na Kenya ndiyo ufike kwenye makao Makuu ya nchi; kwa wale wanaokaa Mtwara, lazima upite majini ndio uweze kufika Dar es Salaam; wale wanaokaa Kigoma, mpaka upate usafiri wa ndege au usubiri reli ambayo itachukua wiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hii ni picha ya kwamba, katika upande wa barabara lazima tukubali hata awamu ya nne ya Serikali hii nayo inashindwa.

Mheshimwia Naibu Spika, eneo ambalo wameshindwa zaidi, wameshindwa katika *planning* kwa sababu mipango ndiyo inayowezesha kitu kufanyika. Mimi sikubali ya kwamba Serikali haina fedha. Hii Serikali ina fedha za kutosha hata kabla hatujatafuta hela za wafadhili, fedha za walipa kodi zinatosha kabisa kujenga barabara katika nchi hii kwa sababu huo ndiyo mkataba uliopo baina ya wananchi na Serikali, yaani mkataba wa

kikatiba unasema wananchi wajibu wao ni kulipa kodi na wananchi wanalipa kodi sana. Hata wananchi wa Jimbo langu, Wilaya yangu, Mkoa wangu mimi nafahamu wanalipa kodi nyingi kweli kweli Serikali. Kwa hiyo, wao wanatimiza wajibu. *(Makofi)*

Wajibu wa Serikali ni kukusanya kodi na kuzitumia katika miradi ya maendeleo, huo ndio mkataba uliopo baina ya Serikali duniani. Wananchi walipe kodi, kodi itumike kuleta maendeleo. Sasa ikoje Tanzania?

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Tanzania yetu, wananchi wanalipa kodi na hiyo kodi haitumiki kuleta maendeleo, inatumika kufanya mambo mengine, kwa mfano kununua mashangingi mengi sana, inatumika vile vile kwa safari nyingi sana na kwa mambo ambayo hayahusiani na maendeleo. Halafu Serikali inapopungukiwa inarudi kuwaambia wananchi waisaidie. Kwa hiyo, wananchi wanalazimishwa kujenga shule na kadhalika.

Sasa naona hatua tunayokwenda sasa, kwa sababu wananchi wamekuwa wakilazimishwa kujenga shule ambao ni wajibu wa Serikali, sasa tunakwenda kwenye kulazimishwa kujenga barabara. Hili hatutalikubali. Hata mimi katika Jimbo langu nitawaambia wananchi wasikubali michango ya lazima kwa sababu katiba inasema wazi kabisa katika ibara kwamba hakuna kazi ya shuruti. Hakutakuwa na kazi ya kushurutishwa. Hiyo ni katiba! Subiri. *(Mkofi/Kicheko)*

Mimi Katiba naifahamu. Katiba vile vile inazungumzia kuhusu wajibu wa Serikali kwamba wajibu wa Serikali ni kutumia fedha kwa ajili ya maendeleo. Sasa kwa sababu wote mnaifahamu Katiba, hakuna Mbunge ambaye hasomi Katiba. Ukweli ni kwamba Serikali ya Tanzania haitumii fedha za wananchi. *(Kicheko)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Chacha Wangwe, kaa chini. Katika kitu kitakatifu ni Katiba. Naomba uisome kama ilivyo, kuliko kusema Katiba kumbe umejazia ya kwako. Usome kama ilivyo ama useme siyo katiba unasema tu.

**MHE. CHACHA Z. WANGWE:** Basi nitaisoma kama ilivyo. Tufungue ukurasa wa 26, naisoma Katiba pale ambapo ni *relevant* ninapotaka kuzungumzia kwa sababu hii Katiba ndiyo inayotuongoza. Katika ukurasa wa 26 ibara ya 25 (3) sikiliza sasa nikusute, inasema hivi: “Kwa madhumuni ya ibara hii na katika Katiba hii, kwa jumla ifahamike kwamba kazi yoyote haitahesabiwa kuwa ni kazi ya shuruti au kazi ya kikatili ya kutweza.” Katika ibara ya pili, inasema: “Bila kujali masharti ya Ibara ndogo ya kwanza, hakutakuwepo na kazi ya shuruti katika Jamhuri ya Muungano. Hiyo ni Katiba.” *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi vijijini wanashurutishwa kujenga shule kwa nguvu, hiyo ni kinyume cha Katiba. Sasa nasema hivi, kwa sababu nafahamu kwamba ni mipango imewashinda, nitawapa ushauri. Mkoloni alipopitisha hii sheria mwaka 1932 aliweza kujenga barabara ambazo zilikuwa zinapitika pamoja na kwamba hazikuwa na lami, ulikuwa unaweza kutoka Mwanza mpaka Mbeya, kwa sababu alikuwa anajenga kwa kutumia nguvu kazi. Anaweza kuwa na *grader* moja na *tipper* mbili lakini wananchi

wanapewa fedha, wanajenga katika maeneo yao, katika vijiji vyao barabara inapitika, kuliko kutumia wakandarasi ambao ukiangalia, ni mchezo mchafu unaochezwa baina ya wakandarasi na watendaji wanakula pesa ya wananchi na hawajengi barabara. Huo ndiyo mchezo ambao Serikali hii inaukubali kwa sababu wana maslahi fulani ndani ya hiyo kazi.

Kwa hiyo, ninachoshauri ni kwamba, hizo fedha mabilioni ambayo mnayatumia, kwa nini msiwape wananchi wafanye hiyo kazi na mikono, lakini siyo kwa kuwashrutisha kwa kuwalipa, mwone kwamba barabara zinatengamaa na kwa gharama ndogo kuliko ilivyo sasa? *(Makofi)*

Mawaziri wanazungukia sana nchi hii kuangalia barabara, hata juzi Mawaziri walikwenda kuangalia magari 500 yalikwama walishindwa kupita wanakwenda na helkopta. Sasa wanakwenda kusema Mbowe anatumia helkopta, mbona wao walitumia helkopta tena kwa kutumia fedha za wananchi kwenda kuangalia magari yaliyokwama na hakuna *solution*, hakuna jibu lolote lililotokea? Mpaka leo Tanzania haina barabara.

Kwa hiyo, kitu cha kuangalia hapa ni kwamba, ile nia ya kujenga barabara haipo na pia suala la rushwa na ufisadi limezuia Tanzania isiwe na barabara, ndiyo sisi tunaokaa pembezoni Kenya na Uganda tunaangalia jinsi barabara zinavyojengwa kwa majirani kwa kutumia kodi za wananchi, wakati hawana madini, hawana dhahabu, hawana samaki, lakini wanaweza kujenga barabara zao na zikawa nzuri. Kwa hiyo, katika huo mpango wa Shirikisho la Afrika ya Mashariki, wananchi wa Tarime wanafikiria waiombe Serikali wawe wanalipa kodi Kenya kusudi watengenezewe barabara. Kwa sababu tangu uhuru, hakuna barabara iliwahi kujengwa pale Tarime. *(Makofi/Kicheko)*

Kwa hiyo, sisi tunalipa kodi tu, migodi yetu inatoa dhahabu Serikali inapata pato, mbunga za wanyama zinatoa fedha, samaki zinaingiza pato Serikalini, hakuna barabara inayojengwa. Kwa hiyo, tunaona kwamba Serikali haina nia ya kutujengea barabara kwa kuwa tunakuja kuungana turuhusu tulipe kodi Kenya tutajengewa barabara kwa sababu inaonekana hakuna nia ya kutusaidia.

Jambo lingine ambalo ningependa kuzungumzia kuhusu barabara ni kwamba Wabunge wanakuja kulialia hapa,tunataka barabara lakini wanashindwa kuibana Serikali itueleze kwamba tangu uhuru ni kiasi gani cha kodi ambacho kimelipwa Serikalini mwaka hadi mwaka na ifikie mahali ambapo Serikali inasema haina fedha hata kodi ya mwaka huu peke yake, kama shilingi bilioni 700 zinaweza kupotea mpaka watoto wanafukuzwa shule kwa kudai shilingi 50 peke yake, maana *management* ni mbovu na Serikali haitumii fedha za wananchi kwa kazi inayotakiwa kuifanya.

Kwa hiyo, naamini kabisa kwamba mpaka tutakapoondoa tatizo la rushwa, mpaka pale tutakapokuwa na nia na dhamira kamili ya kuwasaidia Watanzania ndipo tutakapojenga barabara. Kwa sababu Watanzania hawasafiri ndiyo maana wanaweza kudanganyika kwamba nchi yao ni nzuri sana kwa sababu hawasafiri. Ikifika jioni malori na mabasi yanasimama, hata *circulation* ya fedha ni ndogo sana. Kwa hiyo, wale ambao

wanaishi katika umaskini ambao ndiyo wengi, wanaingia, lakini fedha zao zinatumiwa vibaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, yangu ni hayo machache, nafikiri *message* imefika. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nina wajibu wa kusahihisha mambo. Mheshimiwa Mbunge ame-*refer* kifungu cha Katiba kifungu cha 25 (2) ambacho kinasema: "Bila kujali masharti ya ibara ndogo ya kwanza, hakutakuwa na kazi ya shuruti katika Jamhuri ya Muungano", lakini kifungu kidogo cha tatu kinasema: "Kwa madhumuni ya ibara hii na katika ibara hii kwa jumla ifahamike kwamba kazi yoyote haitahesabiwa kuwa ni kazi ya shuruti au kazi ya kikatili au ya kutweza endapo kazi hii kwa mujibu wa Sheria", ni kifungu cha (d)) "Kazi au huduma yoyote ambayo ni sehemu ya kwanza, majukumu ya kawaida ya kuhakikisha ustawi wa jamii. Ya pili, ujenzi wa Taifa wa lazima kwa mujibu wa sheria; ya tatu, jitihada za Taifa za kutumia uwezo wa kila mtu kufanya kazi kwa ajili ya kuimarisha jamii na uchumi wa Taifa na kuhakikisha maendeleo na tija ya kitaifa."

Kwa hiyo, Mheshimiwa Chacha Wangwe, anakumbuka makanisa yale mengine yanayosoma biblia msahafu mmoja halafu mingine wanaacha. Kwa hiyo, tusome msahafu vizuri. Tunaendelea. *(Makofi)*

**MHE. PAUL P. KIMITI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami niungane na wenzangu kukushukuru kutupa nafasi angalau tukachangia kidogo kwenye hoja hii muhimu ambayo tunayo kwa maendeleo yetu. Kabla ya yote, nataka nimpongeze Mheshimiwa Waziri pamoja na wasaidizi wake kwa kuleta Muswada huu ambao mimi naunga mkono asilimia mia kwa mia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naiunga mkono sheria ya barabara kwa sababu kubwa tatu. Sababu ya kwanza, imeandaliwa vizuri sana na walishirikishwa wadau mbalimbali ambao Mheshimiwa Wangwe anadhani wamesukuma watu ili kuleta mapendekezo yao. Tumekaa nao kwa siku tatu pale Dar es Salaam, kila mmoja ametoa mawazo yake na kwa taarifa yako wameomba ikiwezekana hata viwango vya fedha ambavyo vinatoza kwa ajili ya mafuta kwa barabara viongezwe. Hiyo, nashukuru.

Lakini la pili, naunga mkono kwa sababu Waziri alitumia kila aina ya msaada ili aone namna ya kuboresha Muswada huu. Alichofanya, amekubali masahihisho karibu 60 ambayo yalikuwepo katika Muswada wa awali. Ndio maana wale wanaopenda sana kufanya marekebisho safari hii kama Mheshimiwa Shellukindo, Mheshimiwa Dr. Slaa hakubadilisha chochote alichobadilisha, ni *"shall"* badala ya *"may"*, ndiyo maana nasema Mheshimiwa Waziri amefanyakazi nzuri sana. Nampongeza kwa kazi nzuri. *(Makofi)*

Lakini pia la ziada Mheshimiwa Waziri katika Muswada huu amejibu sana sera ya uchukuzi ambayo sisi tunadhani ndio muhimu na ndiyo dira ya maendeleo yetu. Mimi nimeshangazwa sana na baadhi ya maneno ambayo Mheshimiwa Mzee, namheshimu

sana, ndugu Chacha aliyoyasema nami nina haki kama Mbunge kusema ukweli wa mambo. Katika nchi zinazotuzunguka, hakuna nchi yoyote yenye barabara nyingi za lami na ndefu kama Tanzania. Tatizo letu ni ukubwa wa nchi. Tungekuwa na nchi ndogo, mngeshangaa kila Wilaya ingekuwa na lami. Mimi nasema ni vizuri tukafanya uchambuzi kabla ya kusema ndani ya Bunge hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bunge hili tunazungumza maneno wananchi wanatusikia, ni vizuri tukawa waangalifu kwa chochote tunachozungumza. Ndiyo maana nasema wakati mwingine sio vizuri kuzungumza ndani ya Bunge kama hujafanya utafiti wa kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nitaendelea kuunga mkono Muswada huu kwa sababu naona unajibu matarajio ya Watanzania. Sheria ni nzuri lakini yako mambo ambayo nadhani ni vizuri na sisi tukayawekea mkazo kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Serukamba ametuchokoza hapa, anasema sheria hii pamoja na uzuri wake, kama hatutatafuta mbinu ya kuongeza fedha kwenye bajeti, hatutapata kitu. Tutabaki tunalalamika, lakini hakuna lolote litakalofanyika katika Bunge hili. Kwa nini nasema hivyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, ukitegemea wafadhili kama *World Bank,* masharti yao kama tungeyategemea ya kusini ya kwenda Lindi, Mtwara isingejengwa ndugu yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hii ambayo ni ya *central corridor* hasa ukianzia hapa wenzetu kutoka Nzega uingie Singida uje mpaka Dodoma, hawakuona umuhimu wake, ni fedha zetu wenyewe ndio zimeanza kujenga hizo barabara. Ndiyo maana umuhimu wa kuwa na fedha kwa ajili ya barabara zetu wenyewe bila kutegemea wahisani lazima upewe kipaumbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, nalisema hili kwa sababu sisi tumeshaonja joto la jiwe. Mkoa wa Rukwa tuliwahi kutoa shilingi miaka ya 80 wakati Mheshimiwa Malecela akiwa Waziri Mkuu ili barabara yetu ya kutoka Tunduma kwenda Sumbawanga itengenezwe kwa kiwango cha lami. Kwa bahati Serikali ilitusikiliza ikasema, basi tutaanza na barabara ya vumbi na kweli wakajitahidi kampuni ya China *CETCO* ikaja ikaitengeneza vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini barabara ya vumbi ni vumbi hata ufanyaje, baada ya miaka mitatu, minne *back to squire one,* ukaanza upya. Lakini tukaambiwa kwamba bado baada ya miaka miwili mtengenezewe barabara, nikafuatwa baada ya miaka mitatu kweli ahadi ikatolewa ndani ya Bunge na mimi *record* ninazo ya kwamba tutaanza kutengeneza barabara kutoka Tunduma mpaka Ndalambo, kilometa 50 za kuanzia. Watu wa Rukwa wakashangilia sana ya kwamba ni hatua ya kwanza. Miaka 10 iliyopita hakuna lililofanyika, baada ya miaka miwili zaidi tukapewa ahadi ya kwamba barabara sasa itatengenezwa, kwa kuanza kutengeneza madaraja yote na kweli jitihada ikafanyika na Serikali. Nataka kuipongeza Serikali angalau nusu ya madaraja yalijengwa. *(Makofi)*

Mimi nasema tunawashukuru Serikali mliangalie hilo. Lakini la ziada tukaambiwa *World Bank* imetoa dola 34 milioni kwa kutengeneza barabara hiyo. Lakini zilipohamishwa hatukuambiwa hata kidogo na hii ni miaka mitano iliyopita, yote ni kwa sababu tunategemea, wafadhili ili watujengee barabara. Sasa ningemwomba Mheshimiwa Waziri atusaidie. Watu wa Rukwa sasa wamechoka na ahadi. Mheshimiwa Dr. Diodorus Kamala ni shahadi wangu, ametoka juzi kutembelea Mkoa wa Rukwa, wamesema wala usizungumze juu ya barabara zungumza mengine. *(Makofi)*

Oh! Itajengwa, wanasema hatutaki kukusikia. Mimi ni shahidi wangu. Kwa sababu wamefikia mahali fulani wamechoka na ahadi hewa. Nini kinafanyika, tunamwomba sana Mheshimiwa Waziri, tuliangalie suala hili kwa kutegemea mapato yetu wenyewe humu ndani na ndiyo maana tutake, tusitake, kama barabara zetu tunataka tuzijenge, njia ya kwanza ni kutafuta mapato yetu ya ndani kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni uamuzi wetu wenyewe kujenga barabara kwa kutumia shilingi bilioni 78 kwa mwaka tutajenga barabara moja tu labda ya kutoka Tunduma wala Sumbawanga haitafika na katika Ilani yetu ya Uchaguzi tumeoanisha barabara nyingi ambazo zitajengwa kwa lami kwa kipindi cha miaka mitano. Leo hata moja bado. Ndiyo tuko katika maandalizi. Nini? Tunategemea misaada kutoka nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani tuanze kuliangalia kwamba hili litaturudisha nyuma, makusudi mazima Serikali chini ya Rais wetu, Jakaya Mrisho Kikwete ni kuamua kwa dhati kufa na kupona, tutenge fedha zetu za kutosha kuanzia mwaka huu wa fedha kwa ajili ya kutengeneza barabara zetu hapa nchini. *(Makofi)*

La pili, nitamwomba Mheshimiwa Waziri anisaidie, tunayo taarifa katika Mkoa wetu ya kwamba kuna uwezekano wa kupata msaada kutoka *Millenium Development Challenge.* Hii tulikuwa tunaomba kama watakuja kujenga barabara katika Mkoa wa Rukwa wakagwe katika maeneo matatu.

Eneo la kwanza tupate mkandarasi ambaye atatoka Tunduma hapa katikati ya Laela. Mkandarasi wa pili atoke Laela kuja kuungana na mwenzake wa Tunduma na wa tatu atoke Sumbawanga kuja Laela. Kwa nini nasema hivyo, kwa sababu barabara ya kutoka Tunduma mpaka Sumbawanga ina kilometa 230 na hakuna Mkandarasi yeyote ambaye anaweza kujenga zaidi ya kilometa 30 za lami kwa mwaka. Ndiyo viwango vinavyotakikana ndiyo kusema ukimwacha mkandarasi mmoja akujengee barabara itachukua miaka nane kukamilisha barabara kutoka Tunduma mpaka Sumbawanga. Gharama hiyo tutaiweza?

Sasa lakini hawa wakiingia pamoja kwa kipindi cha miaka mitatu barabara itakuwa imekwisha. Ombi letu, lazima tuangalie namna sasa ya kuweza kujipanga upya ili kama inawezekana tuangalie uwezakano tozo inayotolewa kwa ajili ya mafuta Waheshimiwa Wabunge kwa kipindi cha miaka mitatu, minne ni shilingi mia moja tu kwa lita. Ni shilingi mia moja tu, hivi kweli tunashindwa kupitia Bunge hili angalau shilingi 50 tukaongeza au mia lakini barabara zetu zikatengenezwa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vizuri tukaisaidia Serikali kwa sababu wataalamu wanatuambia kila mnapoongeza gharama au bei kwenye mafuta mnaongeza *inflation* ya nchi. Sasa mnadhani itakuwa bilioni nadhani tukiongea hiyo bilioni 190 labda tuipate, ambayo tunaweza kufanya kazi mara tatu, tutafikia viwango vya angalau asilimia 80, 90. Hivi *inflation* yake ni nini? Watalaamu wanasema ukiongeza tu hata shilingi 50 *inflation* yake ni 0*.4 percent*. *Whati is 0.4 percent?* Ingekuwa *inflation 4, 5 percent* tungeomba lakini ni asilimia 0.4.

Mimi nadhani Waheshimiwa Wabunge tusaidiane, tuishauri Serikali tuone uwezekano wa kuongeza kidogo ili angalau barabara zetu zitengenezwe na angalau sheria yetu sasa ionekane sasa inaanza kutekelezwa katika misingi inayokubalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia na naomba Wabunge tuiunge mkono hoja hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. CYNTHIA H. NGOYE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba nikushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi nichangie machache katika Muswada huu mzuri wa barabara. Pili naomba kwa kuwa nilikuwa sijapata nafasi katika kipindi hiki kuzungumza naomba nizungumze kwa niaba ya wanawake wa Mkoa wa Mbeya, kutoa salaam za rambirambi kwa kifo cha aliyekuwa Waziri wa Afya wa zamani Dr. Aaron Chiduo, naamini familia yake itaendelea kupata tulizo la moyo na kumwombea na vile vile wananchi wa Gairo zamani alikuwa Mbunge wao. Mwenyezi Mungu aiweke roho yake mahali pema peponi. *Amin!*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya utangulizi huo, naomba sasa nijiekeleze kwenye Muswada. Nilitaka nizungumze kwa kuanza kabisa kuhusu sehemu ya pili kifungu cha saba, kifungu kidogo cha kwanza ambacho kilikuwa kinazungumzia suala la uundaji wa *Road Boards,* lakini bahati nzuri Waziri ametuletea masahihisho kwenye kifungu cha 7(b) ambacho awali Wabunge wa Viti Maalum walikuwa si wajumbe wa *Road Board* lakini katika masahihisho hayo ameongeza sasa anasema kutakuwepo na wajumbe wa Viti Maalum wasiozidi wawili. Lakini pamoja na masahihisho hayo mimi napenda nijiulize tu ni kwa nini wasiozidi wawili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini wasiwe wote, kwa nini Wabunge wa Viti Maalum wasiingie wote katika kikao hiki kwa sababu nina uhakika kabisa mawazo ya Wabunge wote katika Kikao hiki Wabunge wote yanafanana kabisa na mchango wao unafanana kabisa na Wabunge wa aina nyingine. Kwa hiyo, sifikirii kwamba kutakuwa na tatizo lolote iwapo kifungu hicho kingeweza kuzungumzia *composition* Wabunge wote wa Viti Maalum. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pili nilitaka nizungumzie kifungu cha 10. Kifungu cha 10 kinazungumzia kuwepo kwa Bodi ya Wizara. Bodi hiyo ya ushauri ya Wizara katika majukumu yake yaliyoainishwa pale mojawapo ni kusimamia kazi za barabara zote hapa nchini. Ni kazi nzuri na ni kazi muhimu sana na ni vizuri basi ipo hiyo Bodi ya kumshauri Waziri.

Sasa nilitaka tu kutoa ushauri wangu kidogo kwamba kwa kuwa Bodi hii inamshauri Waziri lakini vile vile inasimamia barabara zote hata zile za Mikoani, basi ikumbukwe kuishauri Mikoa hasa Mikoa inapopanga miradi ya barabara isizoeee tabia ya kupanga miradi ya barabara bila kushirikisha Halmashauri za Wilaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri za Wilaya ndizo ambazo zina watu na ni watumiaji wakubwa wa barabara. Ukishirikisha Halmashauri za Wilaya maana yake umeshirikisha watu, unajenga *sense of ownership* ya hizi barabara. Sasa unapokuwa wewe una-*impose* miradi, matokeo yake ndiyo hayo tunayoyaona kwamba wananchi wengine wanakuwa hawazijali barabara kabisa. Wanajaribu kuzungumzia kwamba hizi barabara ni barabara za Kitaifa au ni barabara au barabara za kimkoa, siyo barabara zao.

Kwa hiyo, katika suala la utunzaji wa barabara hizo inakuwa ni matatizo. Bodi hiyo ya Kiwizara ijaribu kuziagiza hizi Bodi za Kimkoa au Watendaji wa Mkoani, kujenga dhana ya ushirikishwaji katika upangaji wa barabara.

Pili, nafikiri kwa sababu hii Bodi, itakuwa ni kubwa na ni maarufu sana, naomba niiombe tu kidogo kwamba katika kipindi hiki cha miaka mitano naomba sana Serikali ijaribu kukumbuka ahadi ya Mheshimiwa Rais aliyoitoa kule Wilayani Rungwe Mkoani Mbeya kwamba barabara ya Katumba-Lusanje-Isange-Lwangwa-Mbambo mpaka Tukuyu, itajengwa kwa kiwango cha lami. Wote tulisikia hiyo ahadi na naomba Serikali kuanzia sasa iendelee kuiweka barabara hii katika *record* zake kwa sababu kuna wakati nilikuwa ninaangalia ahadi za Mheshimiwa Rais sikuiona hii barabara.

Naomba iingie kwenye *record* kwamba barabara hii iliahidiwa na Mheshimiwa Rais kwamba itajengwa kwa kiwango cha lami. Sasa isipowekwa kuna hatari kwamba sitasahauliwa. Bora iwekwe basi iingie katika utaratibu wa kuombewa fedha kama kawaida kama barabara nyingine na Mheshimiwa Rais alitembelea yale maeneo, aliona umuhimu wa barabara hii kiuchumi kwa sababu ya usafirishaji wa zao moja maarufu sana ambalo linazalishwa kwa wingi katika Wilaya ya Rungwe nalo ni zao la chai. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri naomba hilo lizingatiwe na liingie katika *record* za Wizara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka vile vile nizungumzie kifungu cha 9. Kifungu cha 9 kinaelezea makosa katika ibara zake za 48, 49 mpaka 50 kuna makosa mengine yanatajwa wazi wazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, makosa haya yanayofanyika katika barabara ni mengi sana lakini utashangaa watendaji wako, hamna hatua zinazochukuliwa. Nichukue mfano mmoja tu, mfano nazungumzia sehemu ile ya waharibifu wa barabara katika madaraja. Wakati mwingine kuna shughuli zingine zinafanyika za maendeleo hayo hayo, maendeleo labda uchimbaji wa mitaro ya maji. Hii mara nyingi mitaro ya maji inachimbwa na Halmashauri za Wilaya au za Miji. Mimi nafurahi amemshirikisha Waziri wa TAMISEMI katika suala hili la usimamizi wa barabara. Mara nyingi inapotokea kuchimba mifereji ya kupitisha maji katika madaraja au katika barabara kuu au katika barabara nyingine, mara nyingi kunakuwa kuna fidia tayari ambayo imeshatolewa. Lakini cha kushangaza utaona kwamba miezi na miezi inapita barabara imechimbwa, mabomba yametandazwa lakini hamna ukarabati wowote unaoendelea tena.

Kwa hiyo, mnaendelea kuruka tu kwenye mifereji, mnaruka kwenye mifereji kana kwamba hakuna fedha. Naomba sana hili suala Halmashauri za Wilaya izingatie. Nimefurahi vile vile kuonyesha makosa yanayotokana na wanyama. Inashangaza sana, pamoja na kwamba watumiaji wengi ni watu ambao wanafahamu sheria lakini utaona mara nyingi watumiaji wengi ambao wanaona mambo yanafanyika hawasemi kitu.

Kuna agizo liliwahi kutolewa na Wizara ya Mifugo, inayokataza kabisa kusafirisha wanyama hususan ng'onge kutoka *point A* kwenda *point B* kwa kutumia barabara na hasa hizi barabara za lami lakini mpaka hivi sasa utaona makundi haya yanaswagwa kwenye barabara za lami na siyo kwenye magari. Sasa matokeo yake kingo za barabara nyingi hasa za lami, nazungumzia hapa kuna barabara moja nzuri sana ilijengwa na makandarasi wa Kifaransa kutoka Uyole-Ibanda kuelekea Malawi, sijapata

kuona makandarasi wazuri kama wale, walijenga barabara moja imara sana na mpaka sasa ina zaidi ya miaka karibu 15 haijaharibika kabisa. Lakini huko kwenye kingo kumeanza kumegwa, megwa, kabisa na kunamegwa kwa sababu tunaruhusu wanyama wanapita katika barabara hiyo kwa kutumia utaratibu wa kuswaga. *(Makofi)*

Kwa hiyo, watalaamu lakini wapo wanaangalia. Sasa hapa kuna *commitment* ambayo inaonekana sasa kwamba tunaanza sura mpya. Maadamu sheria hii sasa imeandaliwa hivyo, Muswada huu tunaupitisha, basi na wenzetu wasimamizi wa barabara wabadilike, wasimie hizi barabara, haina maana yoyote kabisa kujenga barabara ambazo hazina msimamizi, hazina faida, haina faida kabisa. Kwa hiyo, napenda kusisitiza kwamba barabara *I mean* sheria hii ikitoka ni msumeno na sasa inaingia kusimamiwa na Waziri, Mwanasheria na makosa yameainishwa hapa na sasa usimamizi utakuwa mzuri na Waziri atakuwa mkali zaidi kuhakikisha kwamba miundombinu ya barabara zetu hapa nchini inatunzwa, inahifadhiwa vizuri iweze kudumu kwa miaka mingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, makosa yanayotajwa hapa ni mengi sana lakini naamini sana wanaosikia, watakaosoma sheria hii watazingatia haya yote ili tuweze kuzihifadhi barabara zetu hapa nchini. Kwa ujumla wake ukiangalia sheria hii kwa kweli ni nzuri tena fasaha kabisa, ndiyo maana tunaposimama hapa wengi tunachangia, hatumalizi hata dakika. Kwa sababu ya ufasaha wa uandishi wa sheria hii. Naamini wote tutaungana pamoja katika kuhakikisha kwamba sheria hii itapitishwa na kwamba itakapoanza kutumika basi sisi wote tutakuwa *over seas* ikiwa ni pamoja na Wizara yenyewe na Wabunge kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo machache na mchango huo mfupi, naomba sasa nitamke kwamba naunga mkono huu asilimia mia moja. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:**Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie Muswada huu muhimu na ningependa kusema kwamba naunga mkono na nampongeza sana Waziri pamoja na Manaibu Mawaziri kwa Muswada mzuri walioleta na ni Muswada muhimu sana kwa Watanzania. *(Makofi)*

Ningependa kusema kwamba bila barabara hakuna uchumi. Kwa hiyo, barabara ndiyo nyenzo ya uchumi na ningependa kuwaunga mkono Wabunge wenzangu waliosema kwamba tutafute namna ya kupata fedha za barabara. Hii asilimia 30 inayogawanywa kwenye Halmashauri zote na urefu wa barabara za nchi yetu ilivyo haitakaa ikatosheleza hata siku moja, itakuwa tunagombana kila siku. Kwa hiyo, ningependa kusema kwamba naungana na wenzangu kwamba hivyo vyanzo vyote viongezwe ili tuweze na sisi tukaweza kupata fedha kwanza za kugawana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, ningependa nimweleze Mheshimiwa Waziri kuhusu barabara iliyoko kwenye Jedwali hili ambalo nimeshangaa sana. Hii barabara ya Monduli Juu - Ketumbene. Mimi nadhani imekosewa, kwa sababu ilikuwa ni Monduli Juu-Ketumbene-Longido. Ukiacha Longido hii barabara haitakuwa na maana kabisa. Kwa sababu Ketumbene iko katika Wilaya ya Longido. Ukitoka Monduli Juu

kwenda Ketumbene usipoenda Longido ina maana kisiasa kwanza ni mbaya sana kwangu. Kwa sababu watu wa Ketumbene hawaendi Monduli Juu na watu wa Monduli Juu hawaji Ketumbene. Watu wa Ketumbene wanakwenda Longido na magari yanayopita yanayotoka Tarafa ya Ketumbene ni zaidi ya magari 20 yanayokwenda Longido kila siku.

Barabara ya kutoka Ketumbene kwenda Monduli Juu kwa kweli naweza kusema inaweza kama magari matano yatapita kwa mwezi ni bahati. Sasa kilichotokea barabara imeanza kujengwa, naulizwa kila siku, hivi Mbunge hii barabara inayotengezwa mkaacha hii tunayopita kila siku ni kwa nini, na mimi sina jibu. Bado nawaambia kwamba barabara inazunguka kuja mpaka Longido ndiyo watakuelewa kidogo. Kwa hiyo, naomba sahihisho na naomba kama barabara kama haitafika Longido ambayo ndiyo Makao Makuu ya Wilaya nasema hiyo barabara mtakapotengeneza, mtatengeneza, ikiisha hakuna magari yatakayopita, haiwasaidii wananchi wa Ketumbene, itakuwa ni barabara ambayo baadaye itafutika haitakuwepo.

Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri, bahati nzuri Waziri Mkuu anafahamu sana hii barabara na nadhani ananiunga mkono kwamba barabara iwe barabara Monduli Juu - Ketumbene - Longido. Isipokuwa hivyo, msitumie fedha za wananchi bure kwa sababu hakuna barabara. Naomba iwekwe kwenye Bunge hili hili iwekwe Longido ndiyo itakuja vizuri. *(Makofi)*

Ningependa kusema kwamba hiyo barabara imepandishwa hadhi, Mkoa umepandisha hadhi hiyo barabara muda mrefu. Kuna barabara zingine ambazo tulisema kwamba sisi Mkoa ipandishwe hadhi, barabara kutoka kule Rombo nadhani mnafahamu historia ya Rombo na Longido bado naisubiri tu bahati nzuri nina mashahidi wawili hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nina Naibu Waziri wa Miundombinu, na Waziri wa Mazingira, wamezunguka wote Mlima Kilimanjaro, ukizunguka Mlima Kilimanjaro unakuta barabara ya lami kutoka Rombo mpaka kijiji kinachoitwa Kamwanga ambayo ndiyo kijiji cha kwanza kuingia Wilaya ya Longido na lami ikaishia hapo hapo, ikawa *corrogation,* sasa sisi tumeunganisha kutoka barabara hiyo, hiyo barabara ya lami mpaka Namanga iwe ni barabara ya Mkoa, haikuandikwa hapa.

Ningependa kusema kwamba naomba Wizara, Mheshimiwa Waziri uandae majibu mazuri kabla ya Bajeti ya barabara kutoka kwenye barabara ile ya lami inaishia Kamwanga uandae majibu mazuri sikuulizi leo, lakini uandae majibu mazuri kwamba Kamwanga ni nini? Kwa sababu hiyo barabara itakuja tu kuwa na *sense* nzuri ikiitwa Rombo mpaka Sanya Juu, ndiyo itakuwa barabara ya lami inayosaidia Watanzania lakini ikiishia Kamwanga, sijui kwanza inakuja nini katika kijiji changu, sijui hii nitanyamaza kwanza. Kwa hiyo, ningependa kusema kwamba tungeomba majibu baadaye kwa sababu hiyo barabara ina matatizo. *(Makofi)*

Jambo lingine ningependa kutoa tena sahihisho kwenye hili hili Jedwali. Nadhani ni makosa, Mto wa Mbu-Ketumbene. Halafu Ketumbene-Ngaleserwa nadhani hiyo

barabara ni ile inayokwenda Loliondo, sasa hii Mto wa Mbu-Ketumbene hiyo barabara haipiti Ketumbene. Ukisema Ketumbene watu watakushangaa kwamba hivi barabara hii inapita wapi, msituletee matatizo, maswali makubwa tuulizwe na wananchi mbona hii barabara Mto wa Mbu-Ketumbene kwa nini haijafika Ketumbene, inapita mbali sana na Ketumbene.

Kwa hiyo, mfute Ketumbene muandike Mto wa Mbu-Engaruka halafu Engaruka-Ngareselo, nadhani hiyo ndiyo itakuja, italeta *sense.* Msiniletee matatizo, hii ni barabara ya lami, wala haipiti kwangu, inapita Mto wa Mbu-Engaruka halafu Engaruka-Ngareselo sasa mnaweka nini Ketumbene, Ketumbene iko wapi na iko mbali sana na Ketumbene, kwa hiyo naomba ifutwe au kama ni kupitisha ninaweza tu ikapita ikaenda Gareselo.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine nataka kuzungumzia ni mradi uliosemekana mradi wa magadi ambayo, nadhani asubuhi ilizungumzwa kwamba reli ya Arusha itaimarika tu endapo magadi itapatikana *Lake Natron.* Sasa *Lake Natron,* iko kwangu na hapo mnaposema *Lake Natron* ni kijiji tunachoita magadi. Sasa mnapoandaa mradi na watu waliopo hapo hawajapewa taarifa hata siku moja ni makazi ya watu, nyie mnaandaa mradi halafu baadaye mnawashitukiza tu kama mwewe kwamba hameni. Msitoe matatizo mengine ya Ihefu, kwa sababu hapo ni makazi ya watu, halafu kama ni magari halafu barabara hii isipite Longido na mradi upo Longido, tawashangaa sana naomba kama kuna mradi pale hiyo barabara ya mkoa iitwe Longido Ketumbene, Igalesewa ambayo hiyo Igalesewa ndiyo kuna magadini, ndiyo *Lake Natron. Lake Natron* inagawa Wilaya mbili, Wilaya ya Longido na Wilaya ya Ngorongoro. Kama ni kutoa magadi pande zote kuna magadi, lakini naomba sana hao wananchi waanze kuarifiwa, hao wananchi waanze kuelezwa na manufaa watakayopata hapo baadaye, sio kuwahamisha tu. Tukisema kwamba ni faida kwa Taifa, ni faida kwa hao walioko pale nao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nakushukuru sana kunipa nafasi, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. BENITO W. MALANGALILA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa napenda kukushukuru sana wewe mwenyewe kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kutoa mchango katika Muswada huu. Awali ya yote kwanza ningependa kumpongeza ndugu yetu Mheshimiwa Mtutura Abdallah Mtutura kwa kushinda kwa kishindo kuwa Mbunge wa Jimbo la Tunduru. *(Makofi)*

Pia ningependa kutoa pole kwa wananchi wa Jimbo la Gairo na familia nzima ya Marehemu Dr. Aaron Chiduo, kwa kufiwa na ndugu yao Dr. Aaron Chiduo ambaye alikuwa Mbunge mwenzetu hapa na pia alipata kuwa Waziri wa Afya.

Kimsingi niipongeze sana Wizara ya Miundombinu, kwa kuleta Muswada huu ambao mimi binafsi nimeusubiri kwa muda mrefu na kwa miaka mingi sana. Wananchi wa Jimbo la Mufindi Kusini nao pia waliusubiri kwa hamu kubwa na kwa muda mrefu pia. Kama sote tunavyofahamu umuhimu wa barabara, barabara kwa mwili wa

mwanadamu unaweza kusema ni mishipa ya damu maana yake mwanadamu kama hana mishipa ya damu hawezi kuishi, huo ndiyo ukweli wenyewe. *(Makofi)*

Sasa tumekuwa na taratibu nyingi, mifumo mingi sana ya kutumia fedha zetu katika matengenezo ya barabara, nakumbuka miaka ya nyuma huko kulikuwa na makambi na wafanyakazi walikuwa wanawekwa katika makambi hayo kwa ajili ya kutengeneza barabara mara tu inapokuwa imeharibika. Lakini sielewi ni nani aliyekuja kurekebisha kwamba barabara zote itabidi tuzitengeneze kwa kutumia wakandarasi tu. Sasa mimi nadhani hapo ndipo tulipokuja kupotea njia.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli wakandarasi tunaweza kuwatumia katika barabara kubwa lakini *region roads* au hizi barabara ndogo ndogo zinazopita vijijini ni vizuri sana kwa maoni yangu tukawatumia wananchi katika kuhakikisha kwamba kazi ndogo ndogo kama kuziba mashimo, kufukua mifereji, wananchi wanapewa kandarasi hizo. Maana yake tunaelewa kabisa kwamba tunatumia mabilioni mengi sana na kama pesa hizo tungezitumia kuwaajiri wananchi wa vijijini kwanza zingesaidia sana hata kupigana vita dhidi ya umaskini. Watu wangepata pesa hapo na barabara zetu nina hakika zingekuwa nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, maana yake makofi yote haya ina maana Wabunge hawa wanaunga mkono wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kupigiwa makofi haya, nimesema kwamba awali mimi nilikuwa na mategemeo makubwa sana na Muswada huu, kwa sababu Mawaziri siku zote nikizungumzia barabara ya Nyigo - Mgororo, wanatuambia hamna shaka, utakuja Muswada ambao barabara ya Nyigo - Mgororo itakuwa *inclusive,* lakini nasikitika tena kwa uchungu mkubwa sio mimi tu na wananchi wote wa Mufindi Kusini, kwa nini barabara ya Nyigo - Mgororo haimo katika *schedule* hii? Mheshimiwa Michael Laizer amesema anasubiri wakati wa Bajeti, leo ameamua ananyamaza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli inatia uchungu sana, barabara ya Nyigo - Mgororo, ina kilometa 60 na inakwenda katika kiwanda kikubwa kabisa cha karatasi katika Afrika. Mwekezaji yule analalamika sana kwamba anapata bidhaa nyingi kutoka Malawi, Zambia, sasa ukitoka Nyigo mpaka Mgololo ni kilometa 60, kwa hiyo, inabidi asafiri kutoka kule Mgololo aende Mafinga kilometa 80, atoke Mafiga mpaka Nyigo kilometa 70, jumla kilometa 150 wakati barabara ya Nyigo - Mgololo ni kilometa 60, sasa naiomba sana na wananchi wa Jimbo la Mufindi Kusini, wanaiomba sana Serikali ikubali kuichukua barabara ile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nifanye *quotation,* mwezi Desemba mwaka jana, Serikali yenyewe ilitoa taarifa katika hii karatasi ya ubinafsishaji na aliyetembelea pale moja ya watu waliotembelea pale alikuwa ni ofisa wa Benki ya Dunia, anaitwa Vedasto Rwechugura.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba ruhusa ni nukuu maneno aliyosema mtaalamu huyu wa Benki ya Dunia. Meneja wa kiwanda kile analalamikia sana juu ya hii barabara ya Nyigo - Mgololo na yule mkuu wa Benki ya Dunia wa Tanzania alisema nini napenda

kunukuu; “kwa mfano mmezungumzia ubovu wa barabara, Benki ya Dunia haiwezi kufadhili ujenzi wa barabara hiyo mpaka hapo itakapohusishwa katika mipango ya Serikali na kuufanya mradi huu kama moja ya miradi inayohitaji ufadhili wa Benki ya Dunia.”

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hivyo hata Benki ya Dunia yenyewe imeona kwamba barabara hii ni muhimu sana, kwa nini Serikali yetu haioni? Na mimi kama Mbunge kwa miaka 12 sasa barabara hii nimeanza kuiulizia toka siku ya kwanza ya Ubunge ndani ya Bunge hili, sasa kwa nini wenzangu hamtaki kunielewa? Kiwanda hiki ni kiwanda kikubwa mno, kiukubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuthibitisha, ningeomba Waziri wa Miundombinu atembelee, mimi nitaungana naye tukitembelee kiwanda kile, kiwanda kikubwa ajabu, kinaajiri zaidi ya wafanyakazi 2000, lakini hawana barabara, nadhani kwa haya machache, unajua kabla hatujaanza kikao hiki huwa tunaomba dua maana yake tunamuomba Mungu awepo hapa, naamini hivi anasikia maneno haya na huwa tunamalizia kwa kusema amina na mimi nasema amina kwa maneno niliyoyasema hapa, jioni hii ya leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, unajua mimi namshukuru sana Mungu kwa sababu kwanza amenipa hekima katika kulizungumzia suala hili, unajua mtu unapofanya kazi yako miaka kumi na mbili, haikuzalii matunda, hivi unafanya nini? Unaongelea jambo hilo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, unajua, sisi wakristo tuna kitabu chetu kinaitwa *biblia,* kinasema kwamba yuko mtu mmoja alikuwa maskini, lakini mtu yule kila siku alikuwa anamwendea yule tajiri, yule tajiri alikuwa katili hataki kumsikiliza mtu yeyote, lakini kila anapomgongea ngo ngo ngo, naomba unisaidie mkate, yule tajiri anasema nikusaidie maana yake nini, ngo ngo ngo, mwisho akasema basi mpe tu bwana maana yake kila siku ananisumbua. Sasa mimi nitaendelea kuwasumbua suala hili mpaka lini? *(Kicheko/Makofi)*

Mimi nadhani kimsingi Serikali Mheshimiwa wetu mpendwa kabisa, Rais Jakaya Kikwete, amechagua watu wenye akili nyingi, watu werevu, watu waelewa, naamini kabisa kwamba suala hili wamenielewa na suala hili tumekwishaelewana.*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia sisi kule Mufindi tuna barabara yetu moja inaitwa Mufindilu, barabara inaanza pale Mafinga inakwenda Kibao, inakwenda Igole halafu inarudi Nyororo, *is the same circle road,* ilikuwa kilometa 80, barabara iko kweli, Serikali inajitahidi kutengeneza, lakini barabara hii iko *very busy* yaani inashughuli nyingi sana ndiyo inabeba chai yote na ndiyo inabeba mbao hizi kubwa, hizi *soft wood* zote asilimia 60 ya mbao tunazotumia Tanzania zinatoka, zinapitishwa na barabara hii, asilimia 67 ya chai ya Tanzania yote inapitia barabara hii. Kwa hiyo, hii barabara muhimu sana. Sasa sisi tulivyokaa katika bodi ya Mkoa, tulipendekeza barabara hii iwekwe lami, ni barabara ya vumbi, wewe jaribu kufikiria yale malori makubwa kabisa yanabeba magogo tani 60 barabara ya vumbi, itastahimili vipi uzito mkubwa namna hii?

Kwa hivyo, ili iwepo angalau ina maana kila baada ya miezi mitatu utakuwa unagharamia, ili angalau tuhakikishe kwamba tumetatua tatizo hili, naiomba Serikali kwa dhati kabisa kwamba iweke barabara hii moja kati ya barabara za lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimezungumzia sana habari ya Mufindi, ningependa kumuunga mkono ndugu yangu Mheshimiwa Paul Kimiti, yule Mbunge wa Sumbawanga Mjini, kwa kweli watu wa Sumbawanga wana adha kubwa sana ya barabara na kwa sababu Mheshimiwa Paul Kimiti amesema Serikali iliwahi kutoa bilioni 34,000 za dola sijui ngapi? Sasa Serikali ituambie hizo pesa ziko wapi, ni hakika wananchi wa Sumbawanga wanataka kujua hizo pesa zao walizokuwa wamehesabiwa ziko wapi? Unajua Mheshimiwa Paul Kimiti, ni mwanasiasa wa siku nyingi, huwa hapendi kuuliza maswali makavu makavu, kama ninavyouliza mimi. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini naomba hata hivyo naomba nimalizie kwa kusema naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia katika Muswada huu wa Barabara uliowasilishwa Bungeni leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu umekuja kwa wakati ni muhimu sana na kwa kweli kuziboresha barabara zetu, kwanza kutufahamisha, kwa sababu tulikuwa wengi hatuzifahamu barabara zetu zinakuwa katika maeneo, zinakuwa katika madaraja gani. Sasa tumeweza kufahamu barabara zetu zimewekwa katika madaraja gani na urefu wake ni kiasi gani, pamoja na kwamba si barabara zote zimewekwa hapa lakini hiyo inatupa mwanga walau kuona kwamba kitu kizuri basi kimeletwa kwa ajili ya kufanyika kupata maamuzi ya Bunge hili Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesimama kwa lengo la kutaka niunge mkono hoja hii, kwa hiyo, ninayo machache ambayo nitayazungumza katika Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, miongoni mwa mikoa yenye mvua nyingi, Mkoa wa Kagera ni mmoja ambao una mvua nyingi katika kipindi cha mwaka. Unakuta kutokana na mvua hizi nyingi hapo zinapokuwa zimekwisha mvua, msimu wa mvua kwa kipindi hicho, basi unakuta barabara zote kimsingi zimeharibika zile ambazo zinatengenezwa kwa udongo, moramu ya kawaida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nilichokuwa naomba, niliomba katika utengenezaji wa barabara pengine ungejaribu kuangalia tofauti ya barabara hizi kulingana na hali ya hewa tuliyo nayo kutoka mkoa hadi mkoa, kwa sababu kuna mikoa mingine ambayo inapata mvua chache kwa mwaka. Kwa hiyo, kuna mahali ambapo barabara inaweza ikadumu walau kwa miezi nane, hata kwa mpaka miezi kumi. Kwa sababu mikoa inayopata mvua kwa mfano kwa miezi minne tu kwa mwaka, kwa kipindi kama cha miezi miwili wanakuwa hawana barabara. Lakini miezi kiasi kama kumi wanaweza kuwa na barabara, lakini kwa mkoa kama wa Kagera unakuwa na mvua karibu miezi nane, kwa hiyo, hata mimi sielewi, mkandarasi atatengeneza barabara hizi kwa wakati

gani? Kwa sababu mara nyingi ni mvua, mvua ikiacha kunyesha ni wiki moja, ikiwa ni muda mrefu ni wiki mbili.

Kwa hiyo, katika barabara zinazotumika sana, unakuta mara nyingi baada ya mvua kumekuwa barabara zote zimeharibika, kwa hiyo, nilikuwa naombi hilo kwamba iangaliwe namna ya kutenga pesa ili kuhakikisha kwamba barabara zote zinaweza kupitika vizuri kwa muda wote katika nchi nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini lingine nililokuwa naomba liangaliwe ni kuangalia pengine *competence* ya wahandisi hao wanaokwenda kujenga barabara zetu, wanaokwenda kusimamia hasa ujenzi, ili kusudi ile *competence* yao isaidie katika kusimamia hii tofauti ya barabara hizi. Kwa mfano mkoa wa Kagera barabara nyingi zina udongo wa mfinyanzi na ziko katika mabonde makali na baada ya bonde kunakwenda kutokea daraja, kunakuwa na mto lazima kuwekwe daraja. Sasa sisi tusiofahamu sana vigezo, unashangaa kunakuwa na kona kali wakati unakwenda kuishia kwenye daraja na halafu kuna mwinuko mkali.

Mimi nilidhani pengine, baadhi ya barabara ambazo zilikuwepo mapema kabla ya kupimwa, pengine zilitengenezwa na wananchi baadaye zikaingia katika vigezo vya barabara hizi tunazozizungumza, ingekuwa ni vizuri zikazingatia vigezo na kuzingatia usalama wa mahali. Lakini atakayeweza kuyaona hayo ni aina gani ya Mhandisi ambaye tumekuwa nae. Kwa hiyo, nilikuwa naomba hiyo mikoa yenye aina hii ninayoieleza basi ingekuwa vizuri kama wangeweza wakapata wahadisi ambao wana sifa za kutosheleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kingine ambacho nilikuwa naomba katika suala hilo hilo, ni kwamba mameneja wa *TANROAD* wawe karibu sana wahandisi wetu wa Halmashauri za Wilaya. Kwa sababu barabara hizi zinapita katika Wilaya na hizi sio *truck road,* mara nyingi zinakuwa ziko kwenye *highway* kwa maeneo ya kwetu, natoa mfano wa mkoa wa Kagera. Kwa hiyo, nakuta mara nyingi ambaye anaweza akatoa taarifa haraka na nini kinachoendelea ni yule Mhandisi wa Wilaya.

Kwa hiyo, ni vizuri basi Meneja wa *TANROAD* akawa karibu naye ili kuweza kusaidia hata kumpa taarifa na ufuatiliaji. Wakati wanapochonga barabara mara nyingi wanasema hawataki wanaingiliwa na Wahandisi wa yale maoni yanayoelekea. Lakini mimi nadhani wakati mwingine inatoa nafasi pengine ya kujenga sio katika viwango vizuri zile barabara. Ni vizuri pale barabara inapopita yule mhandisi wa mahali pale naye akawa karibu kuweza kutoa mawazo yake na kuchangia kuona barabara ile inakuwa kwa kiwango gani.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii inaenda pamoja na mgawanyo wa fedha, sijui zinaitwa za mafuta, *fuel level* huu mgawanyo wa asilimia 70 kwa asilimia 30, ukweli wenyewe unaendelea kuipa nafasi barabara za mikoa, lakini hautoi nafasi nzuri kwa barabara za Wilaya. Kwa hiyo, mimi nilikuwa naomba kwamba hili lingeangaliwa kwa sababu barabara nyingi zinapoendelea kupata lami, ni kwamba barabara nyingi zinabaki ni za udongo ambazo nyingi zinaendelea kuwa chini ya *council* na *council* zinakuwa na kiasi kidogo cha pesa, kwa hiyo, unakuta kwa kipindi kirefu barabara zinakuwa ni

chakavu na kama hatuna barabara za *council* hazikukaa vizuri, hata namna ya kufika katika barabara nzuri, *truck roads* pamoja na barabara zile za mkoa bado inakuwa ni vigumu na mimi ningeliomba hili likaangaliwa ili likaweza kusaidia katika utunzaji wa barabara zetu, hao wakawa na ushirikiano wa eneo kwa eneo. Badala ya kuona hii barabara inajengwa na mkoa basi yule Mhandisi wa Wilaya anaona hausiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ninalopenda kuzungumzia mimi niliite pengine usalama wa barabarani au usalama wa vyombo vya barabarani na watumiaji wengine. Kunaudhibiti wa mwenendo barabarani, ni kitu kizuri, lakini unakuta alama zile za barabarani zina matatizo mengi, kwanza nataka nitolee mfano wa barabara ninazoziona mara kwa mara, unakuta kuna barabara inayokwambia pale mbele kuna tuta, lakini tuta lile utaliona kama bado kiasi kama cha mita kumi, kumi na tano kufikia lile tuta.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii inategemea barabara ile inaruhusiwa kwenda kwa mwendo gani? Kama ni *highway* unashtuka kwa vyovyote hakuna gari inayokwenda kwenye *highway* kama sio mbovu, gari itakuwa chini ya *speed* ya 100. Ni kwa kiwango gani ambavyo katika mita kumi na tano gari linaweza likafunga *break* na likapunguza mwendo kuweza kufikia mwendo ambao unafaa kupita kwenye matuta na haya yako sana katika barabara ya Dodoma, Dar es Salaam, nilikuwa naomba suala hili liangaliwe sana, hizi alama zirekebishwe, alama ziwekwe katika kiwango kinachotosheleza kuweza dereva ku-*control* gari lake kwenda katika mwendo mzuri, hapa nazungumza kama dereva ambaye anaendesha katika hii barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapata matatizo makubwa sana namna ya ku-*control* mwendo katika barabara yetu hii. Kwa hiyo, mara nyingi unakuta kuna namna mbalimbali ambazo zinaweza zikasababisha ajali ambazo sio za lazima hata uharibifu wa gari ambavyo haikuwa ni lazima. Sasa sielewi kwa magari ambayo ni mazito zaidi yanawezaje kupunguza mwendo, mara nyingi mazito hayana mwendo mkali lakini bado hata hizi zinawahusu namna ya kupita mle barabarani. Lakini bado unakuta pia humo barabarani kuna alama zingine ambazo ni za kuzingatia, kwa mfano hapa kuna mifugo inapita, hapa kuna wanafunzi wanapita au watu wengi na kadhalika. Hizi alama za barabara kama zinakuwa ni karibu sana sio rahisi kwa mwendeshaji kuzizingatia.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hizo alama, nadhani wananchi wanahitaji elimu zaidi, sielewi huu wizi wa alama hizi za barabarani hasa za vyuma umeongezwa na kasi ya ununuaji wa vyuma, sielewi. Basi nilikuwa naomba ziangaliwe hizi alama kusudi ziweze kuwa na manufaa kwa watumiaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, utoaji wa leseni uangaliwe, madereva wengi wanaoendesha magari ya *automatic,* kuendesha magari ya *manual* kwa kweli sio rahisi mpaka wajifunze tena na leseni ziangaliwe ili kuondoa hizi ajali ambazo nyingine sio za lazima. Dereva wa *manual* anaweza akiji-*switch* kwenye *automatic* kwa sababu ni rahisi atapata shida kama kilometa moja baada ya hapo ataendesha vizuri. Lakini wa *automatic* kwenda *manual* ingeangalia hata wakati wa kutoa leseni, kusudi mtu aliyejifunzia kwenye gari lile anapotoka kwenye *automatic* anapotaka kwenda gari la *manual* apate tena elimu kusudi aweze kuwa dereva mzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho ninalopenda kulizungumza nilikuwa na *classification* ya barabara, katika Muswada haukuonyesha barabara zile ambazo zinaishia kwenye Ziwa zinapewa sifa gani, kasoro barabara chache sana. Barabara zote zinaelekea Ziwani, kwenye Maziwa, hasa katika nchi ya Tanzania zinaishia katika mikoa mingine ama katika nchi jirani, lakini barabara zote hizi unakuta zimewekwa kwamba ni barabara ambazo ni za Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa naomba barabara hizi zingeangaliwa, kwa mfano na barabara napenda niseme barabara ya Izigo Kyamki katika jimbo la Muleba Kaskazini, inaishia Ziwani na hii Kyamki ni gati ambayo sasa hivi Serikali inaitafutia pesa ili kuiboresha. Kwa hiyo, inaweza kutoa huduma katika Ziwa Victoria, sasa ukitoka pale unapoelekea, unaelekea Mwanza na ukikata kulia kushoto kwako zaidi unaelekea Uganda, kwa hiyo, barabara hii inayo sifa ya kuwa ni barabara ya mkoa. *(Makofi)*

Lakini vile vile iko barabara ya Kagoma Lwazi, vile vile inasifa hiyo hiyo, lakini katika vile vile katika Wilaya ya Misenya iko barabara katika jimbo la Mkenga, inatoka Katoma, inapitia Kanyigo inakwenda Bukwale. Bukwale ni Ziwani ikipita pale inakwenda Kasheshero, lakini unakuta barabara hii inahudumiwa na Halmashauri na barabara hii iliwahi kuwa na bandari lakini sasa hivi hilo limetoweka na hata inastahili kuwa na kivuko na hivi Halmashauri haziwezi zikamudu gharama hizi za kuendesha barabara kama hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara nyingine inayofanana na hiyo ni barabara moja inayotoka Kyela kupita kwenda mpaka *Itungi Port,* barabara hii inahudumiwa na Halmashauri ya Kyela, lakini ukitazama hii inaishia kwenye Ziwa Nyasa. Barabara ya Mkoa inayotumiwa na mkoa inatoka Dar es Salaam inaelekea Kasumulu, lakini inapokuwa imeharibika hao wanarudi kupita tena kwenye barabara hii ya Kyela ambayo ni Halmashauri. Sasa hapa gharama za utengenezaji, mkoa hauji kuwasaidia, sasa haya ni mambo ambayo nilidhani kwamba ni wakati muafaka wakati Mheshimiwa Waziri atapokuwa katika nafasi yake ana *classify* na kui-*classify* barabara zake, aangalie hizi barabara ambazo zimekuwepo zinazokwenda kuishia kwenye Ziwa kwamba si barabara ambazo hutazipandisha kwa namna nyingine zaidi ya kwamba zinatoa huduma katika Ziwa ambalo ama linapakana na nchi nyingine ama linapakana na mkoa mwingine ndani kwa Ziwani humo humo.

Mimi nilikuwa napenda kusema kwamba hili liangaliwe vizuri, kusudi barabara zetu zisionekane tu kwamba zinaendelea kuwa ni barabara za Wilaya kwa sababu eti inaishia Ziwani haiuganishi mkoa, haiuganishi nchi, hapana, hizi barabara za Maziwa zote zinaunganisha mikoa na zinaunganisha nchi. Kwa hiyo, nilikuwa naomba hilo liwekwe katika marekebisho yatakayokwenda kufanyika ya mara kwa mara anayoyafanya Mheshimiwa Waziri, kwa mamlaka anayopewa na Muswada huu. *(Makofi)*

Lakini vile vile mazingira yanatofautiana, barabara za mkoa wa Kagera zinapokwenda kufikia Ziwani yaani zinakuwa na mteremko mkali sana, kwa hiyo, yaani mvua moja tu barabara yote haipo. Sasa Halmashauri inapesa ngapi? 30% haiwezi

ikamudu kufanya barabara hizi zikawa katika hali nzuri ambayo inapitika kila wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi na niseme nimeomba ziangaliwe barabara zenye mvua nyingi na makandarasi wawe ni wenye ujuzi na pesa vile vile liangalie hilo kusudi barabara zetu zipitike, lakini vile vile nimeomba udhibiti wa mwendo wa barabarani uangalie pia na aina ya madereva na alama zile za barabarani ziangaliwe sio tu zinawekwa walipoziweka basi wakazisahau. Lakini la mwisho nimesema ama zilizoishia katika Ziwa zinastahili kuwa ni barabara za mkoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii, narudia kusema naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**MHE. BALOZI DR. GETRUDE I. MONGELLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi nichangie Muswada huu. Kwanza kabisa naomba nichukue nafasi hii na mimi kuungana na wenzangu Waheshimiwa Wabunge katika kutoa rambirambi kwa familia ya aliyekuwa Mbunge mwenzetu mstaafu Dr. Aaron Chiduo tunamfahamu kwa kazi yake nzuri aliyotumikia Taifa na Mungu aiweke roho yake mahali pema peponi. *Amin!*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Mtutura Abdallah Mtutura, Mbunge wa Tunduru,

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu wa Sheria ya Barabara wa mwaka 2007 ni Muswada ambao umekuja kwa wakati, naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri wa Barabara (Miundombinu) ambaye ameleta Muswada huu mbele yetu. Kawaida huwa napenda kufanya masahihisho madogo madogo lakini masahihisho haya hayapo kwa sababu nadhani mwenye kuhusika ni mzoefu sana katika kuandaa sheria, kwa hiyo, ninampongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu umekuja tukiwa na miaka minne tu mbele yetu kabla hatujafikisha miaka 50 ya Uhuru na miaka minne itafika wakati tunamaliza kipindi chetu cha awamu hii ili tukijiandaa kuingia katika kipindi cha miaka mitano ambayo tumeomba ridhaa ya wananchi. Kwa hiyo, ni kipindi kizuri kabisa kupitisha Muswada kama huu ili tuweze kuufanyia kazi, mimi nikieleza matatizo niliyonayo na barabara ni mengi mno, kwanza nina barabara za aina mbili, barabara ya maji na barabara za udongo. Hizi barabara leo tunazungumzia barabara za udongo za ardhini natumaini kuna siku tutazungumza barabara za majini ambazo kwa kweli Mungu ametupendelea hazihitaji kifusi wala lami, zinahitaji tu vifaa vya kusafiria na ningependa niseme tu kwamba katika barabara hizi suala kubwa ambalo limefanywa na sheria hii tutakayoipitisha na naomba niunge moja kwa moja mkono ni ile *classification,* hatujawahi kuwa na *list* ya *classification* ya kwamba Waheshimiwa Wabunge tukaweza kusoma barabara yangu hii iko katika *grade* hii na *grade* ile kwa pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Wilaya yangu ya Ukerewe tuna kilometa 300 za barabara kwa sababu tulikuwa na ma-*chief progressive* na *chief* wetu alinunua gari katika mwaka 1903 tulikuwa na gari katika Wilaya ya Ukerewe, kwa hiyo, ikatusaidia watu kupenda barabara na miungombinu.

Sasa ninayo mengi ya kulalamika kwa nini barabara ya kutoka Bunda - Kisolya, Lugesi kupitia Mulutungulu kwenda Serema, Bukongo, Nansi na kurudi mpaka Nansio si ya lami, ningeweza kulalamika mwaka jana, Mimi natoka Mkoa wa Mwanza, nimetizama ramani ya barabara inatisha, mkoa wenye samaki, mkoa wenye dhahabu, mkoa wenye kila kitu bado ukiangalia ile ramani ya Mwanza yaani utashtuka na Mheshimiwa sasa ni Waziri sitaki kusema mengi alipiga kelele juu ya barabara ya Usagara - Geita na mkoa mzima tukaunga mkono kwa sababu ile ina-*connect,* ingeitwa hata *International Road,* ingevushwa hata ikafika *International Road* na kukawa na ahadi kwamba itatengenezwa hatujaona matengenezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nasema kama ni kulalamika tu malalamiko ninayo mengi kweli lakini nimekuja kugundua kitu kimoja, hivi pesa zipo? Pesa hazipo kwa hiyo, suala la Muswada huu kama tunaupitisha ni lazima tukubali kuzitafuta pesa, nadhani *that is the bottom right,* tusipokubali kwamba tutafunga mkanda tutafute pesa, mimi nataka kusema siku zote tunasema wafadhili, nimeenda kwenye nchi za wafadhili wanatusaidia kwa sababu wamekubali kujipiga kodi, pesa haziokotwi uende London ukakuta furushi la pesa, uende Marekani ukakuta furushi la pesa, uende Norway ukakuta furushi la pesa na mahali tunakoenda kutafuta pesa wanaweka makusudi ya kwamba tutajipiga kodi ili tuweze kutoa misaada hii tunayoitoa baada ya kutengeneza kazi zetu humu ndani. Hivi kwa nini sisi tupate kigugumizi cha kusema sheria hii ipite katika bajeti Waziri alete namna tutakavyojipiga kodi ili tuboresha barabara hizi, bila kuboresha barabara hata siku moja uchumi wa nchi hii hautaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa tuna hiki kitu kinaitwa *Rift Valley Fever* wengine wanakita *RaAV4* na ukiangalia ni kwamba tusingepaswa kubabaika kwa kutokula nyama, tuna samaki wa kutosha kutoka Ziwa Nyasa, tuna samaki wa kutosha kutoka Ziwa Tanganyika, tuna samaki wa kutosha kutoka Ziwa Victoria tatizo ni miundombinu ya barabara ambayo ingeweza kutoa hao samaki kuja kufidia katika maeneo ambayo hawana Maziwa. Sasa ndio maana mimi nasema Bajeti ya mwaka 2007/2008 lazima ionyesha kodi na sisi Wabunge tushiriki kuelimisha umma ya kwamba tusipojipiga kodi hizi hatutaweza kujenga barabara ya lami na hatutaweza kujenga uchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Waziri nadhani utakubaliana na mimi wakati unajibu hoja zako kwamba utaleta *a serious list of taxation* itakayokupa pesa na ukipata barabara za Ukerewe unazifanya *International* kwa sababu zinatoka Ukerewe zinaelekea Kisumu na Entebe, kwenu ninyi mnaona maji si barabara, sisi *is just a connection, another mode of transportation*.

Kwa hiyo, mimi siwezi kukudai kupita kiasi kama hatujaweza kuzipata hizo pesa kwa hiyo, tusaidiane na Serikali kodi zitakapokuja siyo tena tupinge, tunapiga kelele kila mtu anataka barabara yake iwe ya lami, Waziri apate wapi pesa? Mimi nitaunga mkono kodi zitazoletwa lakini zikiletwa basi naomba katika kifungu kile cha *audit which means financial technical and management audit* kifanyika vizuri, zamani tulikuwa na *search audit* tulikuwa na *PWD* watu walikuwa wanatania wanasema punda wengi duniani, lakini hivi vilikuwa ni vikosi vya ku-*monitor* barabara kila mahali na tukawa na barabara safi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini katika hiyo *audit* Waziri afikirie kurudisha hiyo *unit* ya *inspection* ili zile pesa tunazozitumia na nitakazozipiga kodi ziweze kutumika na barabara zetu ziweze kudumu. Kwa hiyo, Waziri hiyo ni *homework* ndogo ninakupa ya kurudisha hii *audit* ile *way* ambayo tuliizoea kuhakikisha kila mahali kuna watu wanapita kukagua na hao watu sasa waende hatua moja mbele, wanaweza kuwa chini ya *TANROAD* lakini *TANROAD* hawezi kuwa mtengeneza barabara na huyo huyo akawa mkaguzi nadhani hii ingekuwa chini ya Wizara yenyewe ya kwamba iweze kukagua na kutupa *value for money*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna kipengele kimoja ambacho kimenifurahisha katika Muswada kinaitwa *nuisance,* kipo katika kifungu cha 51 yaani maudhi barabarani. Maudhi yale yaliyoorodheshwa ni sawa lakini mimi naomba niongeze mengine maudhi ya walevi kutembea kwenye *highway* ni *nuisance* kupita kiasi lazima tuweke sheria, niliona Singapore wanasheria ukiyumba tu kwa kulewa unafungwa, lazima tufike hapo kwa sababu *accident* nyingi zinatokana na hawa wanaotembea kwenye *highway* wamelewa wanayunga.

Mheshimiwa Naibu Spika, *another category of nuisance* ya maudhi barabarani ni wale wanaokaa kwenye ukingo wa barabara eti wanazungumza, wale nao ni maudhi matupu wanasababisha wale wanaoendesha barabarani kubabaika na wakati mwingine wanakatisha wakati dereva hakuwa amejiandaa kufanya hivyo. Kwa hiyo, *this is a nuisance* naomba iongezwe hayo maudhi na kuwa na taratibu za kuwachukulia hatua hawa watu wanaolewa wanatembea barabarani, hawa watu wanaoamua kufanya *sitting room* yao iwe kwenye ukingo wa barabara. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo nilitaka nisisitize mimi nimependekeza kuwa na kodi ya kuleta pesa za kutosha na wakati Bajeti nitasimama na nitataka nihakikishiwe kwamba Wizara hii imetengewe pesa za kutosha au sivyo tunawapa *headache* wanaohusika na Wizara hii tunawadai lakini hakuna pesa za kutosha na hii barabara ya Usagara - Geita kesi hii haijaisha, bado ipo mezani kama hatujaona tunapimwa kitu au tufanye nini basi ili kuonyesha ya kwamba Waheshimiwa Wabunge wa Mkoa wa Mwanza na mimi nikiwa Mwenyekiti wao walipokuwa wanasisitiza suala hili wamepuuzwa, tupo bado. Kwa hiyo, ikifika kwenye bajeti kama hili suala la Usagara, Geita halijapata majibu mazuri tutapata tabu pamoja na kuunga mkono kwenye kuleta kodi ya kuongeza pesa lakini zile pesa basi zilizotengwa mwaka huu ziko wapi? Zile za Usagara, Geita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo ninaomba niishie kwa kusema kwamba kwa kweli Muswada huu umefika kwa wakati, miaka minne tu kabla ya kufikia miaka 50 ya Uhuru wetu tukitekeleza haya na tukiongeza Bajeti tutaweza kujivuna na kuonyesha baadhi ya miradi mikubwa ambayo tutasema nchi hii imekuwa huru kwa miaka 50. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba nikushukuru sana kwa kunipa nafasi jioni hii na mimi nichangie katika Muswada huu muhimu kabisa lakini kama ilivyo ada naomba nitoe salaam za pole kwa msiba wa aliyekuwa Mbunge Dr. Aaron Chiduo na nimpe pongezi ndugu yangu Mheshimiwa Mtutura Abdallah Mtutura na nimkaribishe Bungeni. Nianze kwa kusema kwamba ninaunga mkono Muswada kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ni siasa, barabara ni uchumi, barabara ni maendeleo, bila barabara hakuna maendeleo, uchumi wala hakuna chochote kitakachofanyika. Mimi nilikuwa naomba nishauri kama ifuatavyo, tunalo tatizo la usimamizi wa hizi barabara zetu zinazojengwa, wenzangu wamesema kwamba tutafute pesa sawa lakini je, pesa zinapotafutwa na barabara zinajengwa ule usimamizi unasimamiwa na hawa wasimamizi, je, wanakuwepo *site* kuthibitisha yale waliyokubaliana katika mikataba? Kwa sababu ukiangalia barabara zetu pamoja na pesa nyingi zinazotolewa ule ubora ni hafifu kweli, ubora haupo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaweza tukapata pesa nyingi kutoka nje lakini kwa sababu tatizo la usimamizi lipo basi hata hizo pesa hazitaweza kufanya kazi yake vizuri, naomba sana Serikali chini ya Waziri wa Miundombinu kazi ya usanifu inapotaka kuanza basi wale wataalamu wasanifu kama inavyotakiwa. Lakini wakati wa ujenzi wa barabara husika na maeneo husika kama walivyoeleza wenzangu kwamba kwa sababu barabara zinatofautiana, ardhi ina tofauti kwa maana ya udongo basi wale wenzetu waainishe kwamba udongo huu unatakiwa ujengwe lami kwa kiwango fulani. Kwa kufanya hivyo tutaepuka yale matatizo ambayo tunaona kwa sasa, mfano barabara yetu ya kutoka Morogoro kuja Dodoma leo imeshaanza kudidimia, ni kwa sababu ya kutokuwa makini katika usimamizi na tumetumia pesa nyingi lakini usimamizi ni hafifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya kutoka Mwanza kuja Shinyanga *boarder,* Mheshimiwa Waziri nenda leo kaitazame utasikitika na kushangaa na tunaambiwa kwamba imetumia karibu shilingi bilioni moja lakini ule ubora wa barabara haupo, barabara imeshaanza kuharibika lakini zipo barabara nyingi, naomba sana usimamizi iwe ni suala la msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia naomba nizungumzie barabara yangu ya kutoka Magu - Kwimba - Jojiro mpaka Nabugi, nilishaomba, niliuliza swali humu ndani na nikajibiwa lakini bahati nzuri leo tena Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Kwimba, Mheshiwa Bujiku Sakila aliuliza swali. Si vizuri sana kwa Serikali yangu ambayo ninaijua ni Serikali sikivu na inajua kupanga vizuri kuwa kila siku Mbunge asimame kusema neno hilo hilo, haileti picha nzuri. Tunaposema humu ndani nia yetu ni kwamba Serikali inasikia, sasa Serikali kama inasikia basi yale ambayo sisi tunayaomba si lazima

kwa mwaka huu kama siyo Bajeti ijayo basi baada ya miaka miwili au mitatu basi liingizwe angalau hata kama ni usanifu tu, kwa mfano leo tungeshukuru na inawezekana kwenye Bajeti ijayo tutaambiwa kwamba barabara ya kutoka Magu mpaka Mabuki usanifu wake imetengewa kiasi fulani cha pesa, kwa kweli tunaomba Serikali isikie na hilo ilipokee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kufanya hivyo utakuwa umefungua uchumi wa Wilaya ya Magu, Wilaya ya Magu nafikiri ni Wilaya ya zamani kuliko Wilaya zote kwa maana hiyo Magu imezaliwa Kwimba, Misumbwi imezaliwa Kwimba na Maswa. Sasa naomba sana Mheshimiwa Waziri alichukue hili. Lakini pia hivi karibuni niliuliza swali kuhusu ujenzi wa Daraja la Mto Simiwi, nashukuru Serikali ilitoa majibu mazuri lakini nilipendekeza na ninaomba na *Hansard* ya leo nayo isome lakini naomba kupendekeza na kuiomba Serikali kwa sababu chanzo kikubwa cha pesa ambacho kilitamkwa na Serikali kwa maana ya Wizara ni shilingi milioni 450 kwa kweli ni pesa nyingi na mimi nakubali. Basi naiomba Serikali kwa mwaka ujao wa fedha 2007/2008 itenge angalau kiasi cha shilingi milioni 50 kwa ajili ya kazi ya usanifu, kwa kufanya hivyo tutakuwa tumeshaanza hatua moja mbele ili baadaye mwaka ujao wa fedha 2008/2009 kiasi cha shilingi milioni 450 kitengwe kwa ajili ya ujenzi wa daraja hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini lingine ni kwamba miji yetu ya Mwanza, miji yetu ya Arusha, miji yetu ya Dar es Salaam ikishafika saa za usiku hakuna taa katika barabara zetu, kwa nini? Tunaambiwa kwamba kwa sababu gharama ni kubwa kwa hizi Halmashauri au Manispaa, ninaiomba Serikali tuondokane na kutegemea umeme wa maji twende kwenye *solar, solar* ni kitu ambacho kinawezekana na ikiwezekana itasaidia hata kupunguza msongamano wa magari mara taa hizi zinapozimika lakini nina uhakika tukitumia *solar* hata ile gharama ya uendeshaji itapungua, Mji wa Mwanza unakua lakini ili mji upendeze ninaiomba Serikali kuweka taa, ni aibu tunapotoka *Airport* Dar es Salaam mpaka unafika mjini Mwanza muda wa usiku ni giza tupu, hakuna taa. Sasa naomba Serikali kwa hizi barabara ambazo ni za Wizara naomba ziwe na taa ikiwezekana kwa bajeti ijayo *solar* ziwekwe ili tuondokane na kutumia hizi taa za kawaida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini lingine ni suala la ushirikishwaji ambalo limetamkwa na mwenzangu, barabara hizi ni zetu na tuna mfano mzuri wa shule za msingi, tuna mfano mzuri wa shule za sekondari kwa sababu tumewashirikisha wananchi, wananchi wanaona kwamba shule zile ni mali yao na katika ujenzi wa barabara tunaomba wananchi washirikishwe ili waweze kuzilinda hizi barabara. Mtakuwa mnaweka hizi alama za barabarani kama wananchi hawashirikishwi mtakuta ile alama imetolewa kwa sababu wananchi hawakushirikishwa lakini kama endapo wananchi watashirikishwa nina uhakika hizo alama za barabarani hazitachukuliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo nakushukuru na ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**MHE. SULEIMAN A. SADDIQ:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia Muswada huu muhimu, Muswada ambao

ninaweza nikasema umechelewa. Awali ya yote naomba kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu na Naibu wake kwa kutuletea Muswada huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara za nchi yetu hali yake naona wenzangu wameizungumza, wenzangu wamegusia maeneo mbalimbali na maeneo mengine naona wamenifilisi. Mimi naomba nianze na suala la *TANROAD,* wenzetu wa *TANROAD* wana jukumu kubwa sana katika kuhakikisha kwamba barabara hizi wanazisimamia katika ngazi ya mkoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, *TANROAD* kutokana na jukumu kubwa walilopewa mimi ningeishauri Serikali hususan Wizara yenyewe kuwa karibu na *TANROAD* na ikiwezekana jicho la Serikali kupitia Wizara husika liwe jirani sana *TANROAD,* yapo mambo ambayo yanasimamiwa na *TANROAD* yamekuwa mazuri lakini yapo mengine bado tunaweza tukasema hayajafikia lengo ambalo limekusudiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hili nizungumzie zaidi ubora, ndio maana nimesama jicho la Serikali liwe karibu. Ubora wa barabara zinazotengenezwa chini ya *TANROAD* nyingine hazina sifa, nitaje moja kwa moja ni barabara ya Wilaya ya Mvomero inayowekwa lami kutoka Sangasanga kwenda Chuo Kikuu cha Mzumbe.

Mheshimiwa naibu Spika, ile barabara kilikuwa ni kilio cha muda mrefu cha jumuiya nzima ya *Mzumbe University,* barabara ile ilikuwa ni kilio cha muda mrefu cha wananchi wa Kata zile za jirani na Mzumbe, Mlali na Mgeta yenyewe lakini ubora wa barabara ile kwa kiwango cha lami haulingani na fedha zilizotolewa na Serikali kwa hiyo, mimi naungana moja kwa moja na wenzangu walizungumzia suala la ubora wa barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ipo haja sasa hivi ya kushirikishwa kwa Halmashauri za Wilaya ili *TANROAD* nayo iweze kufuatiliwa kwa makini zaidi, wenzetu wa *TANROAD* wanafanya kazi zao kwa utaratibu wao na sisi Halmashauri tunafanya kazi kwa utaratibu wa Halmashauri lakini jambo ambalo mimi naliona hakuna masharikiano ya pamoja kati ya Halmashauri na *TANROAD,* unaweza ukatoka Wilayani unakwenda kwenye Makao Makuu ya Kata ukakuta barabara ya Mkoa inatengenezwa chini ya *TANROAD* lakini bado tatizo likawa linajitokeza kwamba hujui barabara ile msimamizi wa *TANROAD* ni nani, anayefuatilia kazi ile ni nani na matokeo yake unaletewa malalamiko kwamba barabara ile ya Mkoa haina ubora unalingana.

Sasa Mbunge ukizungumza utaambiwa unafuatilia watu wa *TANROAD,* Mbunge ukisema sana unaambiwa hukufuatilia mambo ya ndani sasa haujashirikishwa mambo ya ndani utafuatilia saa ngapi? Naomba Wizara itoe maelekezo kwa *TANROAD* waanze kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya katika miradi ya barabara za Mikoa zilizopo ndani ya Wilaya husika, huo ni ushauri wangu wa kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu wa pili ni suala la fedha. Fedha ambazo zipo sasa hivi ni kwamba zote zinatoka Serikali Kuu zinagawanywa katika asilimia, asilimia ambayo Halmashauri inapata ni fedha ndogo ukilingana na wenzetu wa

*TANRAOAD* lakini matatizo makubwa yapo vijijini, vijijini ndiko tunakoambiwa tuhimize kilimo, vijijini tunaambiwa tuhamasishe wananchi wafungue *SACCOS,* vijijini ndiko ambako sisi unasimamia wananchi waweze kujikwamua na wimbi la umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa fedha zinazokuja vijijini ni ndogo ukilinganisha na fedha zinazoenda kwenye barabara za mikoa, hili wenzangu wamelizungumza na mimi ni wajibu wangu kuligusia.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niingie kwenye barabara ambayo ni kichocheo cha uchumi katika Taifa letu, barabara ya kutoka Korogwe, Mziha kupitia Turiani, Mvomero, Magole hadi Mikumi. Hii ni barabara ambayo zamani ilikuwa inapitika muda mrefu sana na barabara hii bahati nzuri katika Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2005 imeainishwa kwamba ni miongoni mwa barabara zitakazowekwa lami. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, bahati nzuri mgombea wa Urais alipokuja katika Wilaya ya Mvomero kuomba kura aliwatamkia wazi wananchi wa Wilaya ya Mvomero iwapo Serikali ya CCM itaingia madarakani na yeye atakuwa Rais wa nchi yetu kwa kipindi hiki cha miaka mitano barabara ile itawekwa lami.

Ombi langu kwa Wizara husika ni kwamba nawaomba wataalamu, Waziri mhusika na wengine wote kazi hii ningeshauri ianze mapema. Ni barabara ambayo inaweza ikasaidia nchi yetu inapopata matatizo hususan ile barabara ya Chalinze - Segera, hii inaweza ikawa ndio barabara mbadala lakini bado ni barabara ambayo inaweza ikaunganisha Bandari ya Tanga na Mikoa yote ya Kanda ya Ziwa, unaweza ukatoka Tanga, ukatoka Arusha, ukatoka Kilimanjaro ukapitia Turiani, Mvomero ukaingia Dumila ukaelekea Dodoma hadi Mwanza ni barabara ambayo bado ninasema inahitaji kufanyiwa kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, namuomba Mheshimiwa Waziri kabla ya Bunge la Bajeti angefanya utaratibu wa kutembelea barabara hii ili aone ni jinsi gani magari yanavyopita, aone ni jinsi gani barabara hii inavyoweza kutumika na inavyosaidia uchumi na kwa siku moja ni magari mangapi yanatoka Korogwe, Handeni hadi Turiani na Mvomero ataona kweli barabara hii ipo haja ya kupatiwa ufumbuzi wa haraka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada kusema hilo sasa naomba niingie kwenye barabara ambazo ni za Mkoa. Katika Wilaya ya Mvomero kuna barabara tatu za mkoa, barabara ya kutoka Langali hadi Sangasanga, barabara ya kutoka Mvomero hadi Muscat na barabara ya Magole - Turiani, Mziha.

Mheshimiwa Naibu Spika, hizi barabara za mkoa kila mwaka ukipiga kelele barabara yenye urefu wa kilometa 80 bajeti inayotoka ni milioni 40 au milioni 50. Fedha zile badala ya kusaidia na kuleta ufanisi na kuondoa kero matokeo yake hazisaidii sana, barabara ya kilometa 80 inatengenezwa kilometa mbili au tatu. Namuomba Mheshimiwa Waziri kwa Bajeti hii inayokuja angeweka kipaumbele barabara hizi za mikoa angalau

kwa asilimia 50 ya fedha zinazoombwa ili tuweze kujiandaa mapema mno kwa suala zima la kuwaondolea wananchi kero yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, langu la mwisho katika hili ni jinsi ya kupata fedha za barabara. Mimi naendelea kuuungana na wenzangu kuhusu suala la kuangalia ni vipi tutaweza kupata fedha za kupata mapato zaidi katika barabara. Suala la fedha ambazo zinatokana na *fuel levy* bado mimi nafikiri iko haja ya kuliangalia tena, ipo haja ya kuangalia tena.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika miezi sita iliyopita mafuta yalipanda bei *taxi,* daladala na mabasi yakaongeza nauli, miezi miwili iliyopita mafuta yakashuka bei lakini gharama zikawa ni zile zile sasa utakuta huu mfumuko wa bei ya mafuta ambayo inapanda karibu kwa shilingi 200 au shilingi 150 kwa lita bado haujaleta nafuu yoyote katika nchi yetu, nafuu ambayo ipo inawaendea wafanyabiashara wa sekta ya usafirishaji. Mimi ningeiomba Serikali iweke utaratibu mzuri.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Suleiman Ahmed Saddiq, kwanza *declare interest* zako.

**MHE. SULEIMAN A. SADDIQ:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na ku-*declare interest,* mimi bado nipo katika hoja ya barabara na fedha kwa ajili ya nchi yetu.

Mimi ni mfanyabiashara wa mafuta lakini bado naona kwamba tatizo lililopo katika sekta hii ni kwamba bei za mafuta zinashuka lakini wananchi hawafaidiki na ushahidi upo kwamba bei za mafuta zinashuka na wananchi hawafaidiki, bei za mafuta zikipanda wananchi wanaumia kwa maana ya gharama za usafirishaji zinapanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nafikiri hapo nimeeleweka vizuri, nia yangu ni kuisaidia Serikali katika eneo hili, naiomba Serikali iweke utaratibu mzuri zaidi wa kuona ni jinsi gani tutaweza kutengeneza barabara zetu kupitia *fuel levy* ambayo tunaweza tukaiongeza hata ikiwezekana kwa 100% kutoka kiwango kilichopo sasa hivi ili mradi barabara zitengengezwe. Hiyo ndiyo hoja yangu.

Hoja yangu ya mwisho katika Muswada huu ni hizi barabara ambazo zimeainishwa humu ambazo moja kwa moja zipo chini ya usimamizi wa Halmashauri ya Wilaya, naomba wenzangu wamezitaja kwa majina na muda hautoshi inaonekana barabara nyingine hazikuguswa wala hakutajwa.

Ningeomba Wizara iangalie uwezekano wa kuwasiliana na Halmashauri moja kwa moja na mimi kwa kuwa Muswada huu na barabara nyingine zimetajwa na nyingine hazikutajwa hizi nitakwenda nazo kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Mvomero. Zipo barabara ambazo zinaweza zikasaidia kuunganishwa na barabara za mkoa ili zilete ufanisi mkubwa zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Yono Stanley Kevela, unaweza kupata nafasi ukipenda kwa dakika 12.

**MHE. YONO S. KEVELA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naona nijaribu kutumia hii dakika 12 ingawa nilikuwa na mambo mengi kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nichukue nafasi hii kukupongeza na kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia huu Muswada kwa dakika hizi 12. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu spika, cha kwanza, napenda nimpongeze sana Mbunge wa Tunduru, Mheshimiwa Mtutura Abdallah Mtutura, halafu kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Njombe Magharibi napenda kutoa pole na rambirambi kwa wafiwa kwa kifo cha Dr. Aaron Chiduo, poleni sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho napenda kutoa pole kwa wafiwa kwa ajali ya gari la *Buffalo* iliyotokea mkoani Kilimanjaro.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa vile muda ni mchache niingie kwenye hoja ambazo zinanikera, hoja ambayo inanisumbua sana na kuhusu suala la barabara ambazo ziko kwenye Jimbo la Njombe Magharibi yaani barabara za Saja, kwenye Kata ya Saja barabara kwa kweli nimejaribu kuziangalia hakuna barabara zilizoandikwa nyingi sana na kule kwa kweli kilio kikubwa cha wananchi wangu wamenituma kwamba hata viongozi kwa bahati mbaya hata wa Kitaifa kufika kule imekuwa ni nadra kwa sababu ya tatizo la barabara.

Pia nichukue nafasi hii nizungumze kuhusu suala la Halmashauri, kuna tatizo pale Halmashauri, Halmashauri zetu hela zinazopewa ni kidogo na siwezi nikalalamika sana kwa sababu niko pembezoni kwamba barabara zangu zinasahaulika lakini tatizo ni kwamba pale Halmashauri fedha zinazopelekewa *through* TAMISEMI ni kidogo sana.

Kuhusu suala la Njombe Magharibi, mimi ninaposimama hapa kwa kweli nasimama kama Mbunge wa Njombe Magharibi yaani maeneo ya Ilembula, Wanging'ombe, Mdandu, Imalinyi nazungumza hivi kwa sababu sehemu kubwa tunasahaulika, barabara nyingi kwa kweli hazipitiki na ninasema hayo kwa sababu sina jinsi ni lazima nizungumze, nilitakiwa nikae kimya na nishukuru vile vile kwamba pamoja na kwamba kuna kipindi hapa Bungeni nilizungumza kwamba baadhi ya viongozi wa Kitaifa kwa vile ni mbali na Wilaya ya Njombe na Mkoa wa Iringa imekuwa ni vigumu sana kututembelea watu wa Njombe Magharibi lakini nashukuru Mwenyezi Mungu baadhi ya Mawaziri wa Kitaifa wamefika kipindi hiki kwa mfano Mheshimiwa Prof. Mark Mwandosya , naona alifika pale, akaja Waziri wa Maji alifika pale namshukuru. *(Makofi)*

Lakini bahati mbaya Waziri Mkuu alianzia kwenye Majimbo ya wenzangu alifika pale Njombe Mjini na pale Makambako labda kwa sababu ilikuwa ni pembezoni

alishindwa kufika pale Ilembula lakini tuliahidiwa kwamba ataweza kufika tu. Kwa hiyo, nalo ni kilio lakini nadhani tatizo lilikuwa ni barabara, barabara kule hazipitiki ni mbovu kwamba Mkuu wa Mkoa kumpangia kule pembezoni au Mkuu wa Wilaya pengine aliona ni tatizo, kwa kweli hicho ni kilio chetu kwamba tutembelewe waone hali halisi, kuna mashimo, barabara ni mbovu tumesahaulika pamoja na kwamba uchumi tunao wa kutosha wa alizeti na viazi mviringo, tuna mifugo ya kutosha kule Saja kwa hiyo, tulikuwa tutashukuru kwamba Serikali yetu itafikiria kwamba itafanya hali ambayo ni ya usawa siyo kwamba itaishia sehemu chache tu za mjini kwa watu wenye uwezo watafika na sehemu ambazo tuna hali ambazo siyo nzuri.

Vile vile pamoja na haya malalamiko lakini nishukuru vilevile kuna barabara tayari wenzetu wametukumbuka kwa mfano kuna barabara ambazo Serikali imejitahidi kutusaidia kwa mfano kuna barabara ya kutoka Njombe kupitia Iyai kwenda Mbeya imetusaidia, kuna barabara za Mlevela-Mdandu zimetusaidia. Lakini kilio kikubwa kingine ambacho kimesahaulika ni hili daraja la Matoo.

Mheshimiwa Naibu Spika, daraja la Matoo, Ilembula ni tatizo. Kuna mkandarasi alikuwa anajenga mwaka juzi lakini kwa sababu ya *poor tendering* yule Mkandarasi imebidi a-*disappear* kimaajabu ajabu kwa hiyo, kuna mkandarasi mwingine akasababisha hasara kubwa ya Serikali lakini yule mtu hajachukuliwa hatua. Kingine ni kwamba yupo mkandarasi pale lakini anasuasua sasa hii kwa kweli tulikuwa tunafikra kwamba *tender* ile *Procurement Act* yaani sheria za manunuzi zifuate mkondo wake kwenye upande wa barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine ambacho nakiona kwamba kwa kweli kuna haja ya kutumia utaalamu sasa hivi kwamba tusiwe tunachagua mkandarasi yeyote tu, kuna wakandarasi wazuri wa kizalendo lakini wale wakandarasi wazuri wa kizalendo inatakiwa waendelezwe na inatakiwa wapewe mafunzo kwa sababu kwa kweli wanaileteа hasara baadhi lakini siyo wote wanaweza wakaleta athari kubwa sana kwa ajili ya *poor tendering*.

Halafu nilitaka nizungumzie kuhusu suala la faini. Nimeangalia kwamba kuna faini mtu akifanya makosa isipungue shilingi milioni moja au kifungo kisizidi miaka mitatu, sasa mimi nataka nijikite upande wa hizi zabuni kwamba hawa wanaotoa *tender* baadhi siyo waaminifu, wanachagua *tenderers* ambao siyo wazuri.

Kwa hiyo, wale watu inatakiwa nao wapewe kifungo kisichozidi walau miaka sita au faini isiyopungua miaka 10 kutokana na uzito wa barabara hizi kwa sababu barabara hizi zina mabilioni ya fedha, sasa mtu amechagua mtu ambaye ni mbovu tena pengine wakati fulani kwa sababu ya kitu kidogo, kwa hiyo, mtu kama yule inatakiwa kwa kweli afungwe au apewe adhabu kubwa ili iwe fundisho kwa wengine na watu wawajibike sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya naona nisiwachoshe Waheshimiwa Wabunge, nawashukuru sana kwa kunisikiliza na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge orodha yetu bado ni ndefu sana na hata pamoja na bidii zote kuna wachangiaji 16 waliobaki na kesho kutwa kama mnafahamu kwamba baada ya maswali kutakuwa na uchaguzi wa Wawakilishi wa Chuo Kikuu. Basi hata hivyo watakaozungumza kesho hawatazidi nane, orodha itakuwa kule kwenye ubao wetu kwa hiyo, anayefikiria kwamba ameomba basi akaangalie kule.

Baada ya hapo ningependa kutangaza Chama cha Wanawake Wabunge kesho saa mbili asubuhi watatembea na wale wageni, Wabunge wa Denmark kwa hiyo, tumechagua Kamati ya Utendaji na Kamati iliyoshughulikia *Strategic Plan* ndiyo wahudhurie hiyo, itakuwa saa mbili asubuhi chumba namba 231.

Wahaohusika ni Mheshimiwa *Engineer* Stella Manyanya, Mheshimiwa Balozi Dr. Getrude Mongella, Mheshimiwa Susan Lyimo, Mheshimiwa Cynthia Hilda Ngoye, Mheshimiwa Pindi Chana, Mheshimiwa Grace Kiwelu, Mheshimiwa Janet Kahama, Mheshimiwa Eliatta Switi, Mheshimiwa Zaynab Vulu, Mheshimiwa Fatma Mikidadi, Mheshimiwa Shally Raymond, Mheshimiwa Bernadeta Mushashu, Mheshimiwa Esther Nyawazwa na Mheshimiwa Kidawa Hamid Salehe. *(Makofi)*

Halafu baada ya hapa tu tumealikwa kule kwenye maonyesho na tafrija iliyoandaliwa na *Zantel* katika eneo letu la kawaida, kutakuwa na chakula cha jioni na mambo mengine yatakayokuwepo pamoja na muziki na vinginevyo mtaviona. Kwa hiyo, wote mnakaribishwa.

Baada ya kusema hayo naomba niwashukuru sana kwa kazi nzuri tuliyofanya kwa siku ya leo kwa hiyo, naahirisha kikao mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 01.44 jioni Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Alhamisi, Tarehe 19 Aprili, 2007 saa tatu asubuhi)*